# ISAYA.

SO
LI
DEO
GL
OR
IA

ZANZIBAR, 1882.

Digitized by Google

Original from
HARVARD UNIVERSITY

# ISAYA.

NJOZI ya Isaya mwana wa Amoz, aliyoi-
ona juu ya Yuda na Yerusalemi, siku
za Uziya, Yotham, Ahaz, Hezikiya, wafalme
wa Yuda.
2 Sikieni, Ee mbingu, upokee masikioni,
Ee inchi, kwani Yahuwa amenena. Nime-
3 lea nikalisha watoto, nao wameniasi. Ng'o-
mbe amjua mwenyewe, na punda pakuli-
sha pa bwana wake, Israeli hajui, wa-
4 tu wangu hawafikiri. Ole wa taifa lenyi
thambi, watu waliolemewa na maovu, wazao
wa wabaya, watoto waharibuo, wamemwa-
cha Yahuwa wamemtia hasira Mtakatifu wa
Israeli, wamerudi zao nyuma.
5 Kwa nini mpigwe tena? Mtazidi kuasi,
kitwa chote kigonjwa, moyo wote umezimia.
6 Toka uayo hatta kitwa hakuna mzima, ma-
jeraha na machubuko, na madonda yaliyo-
oza, hayakufumbika, wala hayakugangwa,
7 wala hayakulainishwa kwa mafuta. Inchi
yenu imeharibika, miji yenu imeteketezwa

Digitized by Google
Original from HARVARD UNIVERSITY

na moto, makoonde yenu wageni wameyala
machoni penu, yakaharibika, yakaangami-
8 zwa na wageni. Na binti Sayuni ameachwa
kama kibanda katika mizabibu, kama kili-
ndo katika shamba la maboga, kama mji uli-
9 ozungukwa. Kama Yahuwa wa majeshi
hangalituachia sisi mabaki yaliyo machache,
tungalikuwa kama Sodoma, tungalifanana
na Gomora.

10 Sikieni neno la Yahuwa, mtawalao Sodo-
ma, mpokee masikioni sheria ya Muungu
11 wetu, enyi watu wa Gomora. Wanifaa nini
wingi wa thabihu zenu? amesema Yahuwa,
Nimeshiba na kafara za kondoo, na shahamu
ya vinono, wala sikupenda damu ya ng'o-
mbe, wala waana kondoo, wala mbuzi.
12 Mkija kuonekana mbele yangu, nani aliye-
litaka hili mkononi mwenu mkanyage nyua
13 zangu. Msilete tena sadaka za uwongo,
buhuri ndiyo inichukizayo, miezi na sabato,
kuita makusanyiko, siziwezi, hatta na ma-
14 kutano makuu uovu. Miezi yenu na siku
kuu moyo wangu umezichukia, zimenitaabi-
15 sha, nimechoka kuzivumilia. Mkitanua



Digitized by Google

Original from
HARVARD UNIVERSITY

mikono yenu nitaficha macho yangu kwenu,
hatta mkizidi kuomba sisikii, mikono yenu
imejaa damu.
16 Osheni, safikeni, wekeeni mbali uovu wa
matendo yenu katika machoni pangu. A-
17 cheni kutenda maovu, jifunzeni kutenda
mema, takeni hukumu, msayidieni mwenyi
kuonewa, mhukumieni yatima, mteteeni m-
18 jaani. Njooni tufanyane maneno, amesema
19 Yahuwa. Thambi zenu zikiwa kama ba-
ndera zitakuwa nyeupe kama thuluji, zikiwa
nyekundu nyekundu 'mno, zitakuwa kama
20 suffuf. Mkikubali, mkisikia, mtakula wema
wa inchi, lakini mkikataa, mkiasi, mtaliwa
na upanga, kwani kanwa la Yahuwa lime-
nena.
21 Umekuwaje kama kahaba mji amini?
Ulijaa hukumu, haki ikakaa humo, illa
22 sasa wauaji. Fetha zenu imekuwa povu,
23 mvinyo wenu umechanganywa na maji, wa-
kuu wenu waasi, na wenzao wevi. Killa
mtu hupenda zawadi, hufuata majazo, ha-
wamhukumii yatima, wala huja ya mjaani
24 haiwawasilii. Kwa ajili hii amenena Bwana



Digitized by Google
Original from
HARVARD UNIVERSITY

Yahuwa wa majeshi, mwenyi enzi wa Is-
raeli, Ah! nitajifariji katika watesi wangu,
25 nitajilipa kwa adui zangu, nitaurejeza mko-
no wangu juu yako, nitatakasa hatta usafi
povu lako, nitaondolea mbali risasi yako.
26 Nitawarejeza waamuzi wako kama kwanza,
na madiwani wako kama mwanzo. Hati-
ma utaitwa mji wa haki, mji wa imani.
27 Sayuni itakombolewa kwa hukumu, na wa-
ongofu wake kwa haki.
28 Kuharibika kwao wenyi kuhalifu na wenyi
thambi pamoja, wamwachao Yahuwa wata-
29 teketezwa. Kwani watatahayarika na mi-
ti waliyoitamani, nanyi mtaaibika kwa bu-
30 stani mlizozichagua. Kwani mtakuwa ka-
ma mti majani yake yakipukutika, na kama
31 bustani isiyo na maji. Naye hodari ataku-
wa kama bushi, naye afanyaye kama cheche
la moto, nao watawaka pamoja wala haku-
na kuzimia.

II. Neno aliloliona Isaya wa Amoz, juu ya
Yuda na Yerusalemi.

2 Itakuwa siku ya mwisho utawekwa mli-
ma wa nyumba ya Yahuwa juu ya milima,



Digitized by Google
Original from
HARVARD UNIVERSITY

utainuka juu ya vilima, mataifa yote wata-
3 upitia. Watu wengi watakwenda, watase-
ma, Haya, tupande mlimani mwa Yahuwa
kwa nyumba ya Muungu wa Yakobo, naye
atatufundisha ya njia zake. Tutapita kati-
ka mapito yake, kwani katika Sayuni ita-
toka sheria, na neno la Yahuwa katika Ye-
rusalemi.

4 Atahukumu kati ya mataifa, atawarudi
watu wengi, nao watafua panga zao kuwa
majembe, na mikuke yao kuwa miundo.
Wala taifa halitainua upanga juu ya taifa,
wala hawatajifunza tena kupigana.

5 Nyumba ya Yakobo njooni, tutembee ka-
tika nuru ya Yahuwa.

6 Kwani umeacha watu wako, nyumba ya
Yakobo, kwani wamejaa katika mashariki,
na wachawi kama Wafilisti, na katika waa-
7 na wageni wameshiba. Inchi yao imejaa
fetha na thahabu, wala hapana mwisho wa
hazina zao, inchi yao imejaa farasi, wala
8 hapana mwisho wa magari yao. Inchi yao
imejaa sanamu, kazi ya mikono yao, wajii-
nama kwa hizo zilizofanyika na vidole vyao.



Digitized by Google
Original from
HARVARD UNIVERSITY

9 Mtu ameinama, na mume amesujudu, wala
usiwaachilie.
10 Ingie katika mwamba, ujifiche katika
mavumbi, mbele ya hofu ya Yahuwa, na u-
11 kuu wa enzi yake. Macho yaliyoinuka ya
mtu yatathilika na urefu wa mume utainama,
12 atainuka Yahuwa peke yake siku ile. Kwa-
ni siku ya Yahuwa wa majeshi juu ya killa
cha kiburi na kirefu, na juu ya killa kinu-
13 kacho, kitashuka. Na juu ya killa mwerezi
wa Lebanoni mrefu, na uinukao, na juu ya
14 mialoni yote ya Bashani. Na juu ya mili-
ma mirefu yote, na juu ya vilima vyote vi-
15 livyoinuka. Na juu ya killa mnara mrefu,
16 na juu ya killa ukuta usiopandika, na juu
ya killa merikebu ya Tarshishi, na juu ya
17 killa taswira iliyotamanika. Na ulioinuka
wa mtu utainamika, na urefu wa mume uta-
thilika, atainuka Yahuwa peke yake si-
18 ku ile. Na sanamu atazipoteza kabisa.
19 Wataingia katika mapaango ya mwambani
na katika mashimo ya inchi, mbele ya hofu
ya Yahuwa na ukuu wa enzi yake, akiondo-
ka aivunjevunje inchi.



Digitized by Google

Original from
HARVARD UNIVERSITY

20 Siku ile mtu atatupa sanamu zake za fe-
tha, na sanamu zake za thahabu, alizozifa-
nya, azisujudie, kwazo zifukuazo na kwa
21 popo. Afike katika mapasuko ya miamba
na mapaango ya majiwe, mbele ya Yahuwa,
na ukuu wa enzi yake, akiondoka aivunje-
22 vunje inchi. Mwacheni mwana adamu
mwenyi pumuzi puani, kwani cheo gani hu-
yu alicho nacho?
III. Kwani yuko Bwana Yahuwa wa maje-
shi, akiondoa katika Yerusalemi na katika
Yuda tegemeo na tegemezo, killa tegemeo
2 la chakula na killa tegemeo la maji, aliye
hodari na mume wa vita, mhukumu na na-
3 bii, na mshauri, na mzee, jemadari wa ha-
msini na mwenyi uso wa heshima, na diwa-
ni, na mwenyi hekima, mstadi na mnenaji.
4 Nitafanya watoto wakuu, na wadogo wata-
5 watawala. Wataonewa watu, mtu na mtu,
na mtu na mwenzake, kijana akiwa na kiburi
juu ya mzee, na mnyonge juu ya mkuu.
6 Kwani mtu atamshika ndugu yake ya nyu-
mba ya baba yake, Unazo nguo, ututawale,
7 na anguko hili mkononi mwako. Ataapa



Digitized by Google

Original from
HARVARD UNIVERSITY

siku ile, kunena, Sitakuwa mponya, wala
nyumbani mwangu hapana chakula, wala
nguo, usinifanye mimi nitawale watu.
8 Kwani Yerusalemi umeanguka, na Yuda
umepotea, kwani ulimi wao na matendo yao
juu ya Yahuwa, watie uchungu macho ya
9 utukufu wake. Kutambua uso wao kuwa-
jibu, na thambi yao kama Sodoma, wame-
onyesha hawakuficha. Ole wa roho zao
kwani wamejilipia mabaya.
10 Mwambieni mwenyi haki kwani mwema
11 atakula mazao ya matendo yake. Ole wa
mtu thalimu, kwani malipo ya mikono ya-
12 ke atafanyiwa. Watu wangu wawaoneao
watoto, na waanaake wawatawalao. Enyi
watu wangu wakuongozao wakukosesha, na
13 njia za mapito yako wamezipoteza. Ame-
simama Yahuwa atete, amesimama awahu-
14 kumu watu. Yahuwa anakuja kwa huku-
mu na wazee wa watu wake na wakuu wao,
nanyi mmeila mizabibu, mateka ya masiki-
15 ni nyumbani mwenu. Ya nini mwaponda
watu wangu, mwasaga uso wa masikini,
amesema, Bwana Yahuwa wa majeshi?



Digitized by Google
Original from
HARVARD UNIVERSITY

16 Akanena Yahuwa kwani wanacho kiburi
binti Sayuni, wamekwenda kwa mashingo
yaliyonyoshwa na macho ya kudanganya,
wakienda, wakienda kwa uzuri, wakitoa
17 sauti kwa miguu yao, atawatia Bwana vi-
gaga kitwani binti Sayuni, Yahuwa atawa-
18 funulia aibu. Siku ile Bwana ataondoa
uzuri wa vijugu, na nyavu, shangwi, vi-
19 dani na vikuku, na mikufu, taji, na mitali,
20 na sarufu, na vibamba, na majassi, (21) na
22 pete, na azama, nguo zenyi rangi, na
23 utaji, na dusamali, na vifuko, miraa, na ki-
24 tani, na vitambi, na shela. Patakuwa kwa
nukato kuvunda, kwa mshipi kutatuka, kwa
nyele zilizosokotwa upaa, kwa kisibau ku-
funga sako, kuungua kwa uzuri.

25 Waume wako wataanguka kwa upanga
26 na nguvu zako katika kupigana. Italia,
itaomboleza milango yake, naye mtupu ata-
kaa chini.

IV. Waanaake saba watamshika mume mmo-
ja siku ile, kunena, Tutakula chakula chetu,
tatavaa nguo zetu, tuitwe tu kwa jina lako
2 juu yetu, uondoe aibu yetu. Siku ile lita-



Digitized by Google

Original from
HARVARD UNIVERSITY

kuwa tawi la Yahuwa kwa uzuri na utuku-
fu, na uzao wa inchi kwa ukuu na kupende-
3 za katika waliotoka ya Israeli. Itakuwa,
masalio katika Sayuni, na yaliyoachwa ka-
tika Yerusalemi, yataitwa matakatifu, killa
aliyeandikwa kwa kuwa hayi katika Yeru-
4 salemi. Akiosha Yahuwa machafu ya binti
Sayuni, na damu ya Yerusalemi akiisafisha
katika ndani yake, kwa roho ya hukumu,
5 na roho ya kuteketeza. Atafanya Yahuwa
juu ya killa mahali pa mlima Sayuni, na juu
ya makusanyiko yake, wingu na moshi
mchana, na kung'aa ndimi za moto usiku,
6 kwani juu ya utukufu wote kufunika. Na
masikani itakuwa mchana uvuli katika hari,
na kimbilio, na kustirika katika tufano na
mvua.

V. Nitamwimbia mpenzi wangu uimbo wa
mpenzi wangu wa mizabibu yake. Mpenzi
wangu alikuwa na mizabibu katika kilima
2 cha kunona. Akalima, akatoa mawe, aka-
panda mizabibu mema mno, akajenga mna-
ra kati yake, akachimba shinikizo, akataza-
mia itazaa zabibu, ikazaa zabibu za mwituni.



Digitized by Google
Original from
HARVARD UNIVERSITY

3 Bassi sasa mkaa Yerusalemi na mume wa
Yuda, Hukumuni sasa kati ya mimi na
4 mizabibu yangu. Kufanya nini tena kwa
mizabibu yangu nisivyofanya? Kwa nini
nimetazamia itazaa zabibu, ikazaa zabibu
5 za mwituni? Bassi nitawaonyesha nifa-
nyayo kwa mizabibu yangu, kuondoa ua,
iwe kwa kuliwa, kuvunja kitalu iwe kwa
6 kukanyagwa, nitaiweka kwa uharibifu, wa-
la haitafekwa, wala haitaliwa, itamea mbigi-
li na miiba, na juu mawingu nitayakataza
wasinye mvua huko.
7 Kwani mizabibu ya Yahuwa wa majeshi
nyumba ya Israeli, na mume wa Yuda mche
wake uliopendeza, akatazamia hukumu aka-
ona jeraha, haki akaona kilio.
8 Ole wao wanaojumlisha nyumba kwa
nyumba na shamba kwa shamba, hatta ka-
ribu kutoa kuwa nafasi, mkajiweka peke
9 yenu kati ya inchi. Masikioni mwangu
Yahuwa wa majeshi, kama si majumba me-
ngi yatakayoharibika, makubwa, na mema
10 pasipo kukaa. Kwani zimede kumi za mi-
zabibu zitafanya bati moja, na kupanda ho-



Digitized by Google
Original from
HARVARD UNIVERSITY

meri kutafanya efah.
11 Ole wao waamkao assubui wafuate ulevi,
wakishinda hatta jioni, hatta mvinyo ume-
12 watia moto. Itakuwa na kinubi, na kina-
nda, ngoma, na filimbi, na mvinyo katika
karamu zao, wala kazi ya Yahuwa hawaku-
iangalia, wala matendo ya mikono yake
hawakuyaona.
13 Kwa hiyo watu wangu wamehamishwa
kwa kutoa kuwa na maarifa, na fahari yao
14 yenyi njaa, na wingi wao wenyi kiu. Kwa
hiyo ahera imejipanua nafsi yake, imefu-
mbua kinwa chake pasipo cheo, utashuka
uzuri wao, na wingi wao, na uvumi wao, na
15 achekaye humo. Mtu atainama, atanenye-
kea mume, na macho yao walioinuka yata-
16 nenyekezwa. Atatukuzwa Yahuwa wa ma-
jeshi katika hukumu, na Muungu Mtakati-
17 fu ametakaswa kwa haki. Watalishwa wa-
ana kondoo kwa desturi yao, na maharibifu
yao wanono wageni watayala.
18 Ole wao wanaokokota mabaya kwa ka-
mba za uwongo, na kama kwa kamba la
19 gari, thambi. Wakinena, Afanye haraka,



Digitized by Google
Original from
HARVARD UNIVERSITY

ahimize kazi yake, tuone, ikaribie, ije hu-
kumu yake Mtakatifu wa Israeli tukajue.
20 Ole wao waitao baya jema, na jema baya,
wawekao giza kwa nuru, na nuru kwa giza,
wawekao uchungu kwa tamu, na tamu kwa
uchungu.
21 Ole wao wenyi hekima machoni pa wenye-
we, na usoni pa wenyewe wenyi busara.
22 Ole wao hodari kunywa mvinyo na wau-
23 me wa nguvu kuchanganya kileo. Waki-
mtia haki thalimu kwa kupewa ijara, na
haki ya mwenyi haki wamwondolea.
24 Kwa hiyo kama ulimi wa moto huteketе-
za majani, na moto huramba makapi, shina
lao kama kuoza litakuwa, na ua lao litapaa
kama mavumbi, kwani wametweza sheria
yake Yahuwa wa majeshi, na neno lake
Mtakatifu wa Israeli wamelitharau.
25 Kwa hiyo ameona hasira Yahuwa kwa
watu wake, akanyosha mkono wake juu
yao, akawapiga, vilima vikatetemeka, na
mizoga yao kama mavi ndani ya njia. Ka-
tika haya yote haikugeuka hasira yake,
hatta sasa mkono wake umenyoka.



Digitized by Google
Original from
HARVARD UNIVERSITY

26 Akatweka bandera kwa mataifa katika
mbali, atawazomelea katika miisho ya inchi,
27 nao wako, watakuja upesi hima. Hapana
aliyechoka, wala hapana asonganaye, wala
hatalala, wala hatasinzia, wala hautalegea
mshipi wa viunoni vyao, wala hautavunjika
28 ukanda wa viatu vyao. Mishale yao yote
mikali, na pindi zao zote zimekunjwa, ma-
kwato ya frasi zao zitahesabika kama mawe,
29 na magurudumu yao kama tufanu. Nguru-
mo yao kama ya simba, watanguruma kama
waana simba, watavuma watashika mawi-
ndo watachukua, wala hapana aokoaye.
30 Watavuma juu yao siku ile kama uvumi wa
bahari, atatazama inchi, liko giza, shidda,
na nuru imetiwa giza katika uwingu wake.
VI. Mwaka wa kufa Mfalme Uziya, nali-
mwona Yahuwa amekaa juu ya kiti kirefu,
kilichoinuka, hekalu ikajaa matandiko yake.
2 Maserafi wakakaa juu yake, mabawa sita,
mabawa sita mmoja, kwa mawili akasetiri
uso wake, kwa mawili akasetiri miguu yake,
3 kwa mawili akaruka. Akalia huyu kwa
huyu, akanena, Takatifu, Takatifu, Takati-



Digitized by Google Original from HARVARD UNIVERSITY

fu, Yahuwa wa majeshi, kujaa inchi yote
4 fahari yake. Ikatikisika miimo ya mla-
ngoni kwa sauti yake aliaye, nyumba ika-
jaa moshi.
5 Nikanena, Ole wangu, kwani nimenya-
maza, kwani mtu wa midomo michafu mimi,
na katika watu wa midomo michafu mimi
nimekaa, kwani macho yangu nimemwona
6 mfalme Yahuwa wa majeshi. Akanirukia
Serafi mmoja na mkononi mwake kaa la
moto, alilolitwaa kwa makoleo katika juu
7 ya mathbahu. Akanigusa juu ya kinywa
changu, akanena, Hili limegusa juu ya mi-
domo yako, umeondolewa uovu wako, na
8 thambi yako imestirika. Nikasikia sau-
ti ya Bwana, akinena, Nipeleke nani, nani
atakayekwenda kwa sisi? Nikanena, Mimi
hapa, nipeleke mimi.
9 Akanena, Nenda ukawaambie watu hawa,
Kusikia msikie wala msifahamu, kuona
10 mwone wala msitambue. Nonesha moyo wa
watu hawa, uzibe masikio yao, macho yao
ufumbe, wasione kwa macho, wala kwa
masikio wasisikie, wala moyoni wasifikiri,



Digitized by Google Original from HARVARD UNIVERSITY

11 wasigeuke nisiwaponye. Nikanena, Hatta
lini Bwana? Akanena, Hatta miji itaka-
poharibika pasipo kukaa, na nyumba pasipo
12 mtu, na inchi itaharibika uharibu. Na Ya-
huwa ataweka mbali watu, na kuacha kwi-
ngi katika inchi.
13 Hatta hivi katika hiyo ya kumi, itarudi
italiwa, itakuwa kama mwela, na kama
mweloni, mwenyi asili ukipukutika, na mbe-
gu takatifu asili yake.
VII. Ikawa siku za Ahaz wa Yotham, wa Uzi-
ya, mfalme wa Yuda, akapanda Rezin mfal-
me wa Aram, na Peka wa Remaliya mfalme
wa Israeli, kwa Yerusalemi wapigane nao,
wala hawakupata kuuweza.
2 Ikahubiriwa kwa nyumba ya Daud ku-
nena, Aram amestarehe juu ya Efraim, mo-
yo wake ukatikisika, na moyo wa watu wa-
ke, kama miti ya mwituni mbele ya upepo.
3 Yahuwa akamwambia Isaya, Utoke sasa
umkute Ahaz, wewe na Shearjashub mwa-
nawe, kwa mwisho wa mfeleji wa maji wa
birika la juu, katika njia ya uwanja wa
4 msafisha nguo. Ukamwambie, Angalie,



Digitized by Google
Original from HARVARD UNIVERSITY

ukastarehe, usiogope, wala moyo wako usi-
legee kwa mikia hii miwili ya vinga vya
moshi, kwa hasira ya Rezin, na Aram, na
5 Wadi Remaliya. Kwa hiyo ya kwamba wa-
mefanya shauri juu yako, Aram kwa viba-
ya, na Efraim, na Wadi Remaliya, kunena,
6 Tupande katika Yuda, tuuangamize tuuga-
wanye kwa sisi, tufanye tumiliki mfalme
7 kati yake Wadi Tabeal. Ndivyo asemavyo
Bwana Yahuwa, haitasimama, wala haita-
8 kuwa, kwani kitwa cha Aram Dameski, na
kitwa cha Dameski Rezin, na tangu leo
miaka sitini na mitano Efraim atavunjika
9 katika kuwa watu. Na kitwa cha Efraim
Samaria, na kitwa cha Samaria Wadi Re-
maliya, msiposadiki kwani sinyi waaminifu.
10 Akizidi Yahuwa kumwambia Ahaz, ku-
11 nena. Ujitakie ishara katika kwa Yahu-
wa Muungu wako, nenda chini kutaka, ao
12 jiinue juu. Akanena Ahaz, Sitataka, wala
sitamjaribu Yahuwa.
13 Akanena, Sikieni sasa, nyumba ya Daud,
ndogo kwenu kuwachosha watu, mtamcho-
14 sha na Muungu wangu? Kwa hiyo, atatoa



Digitized by Google
Original from
HARVARD UNIVERSITY

Yahuwa mwenyewe ishara kwenu, ndiyo
mwanamwali akiwa na mimba akizaa mwa-
15 na, utamwita jina lake Emmanuel. Siagi
na asali atakula, ajue kukataa mabaya na
16 kuchagua mema. Kwani mbele kijana ha-
japata kukataa mabaya na kuchagua mema,
itaachwa inchi uliyochukiwa nayo, mbele
17 ya wafalme wawili wake. Yahuwa ataleta
juu yako, na juu ya watu wako, na juu ya
nyumba ya baba wako, siku zisizokuja ta-
ngu siku ya kurudi Efraim katika Yuda,
mfalme wa Ashur.
18 Itakuwa siku ile Yahuwa atalizomelea
inzi, lililo mwishoni mwa mto wa Misri, na
19 nyuki, iliyo katika inchi ya Ashur. Wa-
takuja watastarehe wote katika mito iliyo
mikavu, na katika mapaango ya miamba,
na katika miiba yote, na katika miti yote.
20 Siku ile Yahuwa atanyoa kwa wembe ulio
kwa ijara, kwa wale ng'ambo ya mto, kwa
mfalme wa Ashur, kitwa na nyele miguuni,
hatta ndevu italika.
21 Itakuwa siku ile mtu atachunga ndama
22 ya ng'ombe, na kondoo wawili. Itakuwa



Digitized by Google Original from HARVARD UNIVERSITY

kwa wingi wa maziwa atakula siagi, kwani
siagi na asali atakula killa aliyesalia ndani
23 ya inchi. Itakuwa siku ile killa pahali pa-
lipo mizabibu elfu kwa fetha elfu, pa mbigili
24 na miiba. Kwa mishale na upindi watai-
ngia humo, kwani kwa mbigili na miiba
25 itakuwa inchi yote. Na milima yote iliyo-
limwa kwa gembe, haitakuja huko hofu ya
mbigili na miiba, itakuwa kupeleka ng'o-
mbe, na kukanyaga makundi.

VIII. Akaniambia Yahuwa, Ujitwalie kita-
bu kikubwa, ukaandike humo kwa kalamu
2 ya mtu kwa Maher-shalal-hashbaz. Nika-
jishuhudisha mashahidi amini, Uriya mko-
hani, na Zekariya wa Yeberekiya.

3 Nikaingia kwa mke nabii akapata mi-
mba, akazaa mwana. Akaniambia Yahu-
wa, Mwite jina lake Maher-shalal-hashbaz.
4 Kwani mtoto mbele hajajua kunena, Baba
wangu na mama wangu, itatolewa hasina
za Dameski na mateka ya Samaria mbele
ya mfalme wa Ashur.

5 Akazidi tena Yahuwa kuniambia, aki-
6 nena, Kwa hiyo kwani watu hawa wame-



Digitized by Google

Original from
HARVARD UNIVERSITY

katαa maji ya Shiloa yapitayo taratibu, na
7 furaha yao Rezin, na Wadi Remaliya, naye
Bwana yupo afurikisha juu yao maji ya
mito ya nguvu na mingi, mfalme wa Ashur
na utukufu wake wote, atafurikisha juu yao
kondo lote la maji yake, atapita juu ya ka-
8 ndo lake lote. Yatapita katika Yuda, ya-
tafurika, yataenea, yatafika hatta shingoni,
kunyosha mabawa yake juu ya inchi yako
yote Emmanuel.
9 Mvunjike watu, na mtapondwa, sikieni
wote walio mbali katika inchi, mjifunge,
na mtapondwa, mjifunge na mtapondwa,
10 mshawiri shauri itatawanyika, semeni neno
wala halitasimama, kwani *ni* Emmanuel.
11 Kwani ndivyo alivyoniambia Yahuwa,
kwa mkono hodari, akanifundisha nisiende
12 katika njia ya watu hawa, akinena, Msiseme
kupatana kwa yote ayasemeayo watu hawa
kupatana, wala woga wao usiogope, wala
13 usione hofu. Yahuwa wa majeshi mwe-
nyewe mmtakaye, naye mwenyewe mmwo-
14 gopaye, naye hofu yenu. Atakuwa kwa
patakatifu, na jiwe la kujikwaa, na mwa-



Digitized by Google
Original from
HARVARD UNIVERSITY

mba wa kujiangusha kwa nyumba mbili za
Israeli, kwa tanzi na kwa wavu kwa mkaa
15 Yerusalemi. Wengi watajiangusha kwa
hizo, wataanguka, watapondwa, watanaswa
16 watakamatwa. Funge ushahidi, tia muhu-
ri kwa sheria pamoja na waanafunzi waugu.
17 Mimi nitamngojea Yahuwa afichaye uso
wake, kwa nyumba ya Yakobo, nitamtaza-
18 mia. Nipo mimi na waana niliopewa na
Yahuwa, kwa ishara na kwa ajabu katika
Israeli, katika kwa Yahuwa wa majeshi.
19 Watakapowaambia, Tafuteni kwa wa-
chawi, na waganga wachunguliao na wano-
ng'oniao, watu wasimtafute muungu wao?
Kwa wale walio hayi kwa wale walio kufa.
20 Kwa torati na kwa ushahidi, wasiposema
kwa neno hili, kwa sababu hawana weupe.
21 Atapita katika hiyo mwenyi ugumu, na
mwenyi njaa, itakuwa akiona njaa atagha-
thabika, atalaani mfalme wake na Muungu
22 wake, atatazama juu. Juu ya inchi atataza-
ma, na yako mateso, na giza, na uvuli wa
shidda, na weusi kumetanda.
IX. Kwani hautiwi uvuli kwake aliye na



Digitized by Google Original from HARVARD UNIVERSITY

shidda, kama kwa wakati wa kwanza alipo-
tendea mapesi inchi ya Zebulon na inchi ya
Nafthali, baadaye akatendea mazito njia ya
bahari, ng'ambo ya Yardeni, Galilaya ya
2 mataifa. Watu waliokwenda gizani wame-
ona nuru kuu, waliokaa katika inchi na ki-
vuli cha mauti nuru imewaangaza.
3 Umelizidisha taifa, hukuzidisha furaha,
wamefurahiwa mbele yako kama furaha
ya mavuno, kama washangilia wakigawa-
4 nya mateka. Kwani uti wa mzigo wake,
na gongo la bega lake, na fimbo yake ao-
neayo umeivunja, kama siku ya Midiani.
5 Kwani killa pigano lao wapiganao kwa u-
thia, na nguo zilizofingirika katika damu,
itakuwa kwa kuteketeza chakula chake
moto.
6 Kwani mtoto tumezaliwa sisi, mwana
tumepewa, kutakuwa kutawala begani
mwake, ataitwa jina lake, Wa ajabu, Mwe-
nyi shauri, Muungu hodari, Baba wa milele,
7 Mkuu wa amani. Kuzidi kutawala na
amani, mwisho hakuna. Juu ya kiti cha
Daud, na juu ya milki yake, kuiandika, na



Digitized by Google Original from HARVARD UNIVERSITY

kuitegemeza kwa hukumu, na kwa haki,
tangu wakati ule hatta milele. Uwivu wake
Yahuwa wa majeshi utatenda haya.
8 Akapeleka Yahuwa neno kwa Yakobo
9 likaanguka katika Israeli. Watu wajue
Efraimi wote na mkaa Samaria katika kibu-
10 ri na katika ukuu wa moyo, akinena, Mato-
fali yameanguka, tutajenga kwa mawe ya
manga, mikuyu imekatika tutaibadili kuwa
11 mierezi. Yahuwa ataleta adui, Rezin juu
12 yake, na maadui atawachanganya. Aram
kwa mashariki na Wafilisti nyuma wataku-
la Israeli, kwa kinwa chote. Kwa haya
yote haikugeuka hasira yake, hatta sasa
mkono wake umenyoka.
13 Wala watu hawakumgeukia awapigaye,
wala hawakumtaka Yahuwa wa majeshi.
14 Naye Yahuwa atakata Israeli kitwa na
15 mkia, tawi na kijani siku moja. Mzee
mwenyi heshima ndiye kitwa, na nabii ato-
16 aye uwongo ndiye mkia. Kwani wanao-
wabariki watu hawa, ndio wawakoseshao,
na waliobarikiwa nao wamepotea.
17 Kwa hiyo Yahuwa hatafurahiwa na vi-



Digitized by Google Original from HARVARD UNIVERSITY

jana vyao, wala yatima zao, wala wajaani
wao hatawarehemu. Kwani killa mtu mna-
fiki na mbaya, killa kinwa chanena upumba-
fu. Katika haya yote haikugeuka hasira
yake, hatta sasa mkono wake umenyoka.
18 Kwani ubaya umewaka kama moto, uta-
kula mbigili na miiba, utawaka katika vi-
chaka vya mwituni, utapanda kama kuinu-
19 ka moshi. Kwa hasira ya Yahuwa wa ma-
jeshi inchi imetiwa giza, na watu watakuwa
kama chakula cha moto, mtu hatamwacha
20 nduguye. Atanyakua kwa kuume, ataona
njaa, atakula kwa kushoto, wala hashibi,
killa mtu atakula nyama ya mkono wake.
21 Manasse Efraim na Efraim Manasse, nao
pamoja juu ya Yuda. Katika haya yote
haikugeuka hasira yake, hatta sasa mkono
wake umenyoka.
X. Ole wao waamuruo amri za thulumu,
2 waandikao mzigo wameuandika. Kumge-
uza katika kuamuliwa asiye na nguvu, wa-
nyang'anyao hukumu yao walioteswa wa
watu wangu, wajaani wawe mateka yao
3 wakawaibia yatima. Mtafanyaje siku ya



Digitized by Google Original from HARVARD UNIVERSITY

kujiliwa na katika uharibifu ujao mbali?
Mtamkimbilia nani kwa msaada, mtaacha
4 wapi utukufu wenu? Pasipo mimi watai-
nama chini ya wafungwa wataanguka chini
yao waliouawa. Katika haya yote haiku-
geuka hasira yake, hatta sasa mkono wake
umenyoka.
5 Ole wa Ashur fimbo ya hasira yangu, na
gongo la mkononi mwao ghathabu yangu.
6 Kwa watu wa unafiki nitampeleka, na juu
ya watu wanitiao hasira nyingi nitamtuma,
ateke mateka, awinde mawindo awaweke
wakanyagwe kama tope la njiani.
7 Wala sivyo athanivyo mwenyewe, wala
moyo wake hauyawazi haya, illa kwa kupo-
teza moyo wake na kukatia mbali mataifa
8 si machache. Kwani asema, Si wakuu wa-
9 ngu kama wafalme? Si kama Karkemish
Kalno? Si kama Arpad, Hamath? Si ka-
10 ma Dameski Samaria? Kama mkono wa-
ngu ulivyoona ufalme wa ubatili, na sa-
namu zao kuliko Yerusalemi na Samaria.
11 Si kama nilivyofanyia Samaria na ubatili
wake, nifanyie hivi Yerusalemi na sanamu



Digitized by Google
Original from
HARVARD UNIVERSITY

12 zake? Itakuwa atakapotimiza Yahuwa kazi
yake yote katika mlima Sayuni na katika
Yerusalemi, nitakuja kwa mazao ya ukuu
wa moyo wake mfalme wa Ashur, na kwa
utukufu wa kuinuka macho yake.
13 Kwani amenena, Kwa nguvu za mkono
wangu nimetenda, na kwa hekima yangu,
kwani nina busara, nimeondosha mipaka ya
14 watu, na akiba zao nimeteka, nikashusha
kama aliye hodari wakaao. Mkono wangu
umeona kama kiota, mali ya watu, na kama
kukusanya mayayi yaliyoachwa, nimekusa-
nya inchi yote, wala hapana aliyetikisa ba-
wa, wala aliyefumbua kinwa, wala aliyelia.
15 Lijisifu shoka juu yake achanjaye, uji-
sifu msumeno juu yake autikisaye, fimbo
ijitikise juu yake aiinuaye, kama kuinuka
16 bakora wala si mti? Kwa hiyo Mola Bwana
wa majeshi ataleta kukonda katika wanono
wake, na chini ya fahari yake ataunguza
17 kuungua kama kuungua moto. Atakuwa
Nuru ya Israeli moto, na Mtakatifu wake
kwa ulimi wa moto, utaungua, utakula
mbigili zake na miiba yake katika siku mo-



Digitized by Google
Original from
HARVARD UNIVERSITY

18 ja. Na fahari ya mwitu wake, na Kar-
meli yake, katika nafusi hatta nyama itali-
wa, itakuwa kama akizimia mwenyi bande-
19 ra. Na iliyosalia ya mwitu wake itakuwa
hesabu, hatta mtoto aiandike.
20 Itakuwa siku ile waliosalia wa Israeli na
waliotoka katika nyumba ya Yakobo hawata-
tegemea tena juu yake aliyewapiga, wata-
tegemea juu ya Yahuwa, Mtakatifu wa
21 Irsaeli kwa kweli. Masalio watarudi, ma-
salio wa Yakobo, kwa Muungu aliye hodari.
22 Kwani wakiwa watu wako Israeli kama
mchanga wa pwani, masalio yatarudi katika
hao, ukomo ulioamriwa utafura kwa haki,
23 Kwani ukomo, na kwa amuru, Bwana Ya-
huwa wa majeshi afanya katika inchi yote.
24 Kwa hiyo amesema Bwana Yahuwa wa
majeshi, Usiogope, watu wangu ukaaye Sa-
yuni, kwa Ashur, kwa fimbo atakupiga, a-
tainua bakora yake juu yako kwa njia ya
25 Misri. Kwani kidogo kidogo tena, hasira
itakoma, na ghathabu yangu, wakipotea.
26 Atainua juu yake Yahuwa wa majeshi jele-
di kwa pigo la Midiani, kwa jiwe la Oreb,



Digitized by Google
Original from
HARVARD UNIVERSITY

na fimbo yake juu ya bahari ataiinua kwa
27 njia ya Misri. Itakuwa siku ile utaondole-
wa mzigo wake katika begani, na mti wa-
ke katika shingoni, na mti utaharibika ka-
tika mbele ya mafuta.
28 Amekuja Ayath, amepita kwa Migron,
katika Mikmash ameweka mizigo yake.
29 Wamevuka kivuko kwa Geba wamekaa ka-
tika kituo. Rama wametetemeka, Gibea
30 ya Saul wamekimbia. Upalize sauti yako
binti Gallim, usikize hatta Laish, maskini
31 Anathoth. Wamehama Madmena, wakaa
32 Gebeim wamejikusanya wakimbie. Hatta
leo kusimama kwa Nob, atatikisa mkono
wake kwa mlima wa nyumba ya Sayuni,
kilima cha Yerusalemi.
33 Yuko Mola Yahuwa wa majeshi atakata
tawi kwa hofu, na warefu watashushwa,
34 atakata msitu wa mwitu kwa chuma, na Le-
banon kwa aliye hodari itaanguka.
XI Itatoka kitawi katika shina la Yese, na
2 tawi litamea katika mashina yake. Roho
ya Yahuwa itakaa juu yake, Roho ya heki-
ma na akili, Roho ya shauri na nguvu,



Digitized by Google
Original from
HARVARD UNIVERSITY

3 Roho ya maarifa na hofu ya Yahuwa. Ita-
mfanya asikie katika hofu ya Yahuwa, kwa
kuona macho hatahukumu, wala kwa kusi-
4 kia masikio hatarudi. Atahukumu kwa ha-
ki masikini, atarudi kwa adili kwa wenyi
upole wa inchi. Atapiga inchi kwa fimbo
ya kinwa chake, na kwa pumuzi ya mido-
5 mo yake atamua mbaya. Haki itakuwa
mshipi wa viunoni mwake, na imani mshipi
6 kiunoni mwake. Mbwa wa mwitu ataketi
pamoja na mwana kondoo, na chui pamoja
na mwana mbuzi atalala, na ndama na
mwana simba na kinono pamoja, na mtoto
7 mchanga atawaongoza. Ng'ombe na dube
watakula, pamoja watalala watoto wao,
na simba kama ng'ombe atakula majani.
8 Atacheza anyonyaye juu ya tundu la nyo-
ka, na juu ya paango la pili aliyeacha ku-
9 nyonya ataweka mkono. Hawatathuru,
wala hawataharibu katika mlima wote wa
utakatifu wangu, kwani imejaa inchi kum-
jua Yahuwa, kama maji yafunikavyo bahari.
10 Itakuwa siku ile shina la Yese, lisimama-
lo ishara kwa watu, kwa hilo watu wa matai-



Digitized by Google
Original from HARVARD UNIVERSITY

fa watatafuta, itakuwa na raha yake tukufu.
11 Itakuwa siku ile atatia tena Yahuwa mko-
no wake awamiliki waliosalia wa watu wake,
waliokaa katika Ashur, na katika Misri, na
katika Pathros, na katika Kush, na katika
Elam, na katika Sinaar, na katika Hamath,
12 na katika visiwa vya bahari. Atatweka
bandera kwa mataifa, atakusanya waliofu-
kuzwa wa Israeli, na waliotawanyika wa
Yuda atawaleta katika pembe nne za inchi.
13 Utakoma uwivu wa Efraim na adui za
Yuda watakatika. Efraim hawatahasidi
14 Yuda, wala Yuda hawatathii Efraim. Wa-
taruka mabegani mwa Wafilisti kwa maga-
ribi, watatekwa waana wa mashariki pa-
moja, Edom na Moabi pakutia mikono yao,
15 na Waana Amon kuwasikia. Yahuwa ata-
futia mbali ulimi wa bahari ya Misri, atati-
kisa mkono juu ya mto kwa nguvu za roho
yake, ataupiga katika mito saba atawapiti-
16 sha wenyi viatu. Itakuwa njia kwa masalio
ya watu wake watakaosalia katika Ashur,
kama ilivyokuwa kwa Israeli siku ya kuto-
ka katika inchi ya Misri.



Digitized by Google

Original from
HARVARD UNIVERSITY

XII. Utasema siku ile, Nitakusifu Yahuwa,
ulikuwa na hasira juu yangu, hasira yako
2 imegeuka, umenifariji. Ndiye Muungu
wokovu wangu, nitatumaini, sitaogopa,
kwani nguvu zangu na uimbo Yah Yahuwa,
amekuwa kwangu kwa wokovu.
3 Mtateka maji kwa furaha katika visima
4 vya wokovu. Utasema siku ile, Msifuni Ya-
huwa, mwiteni jina lake, elezeni matendo
yake kwa watu, kumbukeni ya kwamba
5 jina lake limetukuka. Mwimbieni Yahuwa,
kwani matendo yake makuu, yaliyojulikana
6 katika inchi yote. Palize sauti, hubiri, Ee
mkaa Sayuni, kwani mkuu ndani kwako
Mtakatifu wa Israeli.

XIII. Mzigo wa Babeli aliouona Isaya wa A-
moz.
2 Twekeni bandera juu ya mlima mrefu,
palizeni sauti kwao, pungieni mkono, wa-
3 pate kuingia mlangoni mwa wakuu. Ni-
meamuru waliotakaswa wangu, nimewaita
walio hodari kwa hasira yangu, wafurahio
kwa utukufu wangu.
4 Sauti ya wengi katika milima kwa mfano



Digitized by Google Original from HARVARD UNIVERSITY

wa watu wengi, sauti ya uvumi wa wafalme,
wa mataifa waliokusanyika, Yahuwa wa
5 majeshi ukija kwa majeshi ya vita. Wa-
kija katika inchi iliyo mbali, katika mwi-
sho wa uwingu, Yahuwa vyombo vya hasi-
ra yake kuharibu inchi yote.
6 Pigeni makelele, kwani karibu siku ya
Yahuwa kama kuwinda katika kwa Mwe-
7 nyiezi. Kwa hiyo mikono yote italegea,
8 na killa moyo wa watu utayeyuka. Wata-
ogopa, kuuma na utungu utawashika, kama
azaaye watauma, watashangaa wao kwa wao,
nyuso za moto nyuso zao.
9 Iko siku ya Yahuwa inakuja, kali kwa
kuungua, na kwa hasira kuweka inchi ja-
10 ngwa tu, na wakosao wake watapotea.
Kwani nyota za mbinguni, na jabari zao,
haziangaza nuru yao. Litatiwa giza jua
akitoka, wala mwezi hautatoa nuru yake.
11 Nitaleta juu ya ulimwengu mabaya, na juu
ya waovu uthalimu wao. Nitakomesha ki-
buri chao wenyi makuu, na majivuno yao
wafanyi hofu nitayathili.
12 Nitamfanya mtu kuwa na thamani kuliko



Digitized by Google

Original from
HARVARD UNIVERSITY

thahabu, na mwana Adamu kuliko thahabu
13 ya Ofiri. Kwa hiyo nitatikisa mbingu, na
inchi itatoka katika mahali pake, ghathabu
ya Yahuwa wa majeshi, na siku ya hasira
14 yake. Itakuwa kama paa iliyofukuzwa, na
kama kondoo pasipo mchunga, killa mtu
akitazamia watu wake, na killa mtu ataki-
15 mbia kwa inchi yake. Killa atakayeoneka-
na, atachomwa, na killa aliyeungana ataa-
16 nguka kwa upanga. Watoto wao watavu-
njwa machoni pao, nyumba zao zitatekwa,
na wake wao watatiwa nguvu.
17 Mimi nitaleta juu yao Wamedi, wasiope-
18 nda fetha, wala hawatamani thahabu, pindi
zao zitaangusha vijana, wala hawatahuru-
mia mazao ya matumbo, macho yao hayata-
waachilia watoto.
19 Itakuwa Babeli uzuri wa ufalme, ukuu
wa kiburi cha Wakasidi, kama Muungu
20 alivyoangusha Sodoma na Gomora. Hawa-
takaa milele, wala hapana wakaao kizazi na
kizazi, wala Mwarabu hatatanda huko hema
21 wala wachunga hawatatua huko. Nya-
ma za nyikani zitalala huko, na nyumba zao



Digitized by Google
Original from
HARVARD UNIVERSITY

zitajaa waanguao, na waliao zitakaa huko, na
22 zenyi nyele zitacheza huko. Na mbwa za
mwitu zitaimba katika nyumba zao zilizoa-
chwa, na majoka katika majumba yao ya a-
nasa, na wakati wake karibu kuja, wala si-
ku zake hazitaongezeka.
XIV. Kwani Yahuwa atarehemu Yakobo, hat-
ta sasa atachagua Israeli, atawasterehesha
katika inchi yao, na mgeni ataungana nao,
2 ataambatana na nyumba ya Yakobo. Wa-
tu watawatwaa watawaleta mahali pao, ita-
warithi nyumba ya Israeli katika inchi ya
Yahuwa, kwa watumwa na kwa wajakazi,
watawafunga waliowafunga wao, watatawa-
la juu yao waliowaonea.
3 Itakuwa siku Yahuwa atakapokupa raha
katika kazi yako, na katika hofu, na kati-
ka utumwa mgumu uliotumikishwa.
4 Utainua mfano huu juu ya mfalme wa
Babeli, ukinena, Mwenyi jeuri amekomaje!
5 Umekoma mji wa thahabu. Yahuwa ame-
ponda gongo la wabaya, fimbo yao walio-
6 tawala. Aliyewapiga watu kwa hasira kwa
mapigo dayima, aliyewatiisha mataifa kwa



Digitized by Google
Original from
HARVARD UNIVERSITY

7 ghathabu, ameteswa hapana akataye. Ime-
tulia, imestarehe killa inchi, wameimba si-
8 fa. Hatta miberoshi imefurahi juu yako,
mierezi ya Lebanoni, Tangu ulipolazwa ha-
kupanda akataye juu yetu.
9 Ahera chini imetetemeka kwa ajili yako
kukuona ukija, imeamsha wafu kwa wewe,
wote mabebera ya inchi, imeondokesha ka-
tika vitini mwao wafalme wote wa mataifa.
10 Hawa wote watajibu watakuambia, Hatta
wewe umethoofika kama sisi, umefanana
11 nasi? Kimeshushwa hatta ahera kiburi
chako, sauti ya vinanda vyako, chini yako
zimetandwa funza na kukufunika funza.
12 Umeangukaje katika mbingu, Ee mtoa
nuru, mwana wa assubuhi, umekatika hatta
13 chini, uliowathoofisha mataifa. Nawe ume-
sema moyoni mwako, Nitapanda mbinguni,
juu ya nyota za Muungu nitainua kiti cha-
ngu nitakaa katika mlima wa kusanyiko pa-
14 nde za kaskazini. Nitapanda juu ya virefu
15 vya mawingu, nitafanana naye aliye juu.
Illakini utashushwa hatta ahera, hatta pa-
16 ndeni mwa shimo. Wakuonao watakua-



Digitized by Google
Original from
HARVARD UNIVERSITY

ngalia, watakukumbuka, Siye huyu mtu
17 aliyetetemesha inchi, aliyetikisa ufalme.
Aliyefanya ulimwengu kama unyika, aka-
haribu miji yake, hakufungua mahali pao
aliowafunga.
18 Wafalme wote wa mataifa killa mmoja,
wamelala faharini, killa mtu nyumbani mwa-
19 ke. Nawe umetupwa katika kaburi lako,
kama tawi lichukizalo, mavazi yao walioua-
wa, waliochomwa kwa upanga, washukao
katika mawe ya birika, kama mayiti iliyo-
20 kanyagwa. Hutaungwa nao katika kuzi-
kwa, kwani inchi yako umeiharibu, watu
wako umewaua. Wazao wa mabaa hawa-
tasifiwa milele.
21 Uweke tayari kuuawa kwa watoto wake
kwa ubaya wa baba zao, wasiondoke, wasii-
rithi inchi, wasijaze juu ya ulimwengu kwa
22 miji. Nitaondoka juu yao, asema Yahuwa
wa majeshi, nitakatia Babeli, jina na jamaa,
na mwana, na mjomba, asema Yahuwa.
23 Nitaiweka kuwa milki ya kifodi, na pahali
pa maji, nitafagia kwa ufagio wa uharibifu,
asema Yahuwa wa majeshi.



Digitized by Google
Original from
HARVARD UNIVERSITY

24 Ameapa Yahuwa wa majeshi akinena,
Hivyo nilivyothani, ndivyo itakuwa, nami
25 nilivyoshika itakaa. Kuvunjia mbali Ashur
katika inchi yangu, na katika milima ya-
ngu nitamkanyaga, ndipo mti wake utato-
ka kwao, na mzigo wake utaondolewa katika
26 begani mwao. Ndiyo shauri iliyoshawiriwa
juu ya inchi yote, ndio mkono ulionyoshwa
27 juu ya mataifa yote. Kwani Yahuwa wa
majeshi ameshawiri, nani atakayebatili?
Mkono wake umenyoka, nani atakayeurudi-
sha.
28 Mwaka alipokufa mfalme Ahaz palikuwa
29 mzigo huu. Usifurahi, Ee Ufilisti pia wee,
kwa sababu limevunjika gongo lililokupiga,
kwani katika shina la nyoka pili atatoka,
na uzao wake nyoka ya moto arukaye.
30 Nao wazaliwa wa kwanza wa masikini wa-
takula, na waombaji watajilaza kwa tumai-
ni, nitafisha kwa njaa shina lako, na masa-
lio yako atayaua.
31 Upige yowe, Ee mlango, ulie, Ee mji,
umeyeyuka Ufilisti pia, kwani katika kas-
kazini moshi uaja, wala hapana peke yake



Digitized by Google Original from HARVARD UNIVERSITY

32 wakati wake. Majibu gani watapewa wa-
jumbe wa taifa? Kwani Yahuwa ametia
misinji ya Sayuni, na ndani yake watatu-
maini wanyonge wa watu.
XV. Mzigo wa Moabi. Kwani usiku Ar
Moabi imeharibika, imekatika. Kwani usi-
2 ku imeharibika Kir Moabi imekatika. A-
mepanda Bayith na Dibon, mahali pa juu,
alie. Juu ya Nebo na juu ya Medeba Mo-
abi atapiga kelele, katika vitwa vyake vyote
3 upaa, killa ndevu imenyolewa. Njiani mwa-
ke watavaa sako, katika dari zake, na kati-
ka njia zake, watalia wote pia, wakishuka
4 kwa machozi. Akatoa sauti Heshbon na
Eleale, hatta Yahaz sauti yao imesikiwa.
Kwa hiyo asikari za Moabi watalia, nafusi
yake itamlilia.
5 Moyo wangu utamlilia Moabi, wakimbizi
wake hatta Zoar, ndama ya miaka mita-
tu, kwani katika kupanda Luhith kwa ma-
chozi watapandia, kwani njia ya Horonaim
6 sauti ya kuvunjika watainua. Kwani maji
ya Nimrim yatakuwa maharibika, miche
imekauka, majani yamekoma, hapana imea-



Digitized by Google

Original from
HARVARD UNIVERSITY

7 yo. Kwa hiyo wingi walioupata, na akiba
yao katika mto wa miarabi itachukuliwa.
8 Kwani kilio kimezunguka mipaka ya Moabi,
hatta Eglaim kelele yake, na maombolezo
9 hatta Beer Elim. Kwani maji ya Dimon
yamejaa damu, kwani nitaweka juu ya Di-
mon yazidiyo, simba juu yake akimbiaye
wa Moabi, na masalio ya inchi.
XVI. Lete mwana kondoo kwa mtawala inchi
katika mwamba wa unyika, hatta mlima wa
2 binti Sayuni. Itakuwa kama ndege aenda-
ye aliyeacha tundu watakuwa binti za Mo-
3 abi kwa vivuko vya Arnon. Lete shauri,
fanya hukumu, weka kama usiku kivuli
chako kati ya aththuuri, ufiche waliofuku-
4 zwa, aendaye usimtoe. Waliofukuzwa wa-
ngu wakae kwako, Moabi, uwe uvuli wao
usoni pa mharibu, kwani mwisho wake aso-
ngaye, amekoma atekaye, amepunguka
5 akanyagaye katika inchi. Kitafanyizwa
kwa rehema kiti, atakaa juu yake katika
kweli hemani mwa Daudi, akihukumu, a-
kitaka hukumu, akihimiza haki.
6 Tumesikia kiburi cha Moabi, mwenyi



Digitized by Google
Original from HARVARD UNIVERSITY

kiburi kingi, makuu yake, na marefu yake,
na hasira yake, uwongo wake sivyo.
7 Kwa hiyo Moabi atamlilia Moabi, atajililia
pia, katika misinji ya Kir-hareseth, mta-
8 huzunika, imepigwa. Kwani makoonde ya
Heshbon yazimia, mzabibu wa Sibma, ma-
seyidi ya mataifa wamesetaseta matawi ya-
ke yaliyo mazuri. Yamefika hatta Yaazer,
yamezunguka katika unyika, kutoka kwake
9 kumepita kumevuka bahari. Kwa hiyo ni-
talilia kwa machozi ya Yaazer mzabibu wa
Sibma, nitawatia maji kwa machozi yangu
Heshbon na Eleale, kwa shangwi ya matu-
nda yako, na mavuno yako yameanguka.
10 Furaha imetolewa na kucheka katika Kar-
mel, na katika mizabibu hapana kuimba,
wala kigelegele, mvinyo katika mashiniki-
zo haukanyagwi na wakanyagao, shangwi
11 nimeikomesha. Kwa hiyo italia ndani ya-
ngu kama kinubi kwa Moabi, na matumbo-
ni kwa Kir-haresh.

12 Itakuwa, itakapoonekana ya kwamba
Moabi ameshughulika katika mahali pa
juu, ataingia katika patakatifu pake aombe,



Digitized by Google

Original from
HARVARD UNIVERSITY

illa hataweza.
13 Ndilo neno alilolinena Yahuwa juu ya
14 Moabi hatta leo. Na leo amenena Yahuwa
akisema, kwa miaka mitatu kwa miaka ya-
ke aliye kwa mshahara, utatharauliwa utu-
kufu wa Moabi, katika makutano yale me-
ngi, na masalio machache, madogo, si me-
ngi.
XVII. Mzigo wa Dameski. Iko Dameski
imeondolewa katika kuwa mji, itakuwa
2 chungu la maanguko. Imeachwa miji ya
Aroer, kwa makundi itakuwa, watajilaza wa-
3 la hapana atiaye hofu. Itakwisha ngome
katika Efraim na ufalme katika Dameski na
masalio ya Aram, kama utukufu wa waana
wa Israeli watakuwa, amesema Yahuwa wa
majeshi.
4 Itakuwa siku ile utapunguka utukufu wa
Israeli, na unono wa mwili wake utakonda.
5 Itakuwa, kama mvuna akikusanya mavuno,
na mkono wake wakata masuke, itakuwa
kama akusanyaye masuke boondeni mwa
6 Refaim. Zitaachwa ndani yake za kumali-
za, kama kupigwa mzetuni, matunda mawi-



Digitized by Google
Original from HARVARD UNIVERSITY

li matatu katika kilele, manne matano kati-
ka matawi yaliyozaa sana, amesema Yahuwa,
Muungu wa Israeli.
7 Siku ile mtu atamwangalia aliyemfanya,
8 na macho yake yatamtazamia Mtakatifu wa
Israeli. Wala hataangalia mathbahu kazi
za mikono yake yeye, wala hatatazamia zi-
lizofanyika na vidole vyake ashera na ha-
9 mmani. Siku ile miji yake iliyo ya nguvu
itakuwa kama mwitu na milima waliyoiacha
mbele ya waana wa Israeli, itakuwa uharibu.
10 Kwani umemsahau Muungu wa wokovu
wako, wala hukumkumbuka mwamba wa
nguvu zako. Kwa hiyo utapanda mbegu za
11 kupendeza, na miche ya ugeni utatia. Kwa
siku utachipusha ulioupanda, na assubuhi
utafanya mbegu zako zimee, chungu cha
mavuno siku ya kurithi na ya huzuni iliyo
nzito.
12 Ole wao makutano ya watu wengi, kama
uvumi wa bahari wavuma, na sauti ya maji
13 yaliyo hodari italia. Watu kama sauti ya
maji mengi watalia. Atawapigia kelele,
watakimbia mbali, na kufukuzwa kama ma-



Digitized by Google
Original from
HARVARD UNIVERSITY

kapi milimani mbele ya upepo, na kama ki-
viringo mbele ya taabu, mbele ya assubuhi
hako. Ndiyo sehemu yao watutekao na ba-
hati yao watunyang'anyao.
XVIII. Ole wa inchi kivuli cha mabawa, iliyo
2 ng'ambo ya mito ya Kushi. Ipelekayo wa-
jumbe kwa bahari katika vyombo vya ma-
nyasi juu ya maji. Nendeni wajumbe we-
pesi, kwa taifa lililovutwa na lililochunika,
kwa watu wa hofu, tangu kuwa na tena,
taifa la kupima na kupima, ña kukanyaga,
inchi yao mito imeiharibu.
3 Enyi wakaao ulimwengu wote, na wake-
tio katika inchi, kwa kuinuliwa bandera
milimani mtaona, na kupigwa baragumu
4 mtasikia. Kwani ndilo niambialo Yahuwa,
nitastarehe, nitafikiri mahali pangu kama
hari ya kutakata juu ya mwanga, kama wi-
ngu la umande katika hari ya mavuno.
5 Kwani mbele ya mavuno, ilipopea mbegu,
na zabibu changa yaiva katika maua, ata-
kata vitanzi kwa miundo, ataondoa matawi,
6 atakatia mbali. Zitaachwa pamoja kwa
ndege za milimani na nyama za inchi, na



Digitized by Google Original from HARVARD UNIVERSITY

ndege zitakaa juu yao wakati wa hari, na
nyama zote za inchi zitakaa juu yao wa-
7 kati wa baridi. Wakati ule ataletewa za-
wadi Yahuwa wa majeshi na watu waliovu-
twa na waliochunika, na kwa watu wa hofu
tangu kuwa na tena, taifa la kupima na
kupima na kukanyaga, inchi yao mito ime-
iharibu, hatta mahali pa jina la Yahuwa wa
majeshi, mlima Sayuni.
XIX. Mzigo wa Misri. Yahuwa amepanda
juu ya wingu jepesi, ataingia Misri, sana-
mu za Misri zitatikisika mbele yake, na
moyo wa Misri utayeyuka ndani yake.
2 Nitachanganya Mmisri na Mmisri, watapi-
gana mtu na nduguye, na mtu na mwenza-
3 ke, mji na mji, ufalme na ufalme. Itazimia
roho ya Misri ndani yake, na shauri lake
nitalimeza, naye atafutaye kwa sanamu, na
kwa waganga, nao wenyi pepo, na wacha-
4 wi. Nitafunga Misri mkononi mwa bwana
mgumu, na mfalme hodari atawatawala,
5 amesema Bwana Yahuwa wa majeshi. Na
maji yatapunguka katika bahari, na mto
6 utakauka, utapotea. Nao watageuzia mba-



Digitized by Google
Original from
HARVARD UNIVERSITY

li mito, na vijito vya kulinda miji vitapu-
nguzwa, vitakauka, manyasi na makangaja
7 yatanyauka. Yameayo mtoni, pakutokea
mto, na yote yaliyopandwa mtoni yatakau-
8 ka, yatapotezwa hatta hapana. Nao wavu-
vi watalia, nao wote waliotupa doana kati-
ka vijito watahuzunika, nao walionyosha ja-
9 rifa juu ya maji watazimia. Nao tena wa-
tatiwa hamu wafanyao kitani kilicho safi,
10 na wafumao nyavu. Watavunjika tangu
asili wote wafanyao kufunga maziwa kwa
samaki.
11 Nao wapumbafu wakuu wa Zoani, wenyi
shauri wa hekima wa Farao. Shauri lime-
pumbazika. Mwambiaje Farao, Mwana wa
wenyi hekima mimi, mwana wa wafalme
12 wa zamani? Wako wapi sasa wenyi heki-
ma wako? Wakuonye sasa, wajue alivyo-
kusudia Yahuwa wa majeshi juu ya Misri.
13 Wamepumbazika wakuu wa Zoani, wameda-
nganyika wakuu wa Nof, wamekosesha Mi-
14 sri *walio* pembe za makabila yake. Yahuwa
ametia roho ya upoteo ndani yake, wame-
kosesha Misri katika kazi yake yote, kama



Digitized by Google
Original from
HARVARD UNIVERSITY

15 mlevi hukosa akitapika. Wala haitakuwa
kazi kwa Misri, ifanyike na kitwa ao mkia,
16 tawi ao nyasi. Siku ile itakuwa Misri ka-
ma waanaake, itatetemeka itaogopa mbele
ya kutikisika mkono wa Yahuwa wa maje-
17 shi autikisao juu yake. Itakuwa inchi ya
Yuda hofu kwa Misri, killa anenaye atai-
ngiwa na woga, mbele ya kusudi la Yahuwa
wa majeshi alilokusudia juu yake.
18 Siku ile itakuwa miji mitano katika inchi
ya Misri, inenayo maneno ya Kanaan, iapa-
yo kwa Yahuwa wa majeshi, mji wa uhari-
19 bifu utaitwa mmoja. Siku ile itakuwa
mathbahu kwa Yahuwa kati ya inchi ya
Misri, na nguzo mpakani mwake kwa Ya-
20 huwa. Itakuwa kwa ishara na kwa shahi-
di kwa Yahuwa wa majeshi katika inchi ya
Misri, kwani watamwitia Yahuwa mbele
yao waoneao, naye atawaletea mwokozi, na
21 mashuhuri, atakayewaponya. Atajulika
Yahuwa katika Misri, na Wamisri watam-
jua Yahuwa siku ile, watafanya thabihu, na
sadaka, wataweka nathiri kwa Yahuwa wa-
22 taiondoa. Atapiga Yahuwa Misri akipiga



Digitized by Google Original from HARVARD UNIVERSITY

na akiponya, nao watarudi kwa Yahuwa,
ataombewa nao, atawaponya.
23 Siku ile itakuwa njia katika Misri kwe-
nda Ashur, na Ashur ataingia katika Misri,
na Misri katika Ashur, wakitumika Wami-
24 sri na Ashur. Siku ile itakuwa Israeli ya
tatu na Misri na Ashur, mbaraka kati ya
25 inchi, aliyoibariki Yahuwa wa majeshi aki-
nena, Wamebarikiwa watu wangu Wamisri,
na kazi ya mikono yangu Ashur, na urithi
wangu Israeli.
XX. Mwaka wa kuja Tartan kwa Ashdod,
akimpeleka Sargon mfalme wa Ashur, aka-
2 pigana na Ashdod, akaitwaa. Wakati ule
akanena Yahuwa kwa mkono wa Isaya wa
Amoz, akinena, Nenda, kafungue sako ka-
tika kiunoni mwako, na viatu ufungue ka-
tika mguuni mwako, nikatenda nikaenda
3 mtupu na mguu wazi. Akanena Yahuwa,
Kama amekwenda mtumwa wangu Isaya
mtupu, pasipo viatu, kwa miaka mitatu isha-
ra na ajabu juu ya Misri, na juu ya Kushi.
4 Hivyo mfalme wa Ashur ataleta wafungwa
Wamisri, na kuhamishwa Kushi, vijana na



Digitized by Google Original from HARVARD UNIVERSITY

wazee, watupu na pasipo viatu, hatta mata-
5 ko matupu kwa utupu wa Misri. Watafa-
thaika, wataona haya kwa Kushi walioita-
6 zamia na Misri utukufu wao. Atanena a-
kaaye katika kisiwa hiki siku ile, Hivi ndi-
vyo tulivyotazamia, tulikokimbia kwa msa-
ada tuokoke mbele ya mfalme wa Ashur,
giusi gani tuvuke sisi?

XXI. Msigo wa unyika wa bahari. Kama
tufanu zipitavyo kusini, ndivyo uaja katika
2 unyika, katika inchi ya hofu. Matokeo
magumu yamehubiriwa kwangu; mjanja
hufanyiza ujanja, na mharibu huharibu.
Panda, Ee Elam: zunguka mji Ee Umedi;
3 kilio chake chote nimekikomesha. Kwani
viuno vyangu vimejaa kuuma, uchungu u-
menishika kama uchungu wa mwanamke
azaaye: naliinamishwa kwa kuusikia, na-
4 lishangaa kwa kuuona. Moyo wangu uka-
shtuka, hofu iliniogofisha, usiku wa furaha
5 yangu amenigeuzia kuwa woga. Tandi-
ka meza, kesha katika mnara wa kuke-
shea, ule, unywe: ondokeni enyi wakuu,
6 tieni mafuta katika ngao. Kwani hayo



Digitized by Google
Original from
HARVARD UNIVERSITY

ndiyo aliyoniambia Bwana, Nenda weka
mlinzi, akiona aonyeshe.
7 Akaona gari, wawili wapandao frasi, gari
la punda, gari la ngamia. Akaangalia kwa
8 kuangalia, kuangalia sana. Akalia, Simba.
Juu ya malindo, Bwana wangu, mimi kusi-
mama dayima mchana, na juu ya kuvisia
9 kwangu nakaa usiku kucha. Angalia, laja
gari la watu, wawili wapandao frasi.
Akajibu, akanena, Imeanguka, imeangu-
ka Babeli, na sanamu zote za miungu yao
10 ameivunja hatta inchi. Kufikicha kwangu,
na uzao wa sakafu yangu, niliyoyasikia kwa
Yahuwa wa majeshi Muungu wa Israeli ni-
mewahubiria ninyi.
11 Mzigo wa Duma. Kunililia katika Sair,
12 Mlinzi nini ya usiku, nini ya usiku? Aka-
nena mlinzi, Assubuhi yaja, na tena usiku,
ukiuliza ulize, ukirudi uje.
13 Mzigo wa Arabuni. Katika mwitu wa
Arabuni mtakaa, misafara ya Dedanim.
14 Akifika mwenyi kiu yaje maji, wakaao
inchi ya Tema na chakula chake wamta-
15 ngulie akimbiaye. Kwani mbele ya upa-



Digitized by Google
Original from
HARVARD UNIVERSITY

nga wamekimbia, mbele ya upanga uliofu-
twa, na mbele ya upindi uliopindwa, na
mbele ya uzito wa vita.
16 Kwani alivyoniambia Bwana, Bado mwa-
ka, kwa miaka yake mwenyi mshahara,
17 utaliwa utukufu wote wa Kedar. Na walio-
salia hesabu ya upindi, walio hodari, waana
wa Kedar watapunguka, kwani Yahuwa
Muungu wa Israeli amenena.
XXII. Mzigo wa boonde la kuona. Una nini
2 sasa, kwani mmepanda wote darini? U-
mejaa uthia, mji uliochafuka, mji wa fura-
ha, waliouawa kwako hawakuuawa kwa
3 upanga, wala hawakufa vitani. Wote wa-
kuu wako wamekimbia pamoja, kwa upindi
wamefungwa. Wote walioonekana kwako
wamefungwa pamoja, wamekimbia mbali.
4 Kwa hiyo nalisema, Angalieni mimi ni-
tajifanya mchungu kwa kulia, msifanye
hima kunituliza juu ya uharibifu wa binti
5 wa watu wangu. Kwani siku ya kuponda,
na kukanyaga, na kutatanika, kwa Bwana
Yahuwa wa majeshi katika boonde la kuo-
na, ya kutoboa ukuta na kulia kwa mlima.



Digitized by Google
Original from
HARVARD UNIVERSITY

6 Elam wakachukua podo na magari ya
watu, wapandao frasi, na Kir wakafunua
7 ngao. Ikawa uteule wa maboonde yako
umejaa magari, na wapandao frasi kupanga
wamejipanga mlangoni.
8 Akafunua kufunika Yuda, ukatazama si-
9 ku ile selaha za nyumba ya mwitu. Mka-
ona mavunjiko ya nyumba ya Daud, kwani
yamezidi, mkakusanya maji ya birika la
10 chini, mkahasibu nyumba za Yerusalemi,
mkaharibu nyumba kwa kazi ya ukuta.
11 Mkafanya mahali kati ya kuta mbili kwa
maji ya birika la kale, wala hamkumwa-
ngalia aliyelifanya, wala hamkumtazama ali-
yelifanyiza zamani.
12 Akaita Bwana Yahuwa wa majeshi siku
ile kwa kulia, na kuomboleza, na kufanya
13 kitwa kiwazi, na kuvaa sako. Illa iko fu-
raha na kucheka, kuchinja ng'ombe, na
kuchinja kondoo, kula nyama na kunywa
mvinyo, kula na kunywa kwani kesho tuta-
kufa.
14 Nikafunuliwa sikioni na Yahuwa wa ma-
jeshi, hautatakasika uovu huu kwenu msipo-



Digitized by Google
Original from HARVARD UNIVERSITY

kufa, amesema Bwana Yahuwa wa majeshi.
15 Akanena Bwana Yahuwa wa majeshi,
Nenda ingie kwa yule mtunza hazina Sheb-
16 na aliye juu ya nyumba. Una nini hapa,
nani wako hapa, kwani umejichongea hapa
kaburi, kujichongea kaburi, ukifanya ma-
17 sikani katika mwamba? Naye Yahuwa
kuchukua atakuchukua kabisa, na kuficha
18 atakuficha. Kutupa atakutupatupa, kama
mpila katika inchi ya nafasi nyingi, huko
utakufa, na huko magari ya utukufu wako,
19 aibu ya nyumba ya bwana wako. Nitakuo-
ndoa katika mahali pako, na katika hali
yako atakuangusha.
20 Itakuwa siku ile, nitamwita Eliyakim wa
21 Hilkiya, nitamvika kwa vazi lako na kwa
mshipi wako nitamtia nguvu, uwezo wako
nitampa mkononi mwake, atakuwa baba
wa akaaye Yerusalemi na nyumba ya Yuda.
22 Nitaweka ufunguo wa nyumba ya Daud juu
ya bega lake, atafungua wala hapana afu-
ngaye, atafunga wala hapana afunguaye.
23 Nitamkaza kama msomari mahali imara,
naye atakuwa kiti cha utukufu kwa nyumba



Digitized by Google
Original from
HARVARD UNIVERSITY

24 ya baba wake. Wataangisha juu yake utu-
kufu wote wa nyumba ya baba wake, uzao na
uzidi, killa chombo kidogo, tangu vyombo
vya vikombe hatta vyombo vya makopo.
25 Siku ile, amesema Yahuwa wa majeshi,
utaondolewa msomari uliokazwa mahali
imara, utakatika, utaanguka, utakatika ulio
juu yake, kwani Yahuwa amenena.
XXIII. Mzigo wa Turo. Pigeni yowe, meri-
kebu za Tarshishi, kwani imeharibika, ha-
pana nyumba, hapana kuingia, katika inchi
2 ya Kitim wamefunuliwa. Nyamazeni wa-
kaao kisiwani, wasafiri wa Zidoni wakipita
3 bahari waliokujaza. Katika maji mengi
uzao wa Sihor, mavuno ya mito pato lake,
ndiye soko la mataifa.
4 Uone haya, Ee Zidoni, kwani bahari
nguvu ya bahari imenena, Sikufanya utu-
ngu wala sikuzaa, wala sikulea vijana wala
waanawali.
5 Kama habari za Misri, wataona uchungu
6 wakisikia ya Turo. Piteni hatta Tarshishi,
7 pigeni yowe mkaao kisiwani. Ndiyo hiyo
furaha yenu, tangu siku za zamani za kale,



Digitized by Google
Original from HARVARD UNIVERSITY

8 miguu yake itamleta mbali kusafiri. Nani
aliyefanya shauri hii juu ya Turo utiaye taji,
wafanyi biashara wake wakuu, matajiri wa-
9 ke wenyi jina katika inchi. Yahuwa wa
majeshi amefanya shauri hii, atie aibu ka-
tika kiburi chote, aangamize wote wenyi
jina katika inchi.
10 Upite inchi yako kama mto, Binti Tara-
11 shishi, hapana tena kujifunga. Alinyosha
mkono wake juu ya bahari akazitia hofu falu-
me, Yahuwa akaamuru juu ya tajiri, kupo-
12 teza nguvu zake, akanena, Usizidi kufura-
hi, kijana aliyeonewa, binti Zidoni, ondoke
Kitim, upite hatta huko huna kustarehe.
13 Iko inchi ya Wakasidi, watu hawa ha-
wakuwa, Ashur akaifanya kwa wale walio-
kaa jangwani, wakaweka minara yake, wa-
kainua majumba yake, akaifanya uharibifu.
14 Pigeni yowe, enyi merikebu za Tarashi-
15 shi, kwani nguvu zenu zimeharibika. Ita-
kuwa siku ile, Turo itasahauliwa miaka sa-
bwini kwa siku za mfalme mmoja. Hatta
mwisho wa miaka sabwini Turo itakuwa
16 kama kahaba aimbaye. Twae kinubi, uzu-



Digitized by Google Original from HARVARD UNIVERSITY

nguke mji, Ee kahaba uliyesahauliwa, upi-
ge vizuri, uzidishe nyimbo, upate kuku-
mbukwa.
17 Itakuwa mwisho wa miaka sabuini Ya-
huwa atajia Turo, utarudi kwa biashara
yake, utafanya asharati na wafalme wote
18 wa ulimwengu juu ya uso wa inchi. Na
biashara yake na ijara yake itakuwa uta-
katifu kwa Yahuwa. Haitafichwa wala
haitawekwa, kwani kwao wakaao mbele ya
Yahuwa itakuwa biashara yake, kwa kula
hatta kushiba, na kwa mafuniko ya kale.
XXIV. Angalia, Yahuwa aifanya inchi tupu,
aifanya jangwa, apindua uso wake, awata-
2 wanya wakaao humo. Itakuwa kama watu
hivi mkohani, kama bwana hivi mtumwa,
kama mjakazi hivi bibi wake, kama anunu-
aye hivi akuzaye, kama akopeshaye hivi a-
kopaye, kama atwaaye amana, hivi aweka-
ye amana.
3 Kufanyika tupu, inchi itafanyika tupu,
kuharibika itaharibika, kwani Yahuwa ame-
4 nena neno hili. Imezimia, imeyeyuka inchi,
umethoofika umevivia ulimwengu, wame-



Digitized by Google

Original from
HARVARD UNIVERSITY

4 thoofika watu wa inchi walio wakuu. Inchi
tena imedanganya chini ya wakaao, kwani
wamezikosa sheria, wamebadili haki, wa-
mevunja agano la milele.
5 Kwa hiyo laana limeila inchi, wamea-
ngamia wakaao humo, kwa hiyo wameliwa
na moto wakaao inchi, watasalia watu wa-
7 chache. Umezimia mvinyo mpya, ume-
thoofika mzabibu, wameugua wote wenyi
8 moyo wa furaha. Imekoma shangwi la
ngoma, imekwisha sauti yao wafurahio,
9 imekoma shangwi la kinubi. Kwa nyimbo
hawanywi mvinyo, kichungu kileo kwao
10 wanywao. Umepondeka mji wa ubatili,
imefungwa killa nyumba katika kuingia.
11 Kulia kwa mvinyo njiani, imetiwa giza
furaha yote, limekwenda zake shangwi la
12 inchi. Imekaa mjini ukiwa na uharibifu
umeuvunja mlango.
13 Kwani hivi itakuwa ndani ya inchi, kati
ya watu, kama kupigwa mzetuni, kama za-
14 bibu walipokwisha kuchuma. Hawa wata-
paliza sauti yao, watapiga kigelegele kwa
ukuu wa Yahuwa, wataita katika bahari.



Digitized by Google
Original from
HARVARD UNIVERSITY

15 Kwa hiyo maboondeni mtukuzeni Yahuwa,
katika visiwa vya bahari jina la Yahuwa
16 Muungu wa Israeli. Katika upande ya
inchi tumesikia uimbo, utukufu kwa mta-
katifu. Nikanena, hasara yangu, hasara
yangu, ole wangu, waliodanganya wame-
danganya, kudanganya wadanganyao wa-
medanganya.
17 Hofu, na shimo, na mtego juu yako, Ee
18 ukaaye inchi. Itakuwa akimbiaye sauti ya
hofu, ataanguka shimoni, apandaye katika
kati ya shimo, atanaswa na mtego, kwani
madirisha ya juu yamekuwa wazi, zitate-
19 meka zilizo chini ya inchi. Kuvunjikavu-
njika imevunjika inchi, kutawanyika ime-
tawanyika inchi, kutikisika imetikisikati-
20 kisika inchi. Kulewa imelewa inchi kama
mlevi, itahamishwa kama kibanda, zito juu
yake kosa lake, itaanguka, haitapata kuo-
ndoka.
21 Itakuwa siku ile atakuja Yahuwa juu ya
jeshi lao wa juu walio juu, na juu ya wafal-
22 me wa dunia walio duniani. Watakusanyi-
ka kwa kukusanyika waliofungwa katika



Digitized by Google

Original from
HARVARD UNIVERSITY

shimo, watafungwa katika pa kufungwa,
katika siku zilizo nyingi watajiliwa.
23 Utageuka mwezi, litatahayirika jua, kwa-
ni amemiliki Yahuwa wa majeshi katika
mlima Sayuni, na katika Yerusalemi, na
mbele ya wazee wake kwa utukufu.
XXV. Yahuwa Muungu wangu ndiwe, nitaku-
tukuza, nitakuungama jina lako, kwani u-
metenda ajabu, mashauri ya zamani, kweli,
2 amini. Kwani umefanya mji kuwa chungu,
mji mwenyi boma maanguko, jumba la wa-
geni katika mji, milele usijengwe.
3 Kwa hiyo watakutukuza watu wa nguvu,
4 mji wa mataifa wa hofu watakuogopa. Kwa-
ni ulikuwa nguvu wake thaifu, nguvu yake
fukara katika shidda yake, kuhifathi katika
tufanu, kivuli katika hari, kwani kuvuma
5 kwao hofu kama tufanu ukutani. Kama
hari pakavuni sauti ya wageni utaishusha,
hari kwa kivuli cha wingu, tawi lao la hofu
itashushwa.
6 Atafanya Yahuwa wa majeshi, kwa watu
wote katika mlima huu, karamu ya mano-
no, karamu ya mvinyo mzito, manono ya



Digitized by Google
Original from
HARVARD UNIVERSITY

mabongo, mvinyo mzito ulio safi.
7 Ataharibu katika mlima huu uso wa ki-
funiko cha kufunika watu wote na pazia la
8 kusetiri juu ya mataifa yote. Ataharibu
kufa hatta milele, atafuta Bwana Yahuwa
machozi juu ya nyuso zote, aibu ya watu
wake ataiondoa katika inchi yote, kwani Ya-
huwa amenena.
9 Na kunena siku ile, Huyu Muungu wetu
ndiye tuliyemngoja, atatuokoa, ndiye Ya-
huwa tuliyemngoja, tutapendezwa tutafura-
hiwa kwa wokovu wake.
10 Kwani utakaa mkono wa Yahuwa katika
mlima huu, watakanyagwa Moabi chini ya-
ke; kama kukanyagwa majani katika jaa.
11 Atanyosha mikono yake kati yake kama a-
nyoshavyo aogoleaye aogolee, atanenyeke-
za kuinuka kwake kwa maoteo ya mikono
12 yake. Na boma la juu la kuta zake ataina-
misha, atashusha, ataleta chini hatta mavu-
mbini.
XXVI. Siku ile utaimbwa uimbo huu katika
inchi ya Yuda. Mji wa nguvu kwetu, wo-
2 kovu atatia kwa kuta na maboma. Funu-



Digitized by Google
Original from
HARVARD UNIVERSITY

eni milango waingie taifa la haki, lishikalo
3 maamini. Mwenyi nia imara utamlinda sa-
lamu salamu, kwani ndiwe amwaminiye.
4 Mwamininі Yahuwa hatta milele, kwani
kwa Yah Yahuwa mwamba wa milele.
5 Kwani atainamisha wakaao juu, mji ulioi-
nuka ataushusha, ataushusha hatta inchi, a-
6 tafikisha hatta mavumbini. Umekanya-
gwa na mguu, miguu wake fukara, hatua
zao wanyonge.
7 Njia yake mwenyi haki ni adili, kwa adili
8 aendavyo mwenyi haki atavipima. Na nji-
ani mwa hukumu zako, Yahuwa, tumeku-
ngoja. Kwa jina lako na kukukumbuka
ni tamaa ya roho yetu.
9 Kwa nafusi yangu nimekutamani usiku,
kwa roho yangu assubuhi nakutafuta, kwa-
ni hukumu zako zilipo katika inchi wali-
mwengu watajifunza haki.
10 Mbaya akipendelewa hatajifunza haki,
katika inchi ya wema atatenda vibaya, wa-
11 la hataona ukuu wa Yahuwa. Yahuwa u-
meinuka mkono wako, hawataona? Wata-
ona, watatahayarika kwa hasidi kwa watu



Digitized by Google

Original from
HARVARD UNIVERSITY

wako, hatta na moto adui zako wataliwa.
12 Yahuwa, utafanya amani kwetu, kwani na
13 matendo yetu yote umeyatenda kwetu. Ya-
huwa Muungu wetu, bwana wasio wewe
wametumiliki, kwa wewe peke yako tuta-
14 kumbuka jina lako. Wamekufa hawatai-
shi, wafu, hawafufuki, kwani umewajia, u-
mewafutia mbali, umepoteza kuwakumbuka
kwote.
15 Umelizidisha taifa, Yahuwa, umelizidisha
taifa, umejitukuza, umefarikisha hatta mwi-
sho wa inchi.
16 Yahuwa katika shidda wamekujia, wali-
kutolea neno la siri, kurudi kwako kwao.
17 Kama azaaye wakati wa kuzaa ukikaribia
huona utungu, aliavyo katika utungu wake,
18 hivi tulikuwa mbele yake Yahuwa. Tu-
mekuwa na mimba, tumeona uchungu, tu-
mezaa kama upepo, wokovu haukufanyika
katika inchi, wala hawakuanguka wakaao
ulimwenguni.
19 Wahayi waliokufa wako, na mayiti ya-
ngu watafufuka. Ondokeni, imbeni, mka-
ao mavumbini, kwani umande wa vijiti,



Digitized by Google Original from HARVARD UNIVERSITY

umande wako, na inchi atawatupa wafu.
20 Haya, watu wangu, ingie katika ndani
kwako, ufunge mlango wako juu yako.
Ujifiche kama kidogo cha wakati, hatta
21 ipitapo hasira. Kwani yuko Yahuwa aki-
toka katika mahali pake, awajie wakaao
inchi juu ya ubaya, inchi itaonyesha damu
zake, wala haitafunika tena walionawa kwa-
ke.

XXVII. Siku ile atakuja Yahuwa kwa upa-
nga wake mzito, na mkubwa, na hodari,
juu ya Lewiathani, nyoka apenyaye, na juu
ya Lewiathani, nyoka aliyepotoka, atamua
2 nyamgumi aliye baharini. Siku ile miza-
bibu ya mvinyo mwekundu, umwimbie.
3 Mimi Yahuwa nailinda, killa wakati naitia
maji, kitu kisije juu yake, mchana na usiku
4 nitailinda. Hasira hapana kwangu, nani
atakayepanga juu yangu mbigili na miiba,
ningekwenda vitani juu yao, nitaiteketeza
5 pamoja. Ao anishike nguvu zangu afanye
amani nami, amani ataifanya nami.
6 Atawafanyia shina watokao Yakobo, Isra-
eli atasitawi, atatoa mafundo ya maua, wa-



Digitized by Google
Original from
HARVARD UNIVERSITY

tajaza uso wa ulimwengu kwa mazao.
7 Amempiga kwa pigo lao waliompiga, ao
kwa kuuawa kwao waliomua ameuawa?
8 Kwa kiasi ikitoka utaihukumu, azuia upepo
wake mbali siku ya matlai.
9 Hivi kwa hiyo utastirika uovu wa Yakob,
na hiyo uzao wote wa kumwondolea thambi
yake, kuweka mawe yote ya mathbahu,
kama mawe ya chokaa yaliyopondwa, ha-
yatasimama maashera wala sanamu za jua.
10 Kwani mji mwenyi boma peke yake, ma-
kao yaliyoachwa yaliyotupwa kama jangwa,
huko hula ndama, na huko atalala, atakula
11 matawi yake. Matanzi yake yakikauka
yatavunjiwa mbali, waanaake wakija waki-
yatia motoni, kwani si watu wenyi akili ha-
wa. Kwa hiyo aliyewafanya hatawahuru-
12 mia, aliyewaumba hatawarehemu. Itakuwa
siku ile, Yahuwa atang'utia mbali katika
mahali pa mto wa maji hatta wadi wa Misri,
nanyi mtakusanyika, mmoja mmoja, Ee
waana wa Israeli.
13 Itakuwa siku ile litapigwa paanda kuu,
watakuja waliopotea katika inchi ya Ashur,



Digitized by Google
Original from
HARVARD UNIVERSITY

nao waliofukuzwa katika inchi ya Misri,
watamwinamia Yahuwa katika mlima wa
utakatifu katika Yerusalemi.

XXVIII. Ole taji ya kiburi kwa walevi wa
Efraim, na ua likaukalo uzuri wa fahari ya-
ke, iliyo kitwani mwa maboonde ya vinono,
2 iliyoharibika na mvinyo. Naye yuko kwa
Yahuwa aliye hodari, mwenyi nguvu, kama
kumwagika mvua ya mawe, tufano la kuvu-
nja, kama gharika la maji yafurikayo mno,
3 akatupa chini kwa mkono. Kwa miguu
watakanyagwa, taji ya kiburi, walevi wa
4 Efraim. Itakuwa, ua likaukalo uzuri wa
fahari yake, aliye juu kitwani mwa ma-
boonde ya vinono, kama pevu la kwanza
mbele ya wakati wa hari, akiona aonaye
hatta mkononi mwake humeza.

5 Siku ile atakuwa Yahuwa wa majeshi
kwa taji la uzuri, na kilemba cha fahari,
6 kwao waliosalia wa watu wake. Na kwa
roho ya hukumu kwake akaaye kwa huku-
mu, na kwa nguvu kwao wageuzao vita ka-
tika mlangoni.

7 Nao tena wamekosa kwa mvinyo, na kwa



Digitized by Google

Original from
HARVARD UNIVERSITY

kileo wamepotea, mkohani na nabii wame-
kosa kwa kileo, wamezama kwa mvinyo,
wamepotea kwa kileo, wamekosa katika
8 njozi, wamejikwaa katika hukumu. Kwani
meza zote zimejaa matapiko, uchafu, hapa-
na mahali.

9 Nani atakayemfunza maarifa, nani ata-
kayemfahamisha asikiayo, wakomao katika
10 maziwa, walioacha matiti? Kwani amri kwa
amri, amri kwa amri, mstari kwa mstari,
mstari kwa mstari, kidogo huko na kidogo
11 huko. Kwani kwa midomo ya kigugumizi,
na kwa ulimi mgeni atasema na watu hawa.
12 Walioambiwa naye, Raha hii, mpe raha ali-
yechoka, na hii kupumzika, wala hawakupe-
13 nda kusikia. Itakuwa kwao, neno la Ya-
huwa, amri kwa amri, amri kwa amri, mstari
kwa mstari, kidogo huko, kidogo huko, wa-
ende, waanguke nyuma, wapondeke, wana-
swe watwaliwe.

14 Kwa hiyo sikieni neno la Yahuwa, watu
wa thihaka, wakuu wa watu hawa, walio
15 katika Yerusalemi. Kwani mmenena, Tu-
mepatana na kufa, na kaburi tumeagana,



Digitized by Google
Original from
HARVARD UNIVERSITY

pigo la gharika likipita halitafika kwetu,
kwani tumeweka katika uwongo taraja yetu,
na katika udanganifu tumestirika.
16 Kwa hiyo ndivyo anenavyo Bwana Yahu-
wa, Ndimi niwekaye katika Sayuni jiwe,
jiwe la jaribu, pembe ya thamani, msinji wa
17 msinji, aaminiye asifanye hima. Nitaweka
na hukumu ya kamba, na haki ya timazi,
mvua ya mawe itapindua taraja ya uwongo,
18 na setiri litafunikizwa na maji. Litabatili-
ka patano lenu na kufa, wala agano lenu
na kaburi halitasimama, pigo la gharika li-
19 kipita, mtakuwa kukanyagwa nalo. Ta-
ngu kupita litawatwaa, kwani assubuhi as-
subuhi litapita, mchana na usiku, itakuwa
20 kutaharuki tu, kupata kuisikia. Kwani ki-
fupi kitanda asijinyoshe, na kifuniko che-
mbamba asijikunjie.
21 Kwani kama katika mlima Perazim ata-
ondoka Yahuwa, kama katika boonde la Gi-
beon ataona hasira, atende tendo lake, te-
ndo lake la ajabu, afanye kufanya kwake,
22 kufanya kwa mwujiza. Wala tena msithi-
haki, illi msifanye hodari minyororo yenu,



Digitized by Google

Original from HARVARD UNIVERSITY

kwani kumaliza, na kumekatwa, nimesikia
kwa Bwana Yahuwa wa majeshi juu ya in-
chi yote.
23 Pokeeni masikioni, sikieni sauti yangu,
24 pulikeni mkasikie neno langu. Ndiyo mcha-
na kutwa alima alimaye, kwa kupanda afu-
25 nua, avunjavunja udongo wake. Alipote-
ngeneza uso wake, hutawanya ketza, anyu-
nyiza kamina, aweka ngano iliyo kuu, na
shayiri mahali pake, na kusemeth mpakani
26 mwake. Huandika kwa hukumu, Muungu
27 wake amfundishaye. Kwani ketza haipi-
gwi kwa gongo, wala kuzunguka gurudumu
juu ya kamina, illa kwa fimbo hufikichwa
28 ketza, na kamina kwa fito. La mkate hu-
chubuka, kwani sikuzote hatalifikichafiki-
cha, wala hataliponda kwa gurudumu la ga-
ri lake, wala kwa frasi zake hatalichubua.
29 Hatta haya yatoka katika kwa Yahuwa
wa majeshi, amefanya shauri la ajabu, ame-
fanya tendo bora.
XXIX. Ole wa Ariel, simba wa Muungu, mji
alimokaa Daudi, ongezeni mwaka juu ya
2 mwaka, waana kondoo wachinjwe. Nimefa-



Digitized by Google Original from HARVARD UNIVERSITY

nya shidda kwa Ariel, itakuwa kuomboleza
3 na kulia, itakuwa kwangu kama Ariel. Ni-
tatua kuzunguka juu yako, nitakufunga kwa
4 boma, nitafanya minara juu yako. Utaji-
shusha, utanena katika inchi, na mavumbi-
ni, neno lako litakuwa chini, itakuwa kama
mwenyi pepo katika inchi sauti yako, na
katika mavumbi neno lako litanong'onia.
5 Itakuwa kama mavumbi madogo, wingi wa
wageni wako, na kama makapi yapitayo
wingi wao wenyi hofu, itakuwa marra ghá-
fula.

6 Katika kwa Yahuwa wa majeshi utajili-
wa kwa umeme, na ngurumo, na sauti kuu,
kwa chamchela, na tufano, na ulimi wa mo-
to uunguzao.

7 Itakuwa kama ndoto ya usiku, wengi wa
mataifa yote wakipigana na Ariel, na wote
wapiganao nao, maboma yake, na wautiao
8 shidda. Itakuwa kama aotaye na njaa, na-
ye anakula, akiamka roho yake hana kitu,
na kama aotaye na kiu, naye anakunywa,
akiamka naye mchovu, na nafusi yake ata-
mani, hivi utakuwa wingi wa mataifa yote



Digitized by Google

Original from
HARVARD UNIVERSITY

wapiganao juu ya mlima Sayuni.
9 Jizuieni, taajabuni, mpige kelele mkalie,
wamelewa illa si kwa mvinyo, wamewaya-
10 waya illa si kwa kileo. Kwani Yahuwa
amemimina juu yenu roho ya usingizi, ame-
fumba macho yenu, manabii na wakuu wenu,
11 waonao amewafunika. Itakuwa kwenu wa-
onayo yote kama maneno ya kitabu kilicho-
tiwa muhuri, akipewa aliye na elimu, kune-
na, Soma hiki, asema, siwezi, kwani kime-
12 tiwa muhuri, akipewa kitabu asiye na eli-
mu kunena, Soma hiki, asema, Sijui kita-
bu.

13 Akanena Yahuwa, Kwa sababu watu ha-
wa wamenikaribia kwa kinwa, na kwa mi-
domo wameniheshimia, na moyo wao mbali
yangu, ikawa kwa hofu yao kwangu imefu-
14 ndishwa amri ya watu. Kwa hiyo mimi
nitazidi kwa miujiza kwa watu hawa, miu-
jiza na ajabu, itapotea hekima yao wenyi
hekima, na akili za wenyi akili hazitaoneka-
na.

15 Ole wao waendao chini sana wafiche kwa
Yahuwa shauri yao, na katika giza kazi



Digitized by Google
Original from
HARVARD UNIVERSITY

zao, wakisema, Nani atuonaye na atuju-
16 aye? Mkipindua vitu, itafanana na udo-
ngo wa mfinangi, kwani kazi imwambie a-
liyeifanya, Hakunifanya? Na chombo ki-
mwambie aliyekiumba, Hakufahamu?
17 Siyo tena muda mdogo na Lebanon ita-
geuka kuwa Karmel, na Karmel itathaniwa
18 mwitu? Watasikia siku ile viziwi maneno
ya kitabu, na katika weusi na katika giza
19 macho ya vipofu yataona. Watazidi wenyi
upole kwa Yahuwa kufurahiwa, na masiki-
ni wa watu, kwa Mtakatifu wa Israeli wata-
pendezewa.
20 Kwani atakoma wa hofu, na atatoweka
mdanganya, watakatika wote walindao u-
21 ovu, wamfanyia mtu akose kwa neno, na-
ye arudiye mlangoni wamtegeao mitego,
wageuzao haki kwa kitu kisichofaa.
22 Kwa hiyo asemavyo Yahuwa kwa nyu-
mba ya Yakobo, aliyemkomboa Ibrahimu,
hatatahayarika Yakobo kwa haya, wala te-
23 na uso wake usikose rangi yake. Kwani
akiona watoto wake, kazi ya mikono yangu
ndani yake, watatakasa jina langu, wata-



Digitized by Google
Original from
HARVARD UNIVERSITY

mtakasa Mtakatifu wa Yakobo, na Mun-
24 ngu wa Israeli watamwogopa. Watajua
busara waliokosa rohoni, na walionong'onia
watajifunza elimu.

XXX. Ole wa watoto waasi, amesema Yabuwa,
wafanyao shauri, illa si kwa mimi, wafuni-
kao funikizo illa si roho yangu, waongeze
2 thambi kwa thambi. Waendao kushuka
Misri, wala kinwa changu hawakuniuliza,
wajifanye nguvu kwa nguvu za Farao, wa-
hifathike na kivuli cha Misri.

3 Itakuwa kwenu nguvu za Farao kwa aibu,
na kuhifathika na kivuli cha Misri shutumu.
4 Kwani walikuwa katika Zoan wakuu wake,
5 na wajumbe wake wakafika Hanes. Wo-
te wakaona haya kwa watu wasiowafaa,
wala kuwa msaada, wala kuwafaa, illa kwa
haya na kwa aibu.

6 Mzigo wa nyama za kusini, katika inchi
ya shidda, na taabu, simba kwao na mwana
simba, nyoka na joka la moto lirukalo.
Watachukua juu ya mabega ya punda ma-
li zao na juu ya nyundu ya ngamia hasina
7 zao, kwa watu wasiowafaa. Kwani Wamis-



Digitized by Google Original from HARVARD UNIVERSITY

ri burre na pasipo kufaa watasayidia. Kwa
hiyo nimeita kwa haya, nguvu zao kukaa.
8 Bassi ingie, andike juu ya meza kwao,
na katika kitabu uweke, itakuwa hatta si-
9 ku ya mwisho dayima hatta milele, ya kwa-
mba watu waasi hawa, waana wa uwongo,
waana wasiopenda kusikia sheria ya Yahu-
10 wa. Wawaambiao waonao msione, na wa-
tazamao msitutazamie ya kweli, mtuambie
11 mororo, mwone madanganifu. Tokeni ka-
tika njia, mkose katika mapito, mkomeshe
Mtakatifu wa Israeli katika mbele yetu.
12 Kwa hiyo amenena Mtakatifu wa Israeli,
Kwa sababu mmekataa neno hili, mmetara-
ja kwa jeuri na upotoe, ukategemea juu yao.
13 Kwa hiyo itakuwa kwenu ubaya huu kama
ufa wa kuanguka, ukivimba katika ukuta
mrefu, gháfula marra moja utakuja kuvu-
14 njika kwake. Atauvunja kama chombo cha
udongo, kuponda haachi, wala hakitaone-
kana katika vipande vyake kigai cha kupa-
sha moto katika kuungua, wala kuteka ma-
ji katika kisimani.
15 Kwani ndiyo asemayo Bwana Yahuwa,



Digitized by Google
Original from
HARVARD UNIVERSITY

Mtakatifu wa Israeli, katika kustarehe na
kutulia mtaokoka, katika kunyamaza na
kutumaini zitakuwa nguvu zenu. Wala
16 hamkukubali. Mkanena, Siyo, kwani juu ya
frasi tutakimbia, kwa hiyo mtakimbia, na
juu ya mwepesi tutapanda, kwa hiyo wepe-
17 si wawafuata. Elfu moja mbele ya kuke-
mea mmoja, mbele ya kukemea watano mta-
kimbia, hatta mtakaa kama mlingote juu
ya kilele cha mlima, na kama bandera kili-
mani.

18 Kwa hiyo atangoja Yahuwa, awahurumie,
na kwa hiyo atatukuka, awarehemu. Kwa-
ni Muungu wa hukumu Yahuwa, heri wote
19 wamngojao. Kwani watu wa Sayuni wata-
kaa katika Yerusalemi, kulia hutalia, kure-
hemu atakurehemu kwa sauti ya kilio cha-
20 ko, akisikia atakujibu. Akiwapa Yahuwa
chakula cha shidda na maji ya kuonewa,
hataondolewa tena waalimu wako, na macho
21 yako yatawaona waalimu wako. Masikio
yako yatasikia neno nyuma yako, kunena,
Hii njia, upite kwa hiyo, ukienda kwa kuu-
me, ao kwa kushoto.



Digitized by Google
Original from HARVARD UNIVERSITY

22 Mtatia unajisi funiko la sanamu za fetha
zako, na setiri la thamani la thahabu yako,
utatupia mbali kama nguo za heth, utaia-
23 mbia, Toka hapo. 'Naye atatoa mvua ya
mbegu zako, utakapopanda inchi, na cha-
kula cha uzao wa inchi. Itakuwa nene, na
nono, siku ile ng'ombe zenu watakula kati-
24 ka malisho mapana. Na ng'ombe tena na
waana punda, walimao inchi, watakula cha-
kula safi, kilichopeperushwa kwa ungo na
25 kwa pepeo. Na juu ya killa mlima mrefu, na
juu ya killa kilima kilichoinuka, mito, mito
ya maji, siku ya kuua wengi, iangukapo
26 minara. Itakuwa nuru ya mwezi kama nuru
ya jua, na nuru ya jua marra saba kama nu-
ru ya siku saba, siku ya kuganga Yahuwa
machubuko ya watu wake, na kuponya je-
raha ya pigo lao.
27 Liko jina la Yahuwa laja katika mbali,
ikiwaka hasira yake, na uzito wa mzigo,
midomo yake imejaa ghathabu na ulimi wa-
28 ke kama moto uunguzao. Na roho yake
kama mto ufurikao hatta kati ya shingo
itafika, kupepeta mataifa katika ungo wa



Digitized by Google
Original from
HARVARD UNIVERSITY

ubatili, na hatamu ya kukosesha katika
mataya ya watu.
29 Mtakuwa na uimbo kama usiku wa ku-
takasa idi, na furaha ya moyoni kama kwe-
nda na filimbi kuingia kwa mlima wa Ya-
30 huwa kwa mwamba wa Israeli. Atasikiza
Yahuwa uwezo wa sauti yake, na kushuka
mkono wake, ghathabu ya hasira, na ulimi
wa moto uwakao, kutawanya, na chamche-
31 la, na mvua ya mawe. Kwani kwa sauti ya
Yahuwa, atapondeka Ashur, apigaye na
32 bakora. 'Na killa pahali lipitapo gongo le-
nyi imara, aliloliweka Yahuwa juu yake,
kwa ngoma, na kwa vinubi, na kwa vita za
kutikisa atapigana naye.
33 Kwani imetengenezwa tangu zamani To-
feti, nayo kwa mfalme imekuwa tayari,
akaifanya kwenda chini, akapanua, tanuru
lake moto na kuni tele, pumuzi ya Yahuwa
kama mto wa kiberiti iwakao humo.
XXXI. Ole wao washukao Misri kwa msaada,
na juu ya frasi wategemea, wakataraja kwa
magari, kwani mengi, na kwa wapandao
frasi kwani hodari sana, wala hawakumwa-



Digitized by Google
Original from
HARVARD UNIVERSITY

ngalia Mtakatifu wa Israeli, wala Yahuwa
2 hawakumtaka. Naye mwenyi hekima ata-
leta mabaya, wala maneno yake hataondoa.
Atasimama juu ya nyumba wa wabaa, na
juu ya msaada wao watendao maovu.
3 Nao Wamisri watu, wala si Muungu, na
frasi zao nyama wala si roho. Na Yahuwa
atainamisha mkono wake, naye msayidia
atapotea, ataanguka aliyesayidiwa, na wote
pamoja watakoma.
4 Kwani ndivyo aniambiavyo Yahuwa,
kama simba angurumavyo, na mwana si-
mba juu ya mawindo yake, wakipiga kelele
juu yake wengi wachunga, hakutiwa hofu
kwa sauti zao, wala kwa uthia wao hakuji-
thili, hivi atashuka Yahuwa wa majeshi
apigane juu ya mlima Sayuni na juu ya
5 kilima chake. Kama ndege zirukavyo,
hivi atalinda Yahuwa wa majeshi juu ya
Yerusalemi, kuhifathi na kuweka huru,
kupita juu na kuokoa.
6 Geukeni kwake waliyemwasi mno waana
7 wa Israeli. Kwani siku ile atatupia mbali
killa mtu mabatili ya fetha yake na mabatili



Digitized by Google

Original from
HARVARD UNIVERSITY

za thahabu yake, mliyojifanyia mikono ye-
8 nu, thambi. Ataanguka Ashur kwa upa-
nga sio wa mume, na upanga sio wa mtu
utamla. Atakimbia mbele ya upanga, na
9 vijana vyake watatoa kodi. Naye atapita
kwa mwamba wake kwa hofu, na wakuu
wake wataogopa kwa bandera, amesema
Yahuwa mwenyi moto katika Sayuni, na
tanuru yake katika Yerusalemi.

XXXII. Yuko kwa haki atakayemiliki mfalme,
2 na wakuu kwa hukumu watatawala. Ita-
kuwa mtu kama kisetiri kwa upepo, na fi-
cho kwa tufano, kama mito ya maji mahali
pakavu, na kivuli cha mwamba mkubwa
katika inchi ya kiu.

3 Hayataona kiwi macho yao waonao, na
4 masikio yao wasikiao yatasikiliza. Moyo
wake mpesi mno utajua maarifa, na ulimi
wake bubu utafanya hima kunena kwa wa-
5 zi. Hataitwa tena mnyonge mkarimu,
wala mnyima hataitwa mpaji.

6 Kwani mnyonge atanena unyonge, na
moyo wake utatenda ubaya, kufanya una-
fiki, na kunena juu ya Yahuwa, kufanya



Digitized by Google

Original from
HARVARD UNIVERSITY

tupu roho yake mwenyi njaa, na kinywa
7 chake mwenyi kiu kuikomesha. Na vyo-
mbo vya mnyonge vibaya, afikiri hila awa-
haribu waliotaabika, kwa maneno ya uwo-
ngo, na kumnenea fukara katika hukumu.
8 Naye mkarimu hufikiri makarimu, na kwa
makarimu atasimama.
9 Enyi waanaake waliostarehe, ondokeni,
sikieni sauti yangu binti msiofikiri, pokee-
10 ni masikioni neno langu. Siku kupita
mwaka mtataabika, msiofikiri, kwani miza-
11 bibu itapunguka mavuno hayatakuja. Ogo-
peni mstareheo, tetemekeni msiofikiri, vu-
eni, ondoeni mavazi, jifungeni viunoni.
12 Watalia kwa matiti, kwa mashamba ya
13 kutamanika, kwa mzabibu uzao. Juu ya
inchi ya watu wangu itamea miiba, mbigili,
juu ya nyumba zote za furaha, mji ufurahio.
14 Kwani majumba yameachwa, makutano ya
mjini yatakaa peke yao, mahali pa juu na
ngome kwa mapaango hatta milele, furaha
ya punda milia, malisho ya makundi.
15 Hatta itamiminika juu yetu roho katika
juu, itakuwa jangwa Karmel, na Karmel



Digitized by Google Original from HARVARD UNIVERSITY

16 itathaniwa mwitu. Itakaa katika jangwa
hukumu, na haki itaketi katika Karmel.
17 Itakuwa kazi ya haki amani, na tendo la
18 haki utulivu na tumaini milele. Watakaa
watu wangu katika makao ya amani, na
katika masikani zilizo imara, na mapumu-
ziko ya raha.
19 Itakunya mvua ya mawe kunya katika
mwitu, na mahali pa chini utanenyekea
20 mji. Heri ninyi mpandaye juu ya maji
yote, mpelekao mguu wa ng'ombe na pu-
nda.

XXXIII. Ole wako utekaye, usipotekwa wewe,
udanganyaye usipodanganyika wewe, uta-
kapokwisha kuteka, utatekwa, utakapokwi-
sha kudanganya utadanganyika wewe.
2 Yahuwa uturehemu, tumekungoja wewe,
uwe mkono wao assubuhi, na wokovu wetu
3 wakati wa shidda. Kwa sauti ya paanda
watu wamekimbia, kwa kutukuka wewe wa-
4 metawanyika mateka yenu yatakusanyika,
kama kukusanya wadudu, kama waendavyo
5 nzige kuenda juu yao. Yahuwa ametuku-
ka, ndiye akaaye juu, amejaza Sayuni kwa



Digitized by Google

Original from
HARVARD UNIVERSITY

hukumu na haki. Itakuwa uamini ya waka-
ti wako, nguvu za wokovu, hekima na ma-
arifa. Hofu ya Yahuwa ndiyo kanzi yake.
7 Mashujaa wao watalia 'nje, wajumbe wa
8 amani watalia machungu. Njia zako zi-
meachwa, amekoma aendaye mapito, ame-
vunja agano, ametharau miji, hakukubali
9 mtu. Inchi yazimika, imethoofika, Lebano-
ni imetahayarika, imekatika, Sharon ime-
kuwa kama jangwa, Bashani na Karmel zi-
10 mepukutika. Bassi nitaondoka, amesema
11 Yahuwa, nitatukuka nitajiinua. Mtakuwa
na mimba ya makapi, mtazaa majani,
12 roho yenu kama moto utawala. Watu wa-
takuwa kama kuchoma chokaa, miiba ili-
yokatika ichomwe na moto.
13 Sikieni mlio mbali niliyoyatenda, mkata-
14 mbue mlio karibu nguvu zangu. Walio-
gopa katika Sayuni wenyi thambi, teteme-
ko limewashika wanafiki. Nani kwetu a-
takayekaa katika moto uteketezao? Nani
kwetu atakayekaa katika kuungua milele?
15 Aendaye kwa haki, anenaye adili, asiyepe-
nda choyo cha jeuri, akung'utaye mikono



Digitized by Google
Original from
HARVARD UNIVERSITY

yake katika kushika rushwa, azibaye sikio
lake asisikie ya damu, afumbaye macho
16 yake asione mabaya. Atakaa juu, maboma
ya jabali ngome yake, atapewa chakula
chake, maji yake amini.
17 Macho yako yatamwona mfalme katika
18 uzuri wake, yataona inchi iliyo mbali. Mo-
yo wako utafikiri hofu. Yu wapi mwandi-
shi, yu wapi apimaye, yu wapi ahasibuye
19 minara? Watu wagumu hutawaona, watu
wanenao chini usiwasikie, ulimi wa kishe-
20 nzi pasipo kutambua. Tazame Sayuni mji
wa idi yetu, macho yako yataona Yerusale-
mi kao la raha, hema isiyoondolewa, wala
mismari yake hatta mmoja haingolewi milele
21 wala kamba zake hatta moja hazikatiki.
Kwani huko Yahuwa mtukufu kwetu, maha-
li pa maji, mito mipana ya nafasi, pasipopita
jahazi kwa makasia, wala merikebu kubwa
22 haupiti. Kwani Yahuwa mhukumu wetu,
Yahuwa mfanya sheria wetu, Yahuwa mfal-
me wetu, ndiye atakayetuokoa.
23 Kamba zako zimelegea, hawakuzuia ve-
ma mlingote, hawakutweka bandera, ndipo



Digitized by Google

Original from
HARVARD UNIVERSITY

yakagawanyika mapato ya mateka mengi,
24 waliochechemea wakashika mateka. Wala
hasemi akaaye, nimeugua, watu wakaao humo wameachiliwa maovu.

XXXIV. Karibuni mataifa msikie, sikilizeni watu, inchi isikie na ujao wake, ulimwengu na mazao yake yote.

2 Kwani ghathabu ya Yahuwa juu ya mataifa yote, na hasira juu ya majeshi yao yote. Amewaharibu kabisa, ametoa wachi-
3 njwe, waliouawa wao watatupwa, na katika
mayiti zao uvundo utapanda, na milima ita-
4 yeyuka kwa damu zao. Jeshi lote la mbi-
nguni litalegea, na mbingu zitazingwa kama karatasi, na majeshi yote yao yataanguka, kama mzabibu hupukutika majani, na
5 mtini tini zake. Kwani upanga wangu
utaoshwa katika mbinguni, nao juu ya Edom utashuka, na juu ya watu wa laana langu kwa hukumu.

6 Upanga wa Yahuwa umeshiba kwa damu, umenona kwa shahamu, kwa damu ya kondoo na mbuzi, kwa shahamu ya nso za kondoo waume, kwani thabihu kwa Yahu-



Digitized by Google
Original from
HARVARD UNIVERSITY

wa katika Bozra, kuchinja wengi katika
7 inchi ya Edom. Watashuka nyati pamoja
nao, na ng'ombe na mafahali, inchi itaku-
nywa damu zao, na mavumbi yatatiwa ma-
futa na shahamu.
8 Kwani siku ya kisasi cha Yahuwa, mwa-
9 ka wa kulipia kwa teto la Sayuni. Mito
yake itageuka kuwa lami, na mavumbi
yake kuwa kiberiti, itakuwa inchi yake
10 lami iwakao. Mchana na usiku haizimiki,
milele wapanda moshi wake, kizazi kwa ki-
zazi itaharibika, milele kwa milele haipitiki.
11 Wataimiliki kaati na kipori, na bundi
na kunguru watakaa humo, atanyosha juu
yake kamba ya utupu, na mawe ya ubatili.
12 Mashujaa wake watawaita kwa ufalme, wala
13 hapana, na wote wakuu wake si kitu. Mii-
ba itamea katika majumba yake, kamushi na
yahohe katika maboma yake, itakuwa kao la
14 majoka, ua wa mabundi. Watakuja ziim na
iyim, na sairi ataita kwa mwenziwe, ndiko
huko ametulia ndege ya usiku, akajiona
15 katika raha. Huko atafanya kiota kipozi,
na kuzaa, na kutama, na kukusanya chini



Digitized by Google
Original from
HARVARD UNIVERSITY

ya kivuli chake, huko na wamekusanya na
tai, killa mmoja na mwenzake.
16 Tafuteni katika kitabu cha Yahuwa, mka-
some, mmoja wao hatapunguka, yo yote
hakosi mwenzake, kwani kinwa changu ki-
17 meamuru, na roho yake amewakusanya. A-
mewapigia kura, na mkono wake amewa-
gawanyia kwa kamba, hatta milele wataimi-
liki, kwa kizazi na kizazi watakaa humo.
XXXV. Unyika na pakavu utawafurahia, pata-
cheka pasipo watu, patatoa maua kama wa-
2 ridi. Kumea itamea, itafurahi hatta sha-
ngwi, na kuimba, imepewa utukufu wa Le-
banoni, uzuri wa Karmel na Sharon, zitao-
na utukufu wa Yahuwa, uzuri wa Muungu
wetu.
3 Tieni nguvu kwa mikono thaifu, na ma-
4 gote yatetemekayo mfanye hodari. Mwa-
mbieni moyo uliokasirika, Uwe hodari, usi-
ogope, yuko Muungu wenu kwa kisasi ata-
kuja, malipio ya Muungu, ndiye atakayeku-
ja awaokoe.
5 Ndipo yatafumbuka macho yake kipofu,
6 na masikio ya kiziwi yatazibuka. Ndipo a-



Digitized by Google Original from HARVARD UNIVERSITY

taruka kama kulungu kijigun, utatoa sifa
ulimi wa bubu. Kwani yamekatiwa jangwa-
7 ni maji, na mito pasipo watu. Mahali pa-
kavu patakuwa ziwa, na pa kiu chemchemi
za maji. Wakaapo nyoka, walalapo, nafa-
si ya manyasi na majani.
8 Njia kuu itakuwako na njia, itaitwa njia
ya utakatifu, hatapita juu yake mnajisi, na-
ye kwao; apitaye njiani na mjinga hapotei.
9 Hapana huko simba, wala nyama mkali ha-
tapanda juu yake, wala hataonekana huko,
10 nao waliokombolewa wataiendea. Nao wa-
lionunuliwa na Yahuwa watarudi, watakuja
Sayuni kwa sifa, na furaha ya milele juu
ya vitwa vyao, kicheko na furaha watape-
wa, zitakimbia huzuni na kuugua.
XXXVI. Ikawa mwaka wa arobatashara wa
mfalme Hezekiya, akapanda Sanherib mfal-
lme wa Ashur juu ya miji yote ya Yuda
yenyi boma, akaitwaa.
2 Mfalme wa Ashur akapeleka Rabshake,
katika Lakish kwa Yerusalemi kwa mfalme
Hezekiya, na jeshi kubwa. Akasimama kwa
mfeleji wa birika la juu ulioko katika njia



Digitized by Google
Original from HARVARD UNIVERSITY

3 ya uwanja wa mfinangi. Wakamtokea Eli-
yakim wa Hilkiya, aliye juu ya nyumba,
na Shebna mwandishi, na Yoa wa Asaf
mkumbushi.
4 Rabshake akawaambia, Mwambieni He-
zekiya, Ndilo asemalo mfalme mkuu, mfal-
me wa Ashur, Tumaini gani unalolitumai-
5 nia? Amesema, maneno ya midomo tu, sha-
uri na nguvu kwa vita. Bassi unamwa-
6 mini nani ukiniasi mimi? Bassi angalia
umeuamini 'mwanzi ule uliopondeka, ndio
Misri, mtu akitegemea juu yake utamwi-
ngia mkononi, utamchoma, ndivyo Farao
mfalme wa Misri kwa wote wamwami-
7 nio. Ukiniambia, Yahuwa Muungu wetu
ndiye tumwaminiye, siye aliye Hezekiya
ameondoa mahali pake pa juu, na mathba-
hu zake, akawaambia Yuda na Yerusale-
mi, na mbele ya mathbahu hii msujudie?
8 Bassi umtolee sasa bwana wangu mfal-
me wa Ashur amana, nitakupa frasi elfeen
9 ukiweza kuwatoa wapande juu yao. Ginsi
gani utageuza uso wa jemadari mmoja wa
watumwa wa bwana wangu walio wadogo,



Digitized by Google
Original from
HARVARD UNIVERSITY

ukawaamini Misri kwa gari na kwa frasi?
10 Bassi asipokuwako Yahuwa nimepanda
juu ya mahali hapa nipaharibu? Yahuwa
akaniambia, Panda juu ya inchi hii uihari-
bu.
11 Wakamwambia Rabshake Eliyakim, na
Shebna, na Yoa, Useme sasa na watu-
mwa wako Kishami, kwani twakisikia, wa-
la usiseme nasi Kiyuda, masikioni mwa
watu walioko ukutani.
12 Akamwambia Rabshake, Bwana wangu
amenipeleka kwa bwana wako na kwa we-
we niseme maneno haya? Si kwa watu wa-
lioko ukutani, wale mavi yao, wakanywe
mkojo wao pamoja nanyi?
13 Rabshake akasimama akalia Kiyuda kwa
sauti kuu, akanena, akasema, Sikieni ne-
no lake mfalme mkuu, mfalme wa Ashur.
14 Ndilo asemalo mfalme, asiwadanganye He-
15 zekiya, kwani hataweza kuwaokoa. Wala
Hezekiya asiwaaminishe kwa Yahuwa, aki-
sema, yakini atatuokoa Yahuwa, mji huu
usitolewe mkononi mwake mfalme wa A-
16 shur. Msimsikilizie Hezekiya, kwani ndilo



Digitized by Google
Original from HARVARD UNIVERSITY

asemalo mfalme wa Ashur, Fanyeni nami
mbaraka mkanitokee, mkale killa mtu
mzabibu wake na killa mtu mtini wake,
mkanywe killa mtu maji ya birika yake,
17 hatta nitakapokuja niwachukue hatta inchi
kama inchi yenu, inchi ya nafaka na mvi-
nyo, inchi ya mikate na mizabibu.
18 Msimsikilizie Hezekiya akisema, Yahu-
wa atatuokoa. Muungu yupi wa mataifa
aliyeiokoa kabisa inchi yake katika mkono
19 wa mfalme wa Ashur? Wako wapi miungu
wa Hamath na Arpad? Wapi miungu wa
Sefarvaim? Wameokoa Samaria mkononi
20 mwangu? Yupi wa miungu wote wa inchi
hizi aliyeiokoa inchi yake mkononi mwangu,
Yahuwa aiokoe Yerusalemi mkononi mwa-
ngu?
21 Watu wakanyamaza, wala hawakumjibu
neno, kwa amri yake mfalme, akinena, msi-
mjibu.
22 Wakaja Eliyakim wa Hilkiya, aliye juu
ya nyumba, na Shebna mwandishi, na Yoa
wa Asaf mkumbushi kwa Hezekiya, mavazi
yakiraruliwa, wakamhubiria maneno ya



Digitized by Google
Original from
HARVARD UNIVERSITY

Rabshake.
XXXVII. Ikawa akisikia mfalme Hezekiya a-
kayararua mavazi yake, akavaa sako, aka-
ingia nyumbani mwa Yahuwa.
2 Akawapeleka Eliyakim aliye juu ya nyu-
mba, na Shebna mwandishi, na wakohani
walio wazee, wamevaa sako, kwa Isaya na-
bii mwanawe Amoz.
3 Wakamwambia, Ndilo asemalo Hezeki-
ya, Siku ya shidda, na mashutumo, na una-
jisi, siku hii, kwani watoto wamekuja hatta
4 kuzaliwa wala si nguvu za kuzaa. Kama
amesikia Yahuwa Muungu wako maneno
yote ya Rabshake, aliyempeleka mfalme wa
Ashur bwana wake amshutumu Muungu
aliye hayi, ayarudi maneno aliyoyasikia Ya-
huwa Muungu wako; ukafanye kuwaombea
waliooneka wamesalia.
5 Wakaja watumwa wa mfalme Hezekiya
6 kwa Isaya. Akawaambia Isaya, Mwa-
mbieni haya bwana wenu. Ndilo asemalo
Yahuwa, Usiogope kwa maneno uliyoyasi-
kia, mashutumu walivyonishutumu watu
7 wake mfalme wa Ashur. Mimi nitamtolea



Digitized by Google
Original from
HARVARD UNIVERSITY

pepo, atasikia habari, atarudi katika inchi
yake, nitamfanya aanguke kwa upanga ka-
tika inchi yake.
8 Akarudi Rabshake akamwona mfalme
wa Ashur akipigana na Libna, kwani ame-
9 sikia kwamba ametoka katika Lakish. A-
kapata habari ya Tirhaka mfalme wa Kushi,
kwamba ametoka apigane nawe. Akisikia
akampelekea wajumbe Hezekiya akisema,
10 Hivyo mwambieni Hezekiya mfalme wa
Yuda, mkisema, Asikudanganye Muungu
unayemwamini akisema, Yerusalemi hai-
tolewi mkononi mwa mfalme wa Ashur.
11 Angalia, umesikia wafalme wa Ashur wa-
livyozifanyia inchi zote, wakiziharibu, nawe
12 utaokoka? Wamewaokoa miungu wa ma-
taifa waliowaharibu baba zangu? Gozan,
na Haran, na Rezef, na waana wa Eden wa-
13 lioko katika Thelassar? Yuko wapi mfalme
wa Hamath, na mfalme wa Arpad, na
mfalme wa mji wa Sefarvaim, Hena, na
Hiva?
14 Hezekiya akazitwaa nyaraka kwa mkono
wa mjumbe, akazisoma, akapanda nyumba-



Digitized by Google
Original from
HARVARD UNIVERSITY

ni kwa Yahuwa, Hezekiya akazifunua mbe-
le ya Yahuwa.
15 Akaomba Hezekiya mbele ya Yahuwa,
16 akasema, Ee Yahuwa wa majeshi, Muungu
wa Israeli ukaaye katika makerubi, ndiwe
Muungu, ndiwe peke yako wa falme zote
za inchi, ndiwe uliyezifanya mbingu na in-
17 chi. Uiname, Ee Yahuwa, sikio lako ukasi-
kie, ufumbue, Ee Yahuwa, macho yako u-
kaone, uyasikie maneno yote ya Sanherib,
aliyepeleka amshutumu Muungu aliye hayi.
18 Kweli, Yahuwa, wameharibu wafalme
19 wa Ashur mataifa yote na inchi zao. Wa-
meitupa miungu yao katika moto, kwani
siyo miungu, illa kazi za mikono ya watu,
mti na mawe, wakaziharibu.
20 Hatta sasa, Ee Yahuwa Muungu wetu,
utuokoe katika mkono wake, falme zote za
inchi zijue kwamba ndiwe Yahuwa, ndiwe
peke yako.
21 Akapeleka Isaya wa Amoz kwa Hezeki-
ya akisema, Ndilo anenalo Yahuwa Muu-
ngu wa Israeli, Kama ulivyoniomba juu
22 ya Sanherib mfalme wa Ashur, ndilo neno



Digitized by Google

Original from
HARVARD UNIVERSITY

alilolinena Yahuwa juu yake.
Amekutharau, amekufionya bikira binti
Sayuni, amekutikisia kitwa binti Yerusa-
23 lemi. Nani uliyemshutumu, uliyemtaya,
juu ya nani umepaliza sauti, ukainua juu
macho yako? Juu yake mtakatifu wa Is-
raeli.
24 Kwa mkono wa watumwa wako umem-
shutumu Bwana, ukasema, Kwa wingi wa
magari yangu nimepanda juu ya milima,
pande za Lebanoni, nikaukata urefu wa
mierezi yake, miteule ya miberoshi yake,
nikaingia katika kituo cha mwisho wake,
25 mwitu wa koonde lake. Nimechimba, ni-
kanywa maji, nimekausha kwa nyayo za
miguu yangu mito yote yao iliyo nalo bo-
ma.
26 Hukusikia zamani nililolifanya, tangu
hapo nikaliumba? Sasa nimelileta, uwe
wewe kuharibu, chungu za maanguko miji
27 yenyi boma, wakaamo wakapungua miko-
no, wakapondeka, wakatahayarika, wame-
kuwa majani ya koondeni, miche imeayo,
majani ya darini, yaliyopigwa na pepo



Digitized by Google Original from HARVARD UNIVERSITY

mbele ya mabua.
28 Nami nimekujua kukaa kwako, na ku-
toka kwako, na kuingia kwako, na kuni-
29 ghathabikia kwako. Kwani kunighatha-
bikia kwako, na uthia wako umenipandia
masikioni, nitakutia kulabu yangu katika
pua, na hatamu yangu katika midomo, ni-
kurudishe kwa njia uliyoijia.
30 Ndiyo ishara yako, Ule mwaka huu ma-
oteo, na mwaka wa pili utakaoota, na mwa-
ka wa tatu, mpande, mvune, pandeni mi-
31 zabibu mkale mazao yao. Nao waliosalia
waliookoka wa nyumba ya Yuda watatoa
32 mizizi chini, watazaa matunda juu. Kwani
katika Yerusalemi yatatoka masalia, na
katika mlima Sayuni maokoka. Uwivu
wake Yahuwa utayafanya haya.
33 Navyo alivyomwambia Yahuwa mfalme
wa Ashur, hataingia katika mji huu, wala
hatatupa humu mshale, wala hataufikia
na ngao, wala hatafanya kilima juu yake.
34 Kwa njia aliyoijia atarudi, wala katika mji
35 huu hataingia, amenena Yahuwa. Nitau-
linda mji huu, niuhifathi kwa ajili yangu,



Digitized by Google
Original from
HARVARD UNIVERSITY

na kwa ajili yake Daud mtumwa wangu.
36 Akatoka malaika ya Yahuwa akapiga
katika kituo cha Ashur mia na themanini
na tanu elfu. Wakaamka assubuhi, nao ha-
wa wote mizoga ya wafu. Akatoka, akae-
nda, akarudi Sanherib mfalme wa Ashur,
akakaa Ninawe.
37 Ikawa akisujudia katika nyumba ya Nis-
rok muungu wake, Adramelek na Shareser
waanawe wakampiga kwa upanga. Waka-
okoka katika inchi ya Ararati, akamiliki
Esarhadon mwanawe mahali pake.
XXXVIII. Siku zile akaugua Hezekiya hatta
kufa. Akamjia Isaya wa Amoz nabii,
akamwambia, Ndilo asemalo Yahuwa,
uamuru nyumba yako, kwani utakufa, wa-
la hutaishi.
2 Akageuka Hezekiya uso wake kwa ukuta
3 akamwomba Yahuwa, akanena, Nakusihi
Yahuwa, ukumbuke, kama nilivyokwenda
mbele yako kwa kweli na kwa moyo kami-
li, nikayatenda yaliyo mema machoni pako.
Akalia Hezekiya malio mengi.
4 Neno la Yahuwa likamjia Isaya kunena,



Digitized by Google Original from HARVARD UNIVERSITY

5 Rudi, ukamwambie Hezekiya, Ndilo asema-
lo Yahuwa Muungu wa Daud baba yako,
Nimesikia kuomba kwako, nimeona ma-
chozi yako, nami nitazizidisha siku zako
6 miaka hamstashara, na katika mkono wa-
ke mfalme wa Ashur nitakuokoa wewe
7 na mji huu, nitauhifathi mji huu. Ndiyo
ishara yako kwa Yahuwa, kwamba Yahuwa
8 atafanya alilolinena, Nitaleta tena kivuli cha
daraja zilizoshuka katika daraja ya Ahaz,
daraja kumi nyuma. Jua likarudi daraja
kumi, lilizoshukia daraja.

9 Andiko la Hezekiya mfalme wa Yuda,
alipougua, akapona katika ugonjwa wake.

10 Mimi nalisema katika kukatika siku za-
ngu, nitakwenda hatta milango ya kaburi,
11 nimeondolewa masalia ya miaka yangu. Na-
lisema sitamwona Yah, Yah katika inchi ya
wahayi, sitamwona mtu tena pamoja na wa-
12 kaao ulimwenguni. Umri wangu umetoka,
umehama kwangu kama hema ya mchunga-
ji, nimekata kama afumaye maisha yangu,
atanikatia mbali nyuzi kwa ugonjwa, tangu
13 mchana hatta usiku utanikomesha. Nali-



Digitized by Google

Original from
HARVARD UNIVERSITY

hasibu hatta assubuhi, kama simba atani-
vunja mifupa yangu yote, tangu mchana hat-
14 ta usiku wanikomesha. Kama sus na mba-
yuwayu nalipiga kelele, nalilia kama hua.
Macho yangu yamelegea juu, Yahuwa, nime-
15 tiwa nguvu, uwe thamini yangu. Nisemeje,
amesema nami naye ametenda, nitakwenda
miaka yote yangu katika uchungu wa roho
16 yangu. Bwana kwa hayo huishi, na kwa ha-
yo yote maisha ya roho yangu, utaniponya,
17 utanihuisha. Nami kwa amani kwangu u-
chungu, nawe umenipendelea roho yangu
katika shimo la kupotea, kwani umetupa
18 nyuma yako thambi zangu zote. Kwani
silo kaburi litakalokusifu, mauti haikutuku-
zi wala hawatatumaini kwa kweli yako wa-
19 shukao shimoni. Mhayi, mhayi atakayekuu-
ngama, kama mimi leo, baba kwa watoto
20 atajulisha amini yako. Yahuwa aniokoaye,
na kwa vinanda nyimbo tutaziimba siku zo-
te za maisha yetu nyumbani mwa Yahuwa.
21 Kwani Isaya amesema, Twaeni mkate wa
22 tini mkauweke juu ya jipu, atapona. He-
zekiya tena amesema, Ishara gani kama



Digitized by Google Original from HARVARD UNIVERSITY

nitapanda nyumbani kwa Yahuwa.
XXXIX. Wakati ule akapeleka Merodak-Bala-
dan wa Baladan, mfalme wa Babel nyaraka
na zawadi kwa Hezekiya, kwani amesikia
kama Hezekiya ameugua akapona.
2 Akawasikiliza Hezekiya, akawaonyesha
killa nyumba yake ya kupendeza, fetha, na
thahabu, na manukato, na marhamu mazuri,
na killa nyumba ya vyombo vyake, na killa
iliyoonwa katika hazina zake. Wala hapa-
na kitu asichowaonyesha Hezekiya katika
nyumba yake na katika nguvu zake zote.
3 Akaja Isaya nabii kwa mfalme Hezekiya
akamwambia, Wamesemaje watu hawa,
wametoka wapi kuja kwako?
Akamwambia Hezekiya, Katika inchi
iliyoko mbali wamekuja, katika Babel.
4 Akasema, Wameona nini nyumbani
mwako? Akasema Hezekiya, Killa kili-
chomo nyumbani mwangu wamekiona, ha-
pana kitu nisichowaonyesha katika hazina
zangu.
5 Isaya akamwambia Hezekiya, Sikia ne-
6 no lake Yahuwa wa majeshi, Angalia, siku



Digitized by Google
Original from
HARVARD UNIVERSITY

zinakuja, kitakapochukuliwa killa kilicho-
mo nyumbani mwako, navyo walivyoweka
baba zako hatta leo, hatta Babel, hakitasa-
7 lia kitu, amenena Yahuwa. Na katika
waanawo, watakaozaliwa kwako watawa-
twaa, watakuwa matowashi katika nyumba
yake mfalme wa Babel.
8 Hezekiya akamwambia Isaya, Neno la
Muungu jema ulilolinena. Akasema, kwa-
ni itakuwa amani na kweli siku zangu.
XL. Tulizeni, Tulizeni watu wangu, asema
2 Muungu wenu. Semeni na moyo na Yeru-
salemi, mkamwitie ya kwamba vita yake
imekwisha, kwani amekubaliwa kwa uovu
wake, kwani amepokea kwa mkono wa
Yahuwa maradufu kwa thambi zake zote.
3 Sauti yake aliaye unyikani, Fanyizeni
njia ya Yahuwa, nyosheni katika jangwa
4 njia kuu kwa Muungu wetu. Killa boonde
litainuka, na killa mlima na kilima kitashu-
shwa, kipotoe kitanyoshwa, na kuparuza ku-
5 wa sawa. Utafunuka utukufu wa Yahu-
wa, wataona wenyi mwili wote pamoja,
kwani kinwa cha Yahuwa kimenena.



Digitized by Google
Original from
HARVARD UNIVERSITY

6 Sauti kunena, Ulie. Akasema, Nilie ni-
ni? Mwili wote majani, na wema wake
7 kama ua la mashamba. Yamekauka ma-
jani, umeanguka ua, kwani roho ya Muu-
ngu imevuma juu yake, yakini watu ni ma-
8 jani. Yakauka majani, waanguka ua, na
neno la Muungu wetu litasimama milele.
9 Juu ya mlima mrefu upande ubashiriye,
Sayuni. Paliza sauti yako kwa nguvu
ubashiriye, Yerusalemi. Upalize usiogope.
Iambie miji ya Yuda, Yuko Muungu wenu.
10 Yuko Bwana Yahuwa na uwezo anakuja,
na mkono wake wammilikia, iko thawabu
11 yake naye, na kazi yake mbele yake. A-
talisha kundi lake kama mchunga, ataku-
sanya waana kondoo mkononi, atachukua
kifuani, atawaleta polepole walio na mimba.
12 Nani aliyepima maji katika mkononi
mwake, akazigawa mbingu kwa shibiri,
akaweka mavumbi ya inchi katika cheo,
akafanya uthani wa milima kwa vitanga
13 na vilima kwa mizani? Nani aliyemgawia
Roho ya Muungu, ao msiri wake aliyemfu-
14 ndisha? Alifanya shauri na nani, nani ali-



Digitized by Google

Original from
HARVARD UNIVERSITY

yemwelimisha, akamwonyesha katika njia
ya hukumu, akamwarifu maarifa, akamju-
15 lisha njia ya akili? Yako mataifa kama
tone katika ndoo, wakathaniwa kama ma-
vumbi membamba ya mizanini, navyo visi-
16 wa kama vidogo avichukua. Lebanoni ha-
itoshi kwa kuni, wala nyama zake kwa
17 kafara. Mataifa yote mbele yake si kitu,
yamethaniwa kwake hafifu kuliko si kitu
na ubatili.
18 Mtamfafanisha Muungu na nani? Kwa
19 mfano gani mtamfanya sawa? Fundi hu-
yeyusha sanamu, mfua thahabu huifunikiza
kwa thahabu, hufanya kwa kalibu mikufu
20 ya fetha. Aliye maskini kuliko kuwa na
sadaka huchagua mti usiooza, hutafuta
mstadi afanye sanamu, isiyokwenda.
21 Hamkujua, hamkusikia, hamkuambiwa
tangu mwanzo, hamkufahamu tangu ku-
22 wekwa inchi? Ndiye akaaye juu ya kivi-
mba cha inchi, na wakaao humo kama panzi,
atandaye mbingu kama pazia, azinyoshaye
23 kama hema ya kukalia. Awafanya wakuu
wa inchi wasiwe neno, waamuao katika in-



Digitized by Google Original from HARVARD UNIVERSITY

24 chi kama ubatili. Hatta hawatapandwa,
wala kama mbegu hazitatiwa, hatta shina
lao halitatoa mizizi katika inchi, naye ata-
vuma juu yao, nao watakauka, na tufano li-
tawachukua kama takataka.
25 Mtanifafanisha na nani, nitalingana na
26 nani? Amesema Mtakatifu. Inueni macho
yenu juu, mkamwangalie aliyeviumba, apa-
ngaye jeshi lao kwa hesabu, aviita vyote
kwa majina kwa ukuu wa uwezo wake,
kwani hodari nguvu zake, hapana kipungu-
27 kacho. Unenaje, Yakobo, usemaje, Israeli,
njia yangu imefichwa kwa Yahuwa, na hu-
kumu yangu imeachwa na Muungu wangu.
28 Hamkujua ao hamkuambiwa, Muungu
wa milele Yahuwa muumba mwisho wa in-
chi, hachoki, wala hazimii, hazitafutikani
29 akili zake. Ampaye aliyechoka nguvu, na-
30 ye asiyeweza, humzidisha uwezo. Vijana
watachoka, watazimia, na wateule kuangu-
31 ka wataanguka. Wamngojao Yahuwa wa-
tabadili nguvu, watapanda kwa mabawa
kama ndege hodari, watapiga mbio hawa-
tachoka, watakwenda wala hawatalegea.



Digitized by Google

Original from
HARVARD UNIVERSITY

XLI. Mninyamalie visiwa, na mataifa wabadili nguvu, wakaribie, tena wakanene, tukaribu pamoja kwa hukumu.

2 Nani aliyeamsha katika mashariki haki,
akamwita mguuni pake, akampa mataifa
mbele yake, akamtawaza wafalme? Akawatoa
kama mavumbi kwa upanga wake,
kama makapi yaliyopeperushwa kwa upindi
3 wake. Akawafuata akapita salama, kwa
4 njia isiyopitika kwa miguu yake. Nani aliyetenda
aliyefanya, aitaye vizazi tangu asili?
Mimi Yahuwa wa kwanza, na wa mwisho,
ndimi mimi.

5 Vikaona visiwa vikaogopa, miisho ya i-
6 nchi ikashangaa, wakakaribu wakaja. Mtu
akamsayidia mwenzake, akamwambia ndu-
7 gu yake, Uwe hodari. Fundi akamtia moyo
mfua thahabu, afanyaye sawa kwa nyundo
kupiga fuawo, akinena, Ndiyo njema
kwa kuunga, akaikaza kwa misınari isitikisike.

8 Nawe Israeli mtumwa wangu, Yakobo
niliyekuchagua, mzao wa Ibrahimu rafiki
9 yangu, niliyekutwaa katika miisho ya inchi,



Digitized by Google Original from HARVARD UNIVERSITY

na katika wa kwanza wake niliyekuita, ni-
kakwambia, Mtumwa wangu wewe, nime-
10 kuchagua, wala sikukukataa. Usiogope
kwani mimi pamoja nawe, usilegee kwani
mimi Muungu wako, nimekutia nguvu, te-
na nikakusayidia, tena nikakuchukua kati-
ka mkono wa haki yangu.
11 Watatahayarika, wataaibika wote walio-
waka juu yako, watakuwa kama si kitu,
12 watapotea watu wa ugomvi wako. Utawa-
tafuta, hutawaona, watu wa teto lako, wa-
takuwa kama si kitu, nao kama kukoma
13 watu wa pigano lako. Kwani mimi Yahu-
wa Muungu wako nikushikaye mkono wa
kuume, nikikuambia, Usiogope, mimi nime-
14 kusikia. Usiogope mdudu Yakobo, ucha-
che wa Israeli, mimi nimekusayidia, amese-
ma Yahuwa, na mkombozi wako Mtakatifu
wa Israeli.
15 Nimekufanya wewe nauraji kali mpya
yenyi meno, utaponda milima utaisaga, na
16 vilima utafanya kama makapi. Utapepea
upepo utavichukua, tufano itawatawanya,
nawe utamfurahia Yahuwa, kwa Mtakatifu



Digitized by Google

Original from HARVARD UNIVERSITY

wa Israeli utajisifu.
17 Wateswa na watamanio wakitafuta maji
wala hapana, ulimi wao ukiharibika kwa
kiu, mimi Yahuwa nitawasikia, Muungu wa
18 Israeli sitawaacha. Nitafunua mito katika
mahali pa juu, na kati ya boonde chemche-
mi, nitafanya jangwa ziwa la maji, na inchi
19 ya kiu pakutokea maji. Nitaweka katika
jangwa mwerezi, mshita, msheres, na mti
wa zeituni, nitaweka katika unyika mbero-
20 shi, mtidhari na msherbini pamoja. Wao-
ne wajue, wakifikiri watambue pamoja,
kwani mkono wa Yahuwa umefanya hilo,
na Mtakatifu wa Israeli ameumba lile.
21 Leteni teto lenu, amesema Yahuwa, yaje
yaliyo hodari kwenu, amesema Mfalme wa
22 Yakobo. Waje, watupe habari za mambo
yatakayokuwa, wayaonyeshe ya zamani, tu-
yatie moyoni, tujue mwisho wao, ao yata-
23 kayokuwa watusikize. Hubirini yatakayo-
kuwa halafu, tujue ya kwamba miungu ni-
nyi. Hatta mtende mema, mtende maba-
24 ya, tuangalie tuone pamoja. Nanyi ninyi
katika si kitu, na kazi yenu katika si kitu,



Digitized by Google

Original from
HARVARD UNIVERSITY

chukizo kuwakubali.
25 Nimeondokesha katika kaskazini, ataku-
ja katika kutoka jua, ataita kwa jina langu,
atakuja juu ya wakuu kama juu ya udongo,
na kama mfinangi akanyagaye matope
yake.
26 Nani aliyeonyesha tangu mwanzo, tupa-
te kujua, na yaliyo mbele tuseme, Haki?
Illakini hakuna aonyeshaye, wala tena asi-
kizaye, wala tena asikiaye maneno yenu.
27 Wa kwanza kwa Sayuni, Wako, wako,
28 katika Yerusalemi nitatoa mbashiri. Ni-
kaona, wala hakuna, hatta kwao, hakuna
29 mshauri nikiwauliza ajibuye neno. Nao
wote ubatili, kazi yao si kitu, upepo na
utupu sanamu zao.
XLII. Yuko mtumwa wangu, nimchukuaye,
mteule wangu, amtakaye roho yangu, ni-
meweka roho yangu juu yake, atatoa huku-
2 mu kwa mataifa. Hatalia wala hatapaliza
wala hatasikiza sauti yake katika njia.
3 Mwanzi uliopondeka hatavunja, wala kitani
kitoacho moshi hatakizimia, ataleta huku-
4 mu kwa kweli. Hatazimia wala hatalegea,



Digitized by Google
Original from HARVARD UNIVERSITY

hatta atakapoweka katika inchi hukumu,
na kwa sheria yake visiwa vitangoja.
5 Ndilo asemalo Muungu Yahuwa muu-
mba mbingu, azitandaye, anyoshaye inchi
na mazao yake, awapaye watu juu yake
6 pumuzi, nao roho waendao humu. Mimi
Yahuwa nimekuita kwa haki, nitakushika
mkono, nitakulinda, nitakuweka kwa agano
7 na watu, kwa nuru ya mataifa. Kufunua
macho mapofu, kuleta katika mafungo
aliyefungwa, katika nyumba ya kufungwa
wakaao gizani.
8 Mimi Yahuwa, ndilo jina langu, wala
utukufu wangu sitampa mwingine, wala
9 sifa zangu kwa sanamu. Yaliyo ya kwanza
ndiyo yamekuja, na mapya ndimi niyao-
nyeshaye, mbele ya kutokea nitawapa ninyi
habari.
10 Mwimbieni Yahuwa uimbo mpya, sifa za-
ke hatta mwisho wa inchi, washukao baha-
rini na ujao wake, visiwa nao wakaao hu-
mo.
11 Watapaliza unyika na miji yake, vijiji
wakaamo Kedari, wasifu wakaao miambani,



Digitized by Google
Original from
HARVARD UNIVERSITY

12 katika kilele cha milima. Wampe Yahuwa
utukufu na sifa zake wazihubiri kwa visiwa.
13 Yahuwa kama mshujaa atatoka, kama mtu
wa vita atafanya uwivu, atalia, atapiga ke-
lele, atawashinda adui zake.
14 Nalinyamaza tangu zamani, nalitulia,
nalijizuia, kama azaaye nitatweta, nitasha-
15 ngaza nitameza pamoja. Nitaharibu mili-
ma na vilima, na yote yameayo kwao nita-
yakausha, nitafanya mito visiwa, nitanyau-
16 sha maziwa. Nitawaleta vipofu kwa njia
wasiyoijua, nitawachukua kwa mapito wa-
siyoyajua, nitafanya giza mbele yao kuwa
nuru, na mapotoe kunyoka. Haya nitawa-
tendea, wala sitawaacha.
17 Wamerudi nyuma, wameaibika kwa aibu
watumainio kwa sanamu, waambiao sanamu,
18 Ndinyi miungu yetu. Enyi viziwi sikieni,
19 na vipofu tazameni mwone. Nani kipofu
illa mtumwa wangu, na kiziwi kama tume
nimpelekaye? Nani kipofu kama mkamili-
20 fu, na kipofu kama mtumwa wa Yahuwa?
Kuona mambo mengi hatazami, kuzibua
21 masikio hasikii. Yahuwa akapendezwa na



Digitized by Google Original from HARVARD UNIVERSITY

haki yake, ataitukuza torati, ataifanya tu-
kufu.
22 Nao watu hawa wametekwa, wameibiwa,
wamenaswa na mashimo wote, na katika
nyumba ya kufungwa wamefichwa, waliku-
wa katika kunyang'anwya wala hapana ao-
koaye, kutekwa, wala hapana asemaye, Ru-
23 disha. Nani kwenu apokeaye haya masikio-
ni, atajitia, atasikia kwa wakati baadaye?
24 Nani aliyetoa Yakobo kwa mateka, na Is-
raeli kwa wanyang'anyi? Siye Yahuwa, tu-
liyemkosa, wakaona taabu kwenda katika
njia zake, wala hawakusikia sheria yake.
25 Akamwaga juu yao ukali wa hasira yake,
na nguvu za vita, akawasha moto kumzu-
nguka, wala hakutambua, ukamchoma wala
hakutia moyo.
XLIII. Bassi sasa ndilo asemalo Yahuwa aliye-
kuumba, Yakobo, na mfanya wewe, Israeli,
Usiogope kwani nimekukomboa, nimekuita
2 kwa jina lako, wewe wangu. Ukipita kwa
maji, mimi pamoja nawe, na kwa mito hai-
takugharikisha, ukienda kwa moto, hauta-
kuunguza, wala ulimi wa moto hautakucho-



Digitized by Google
Original from
HARVARD UNIVERSITY

3 ma. Kwani ndimi Yahuwa Muungu wako,
Mtakatifu wa Israeli Mwokozi wako, nime-
toa Misri kwa upatanisho wako, Kushi na
4 Seba kwa ajili yako. Kwa sababu ulikuwa
na thamani machoni pangu, umetukuka ni-
kakupenda, nikatoa mtu kwa ajili yako na
5 watu kwa ajili ya nafusi yako. Usiogope
kwani mimi nawe, katika mashariki nitale-
ta uzao wako na katika magaribi nitakuku-
6 sanya. Nitaambia kaskazini, utoe, na ku-
sini, usizuie, lete waana wangu katika mba-
li, na binti zangu katika mwisho wa inchi.
7 Killa aliyeitwa kwa jina langu, na kwa utu-
kufu wangu nime'mumba, nimemunda ni-
kamfanya.
8 Leteni 'nje watu vipofu wenyi macho, vi-
9 ziwi na masikio kwao. Mataifa yote yaku-
sanyike, wakutane watu, nani wao ataonye-
sha haya, na ya zamani atatusikiza? Watoe
mashahidi yao, wawe na haki, wakasikie,
10 wakanene, Kweli. Ndinyi mashahidi wa-
ngu, amesema Yahuwa, na mtumwa wangu
niliyemchagua, mjue mkiniamini, mkafaha-
mu ya kwamba ndimi, mbele yangu haku-



Digitized by Google
Original from HARVARD UNIVERSITY

pata kuwa Muungu, wala baada yangu ha-
11 takuwa. Mimi ndimi Yahuwa wala hapana
12 pasipo mimi Mwokozi. Mimi nimeonya,
nikaokoa, nikasikiza, wala hakuna kwenu
mgineo, nanyi mashahidi wangu, amesema
13 Yahuwa, nami Muungu. Hatta mbele ya
mchana nipo, wala hakuna aondoaye kati-
ka mkono wangu, nitatenda, nani atakayei-
geuza.

14 Ndilo asemalo Yahuwa mwokozi wenu,
Mtakatifu wa Israeli, Kwa ajili yenu nime-
peleka hatta Babel, nitawakimbiza wote pia,
na Wakasidi, katika merikebu kilio chao.
15 Mimi Yahuwa, mtakatifu wenu aumbaye
16 Israeli, mfalme wenu. Ndilo asemalo Ya-
huwa, awekaye baharini njia, na katika
17 maji ya nguvu kivuko. Aletaye gari na
frasi, uwezo na nguvu, watalazwa pamoja,
hawataondoka, wamezimika, kama kitani
wamezimishwa.

18 Hamkumbuki ya zamani, na ya kale ha-
19 mfikiri. Nipo mimi kufanya mapya, sasa
itamea, hamtambui? Nitaweka tena kati-
ka unyika njia, pasipo watu mito ya maji.



Digitized by Google
Original from
HARVARD UNIVERSITY

20 Nyama ya mwituni atanitukuza, majoka na
binti za kulia, kwani nimeweka katika
unyika maji, mito pasipo watu, kuwanywe-
sha watu wangu, wateule wangu.
21 Watu hawa nimejifanyia, wataonyesha
22 sifa zangu. Illa hamkuniitia Yakobo, u-
23 menichokea Israeli. Hamkuniletea kundi
la makafara yako, wala kwa thabihu zako
hukuniheshimia, sikukutumikisha kwa sa-
daka za unga, wala sikukuchosha kwa uvu-
24 mba. Hamkuninunulia kwa fetha nukato,
wala kwa shahamu ya thabihu zako hukuni-
shibisha. Lakini mmenichosha kwa thambi
zenu, mmenichosha kwa maovu yenu.
25 Mimi ndimi afutaye matelezo yako mbe-
le yangu, wala thambi zenu sitazikumbuka.
26 Unikumbushe tufanye huja pamoja, useme
27 upate kuwa na haki. Baba wako wa kwa-
nza alitenda thambi, na wakalimani wako
28 wamekosa kwangu. Nikawatia unajisi wa-
kuu wa utakatifu, nitaweka katika laana
Yakobo, na Israeli katika mashutumo.
XLIV. Bassi sasa sikie Yakobo mtumwa wa-
2 ngu, na Israeli niliyemchagua. Ndilo ase-



Digitized by Google Original from HARVARD UNIVERSITY

malo Yahuwa aliyekubuluku, aliyekufanya
tangu tumboni, atakayekusayidia, Usiogo-
pe, mtumwa wangu Yakobo, na Yeshurun
3 niliyemchagua, kwani nitamimina maji juu
yake mwenyi kiu, na mito juu ya pakavu,
nitamimina roho yangu juu ya wazao wako,
na mbaraka wangu juu ya watokao kwako.
4 Watamea kati ya majani kama miti kwa
5 vijito vya maji. Huyu atasema, Mimi wa
Yahuwa, na huyu ataita kwa jina la Yakobo,
na huyu ataandika kwa mkono wake kwa
Yahuwa, na kwa jina la Israeli atajitaja.
6 Hivi asemavyo Yahuwa mfalme wa Isra-
eli, na mkombozi wake, Yahuwa wa maje-
shi, Mimi wa kwanza na mimi wa mwisho,
7 pasipo mimi hapana Muungu. Nani kama
mimi ataita, atahubiri haya, atakayeniamria,
tangu nilipoweka watu zamani? Na ma-
mbo yajayo, na yatakayokuja awahubirie.
8 Msiogope msione hofu, si tangu hapo ni-
mekusikiza, nikanena, nanyi mashahidi
wangu, yuko Muungu illa mimi, hakuna
mwamba, siujui.
9 Wafanyao sanamu wote ubatili, wala ya-



Digitized by Google
Original from
HARVARD UNIVERSITY

liyotamanika kwa hayafai, nao wenyewe
mashahidi, hawataona, wala hawatajua, kwa
10 maana waaibike. Nani aliyefanya Muungu,
11 akayeyusha sanamu, haifai neno? Wako
wenzake wote wataona haya, na mafundi
ndio watu, watakusanyika wote, watasimama,
wataogopa, watatahayarika pamoja.

12 Mfua chuma kwa makoleo hutenda kwa
makaa, huitengeneza kwa nyundo, huitendea
kwa nguvu za mkono wake, akiona
njaa, nguvu zake zimepunguka, asipokunywa
maji hulegea.

13 Sermala hunyosha cheo, huandika kwa
uzi, hufanyiza kwa maranda, huandika kwa
kompasi, hufanya kwa mfano wa mtu, kwa
uzuri wa mtu ikae nyumbani.

14 Hujikatia mierezi, hutwaa mtirza na mweloni,
hujifanyia hodari katika miti ya mwituni,
hupanda mworeni, mvua zaulisha.
15 Utakuwa kwa mtu kwa kuni, atatwaa katika
huo akote moto, atawasha apike mkate,
tena ataufanya Muungu, ausujudia aufanya
16 sanamu auangukia. Kipande chake huchoma
motoni, kwa kipande chake hula nyama,



Digitized by Google
Original from
HARVARD UNIVERSITY

huoka maoko hushiba, hukota moto, huse-
ma, Haha, nimepata hari, nimeona moto.
17 Uliosalia hufanya muungu, sanamu yake,
huanguka, husujudia, huinama mbele yake,
hunena, Uniokoe, kwani ndiwe muungu wa-
18 ngu. Hawakujua, wala hawakufahamu,
kwani amefumba macho yao wasione, wa-
19 sitambue moyoni. Wala hajitii moyoni, wa-
la maarifa, wala akili kunena, Nussu yake
nimeteketeza motoni, na juu ya makaa ya-
ke nimepika chakula, nimeoka nyama ni-
kashiba, uliosalia nifanye chukizo, niiname
20 kwa tawi la mti. Alaye majifu, moyo ulio-
potea umempoteza, wala hataokoa nafusi
yake, wala hasemi, Sio uwongo mkononi
mwangu.

21 Kumbuke haya, Yakobo na Israeli, kwani
mtumwa wangu ndiwe, nimekufanya, mtu-
mwa kwangu ndiwe, Israeli, usinisahau.
22 Nimefuta kama wingu matelezo yako na
kama wingu zito thambi zako, unirudie
23 kwani nimekukomboa. Imbeni mbingu,
kwani ametenda Yahuwa, pigeni kelele se-
hemu za chini ya inchi, lieni milima kwa sifa,



Digitized by Google

Original from
HARVARD UNIVERSITY

mwitu, na miti yake yote, kwani ameko-
mboa Yahuwa Yakobo, na katika Israeli a-
tatukuka.
24 Ndilo asemalo Yahuwa, mkombozi wako,
na mfanya wewe katika tumboni, Ndimi
Yahuwa nifanyaye yote, ninyoshaye mbi-
ngu peke yangu, nitandaye inchi kwa mwe-
25 nyewe. Nivunjaye ishara zao wanenao u-
batili, na wachawi nawatia wazimo niwaru-
dishaye nyuma wenyi hekima, na elimu yao
26 naifanya upumbafu, nifanyaye imara neno
la mtumwa wangu, na shauri la mitume
wangu, niuambiaye Yerusalemi ukaliwe, na
miji ya Yuda mjengwe, nitainua maanguko
27 yao. Niambiaye kilindi, ukauke, na mito
28 yako nitanyausha. Nimnenaye Kuro, ndi-
ye mchunga wangu, atatenda niyapendayo
yote, akinena kwa Yerusalemi, ujengwe, na
kwa hekalu, misinji yako itiwe.
XLV. Ndilo amwambialo Yahuwa Masiya ya-
ke Kuro, niliyemshika mkono wa kuume,
kuangusha mbele yake mataifa, na kulege-
za viuno vya wafalme, kufungua mbele ya-
2 ke milango, wala mbau zisifungwe. Mimi



Digitized by Google

Original from
HARVARD UNIVERSITY

nitakwenda mbele yako, nitanyosha palipo-
potoka, milango ya shaba nitavunja, na ma-
3 pingo ya chuma nitakata. Nitakupa hazi-
na za gizani, na zilizofichwa kwa siri, ujue
ya kwamba ndimi Yahuwa, akuitaye jina
4 lako, Muungu wa Israeli. Kwa ajili ya
Yakobo mtumwa wangu, na Israeli mteule
wangu nimekuita jina lako, nimekutaja,
wala hukunijua.
5 Mimi Yahuwa, wala tena, illa mimi, ha-
pana Muungu, nimekufunga, wala hukuni-
6 jua. Wajue katika kutoka jua hatta ku-
shuka kwake, ya kwamba hakuna illa mi-
7 mi. Mimi Yahuwa, wala hapana tena. Ni-
fanyaye nuru, niumbaye giza, nitendaye a-
mani, niumbaye ubaya, mimi Yahuwa nifa-
8 nyaye haya yote. Nyeni enyi mbingu ka-
tika juu, mwageni, mawingu, haki; inchi
ifunuke, uchupuke wokovu, ioteshe adili
marra: mimi Yahuwa niliyeiumba.
9 Ole wake agombanaye na mfanya wake,
kigai kwa kigai cha inchi. Udongo umwa-
mbie mfanya wake ufanyaje? Ao kazi ya-
10 ko. Hana mikono? Ole wake amwambiaye



Digitized by Google Original from HARVARD UNIVERSITY

baba wake, umezaa nini? na mke, mimba
11 yako nini? Ndivyo asemavyo Yahuwa Mta-
katifu wa Israeli, na mfanyaji wake, kwayo
yatakayokuwa niulizeni, juu ya waana wa-
ngu, na juu ya kazi ya mikono yangu nita-
12 kieni. Mimi nimefanya inchi, na mtu juu
yake nimemumba mimi, mimi mikono yangu
nikatanda mbingu, na jeshi lao lote naliamu-
13 ru. Mimi nimemwondokesha katika haki,
na njia zake zote nitaagiza, yeye atajenga
mji wangu, na kufungwa kwangu atafu-
ngua, si kwa thamani, wala kwa zawadi, a-
mesema Yahuwa wa majeshi.
14 Ndilo asemalo Yahuwa, Kazi ya Misri na
biashara ya Kushi na Sebaim, watu ware-
fu, watavuka kwako, watakuwa kwako, wa-
takufuata, katika pingu watakuja, na kwa-
ko watainama, watakusihi wewe, Kwako
tu Muungu wala si mgine, illa Muungu.
15 Ndiwe yakini Muungu ujifichaye, Muungu
wa Israeli, Mwokozi.
16 Wameona haya, wamegeuka uso wote,
watakwenda zao kwa aibu wafanyao sana-
17 mu. Israeli ameokoka kwa Yahuwa, kwa



Digitized by Google
Original from
HARVARD UNIVERSITY

wokovu wa milele, hamtaona haya, wala ha-
18 mtageuka uso, hatta milele dayima. Kwa-
ni ndivyo asemavyo Yahuwa muumba mbi-
ngu, ndiye Muungu afanyaye inchi, aifa-
nyizaye, ndiye aliyetia imara, hakuiumba
burre, kwa kukaliwa ameifanya. Mimi Ya-
19 huwa wala hapana mgine, sikunena kwa siri
mahali pa giza pa inchi, sikuambia uzao wa
Yakobo, nitafute burre. Mimi Yahuwa a-
nenaye haki, atoaye adili.
20 Kusanyikeni njooni, karibuni pamoja ma-
huru ya mataifa, hawakujua watwekao mti
wa sanamu yao, waombao muungu asiyeo-
21 koa. Neneni wakaribisheni, wafanye shauri
pamoja. Nani aliyesikiza haya tangu hapo,
aliyeyanena tangu wakati ule? Siye mimi,
Yahuwa, wala si tena Muungu illa mimi,
Muungu wa haki, wala hapana aokoaye, illa
22 mimi. Angalieni mimi, mtaokoka 'ncha
zote za inchi, kwani ndimi Muungu hapana
23 mgine. Nimeapa kwa mimi, neno la haki
limetoka kanwani mwangu, halitarudi, kwa-
ni kwa mimi killa gote litakunjwa, killa u-
24 limi utaapa. Yakini kwa Yahuwa, atasema,



Digitized by Google
Original from
HARVARD UNIVERSITY

haki na uwezo, kwake watakuja, waone ha-
25 ya wote waliowaka juu yake. Kwa Yahu-
wa watatiwa haki wazao wote wa Israeli, na
watajisifu.

XLVI. Bel imeinama, Nebo imejiinamisha, sa-
namu zao ziko juu ya nyama, na ng'ombe,
machukuzi yenu mazito, mzigo wa mchovu.
2 Zimeinika zimeinama pamoja, hazikuweza
kuokoa mzigo, zenyewe zimekwenda kufu-
ngwa.
3 Sikieni mimi, nyumba ya Yakobo, na wo-
te waliosalia wa nyumba ya Israeli, walio-
chukuliwa tangu matumbo, waliotwaliwa
4 tangu tumboni. Hatta uzee mimi ndiye,
na hatta mvi mimi nitegemeao, mimi nime-
fanyiza, na mimi nitachukua, na mimi ni-
5 tategemea, na nitavukisha. Mtanifanya
sawa na nini, na mtanilinganisha, na mtani-
methilisha, nami nitafanana?
6 Hutoa sana thahabu katika mfuko, na
fetha wapima kwa mizani, wampe kwa kazi
mfua thahabu, aifanya muungu, waanguke
7 na wasujudie. Waichukua juu ya mabega,
waenda nayo, waiweka mahali pake, yasi-



Digitized by Google Original from HARVARD UNIVERSITY

mama, katika mahali pake haitoki. Na te-
na mtu akiiitia haijibu, katika mateso yake
8 haimwokoi. Kumbukeni haya, mkajionye-
she waume, wekeeni moyoni, mkosao.
9 Kumbukeni ya kwanza ya milele, kwani
mimi Muungu wala hapana tena, Muungu
10 wala hapana kama mimi. Kuhubiri tangu
mwanzo la mwisho, na tangu hapo lisilote-
ndwa, kunena, Shauri langu litasimama, na
11 killa niipendalo nitalifanya. Kuita ndege
mkali katika mashariki, katika inchi iliyo
mbali mume wa shauri langu, nami nimene-
na, nami nitaleta, nimekusudi, nami nitate-
nda.
12 Sikieni mimi, wenyi moyo hodari, walio
13 mbali ya haki, nitaleta karibu haki yangu,
haitakuwa mbali, wala wokovu wangu hau-
takawia, nitatoa katika Sayuni wokovu,
kwa Israeli utukufu wangu.
XLVII. Ushuke ukae mavumbini, bikira binti
Babeli, ukae chini, hapana kiti, binti Wa-
kasidi, kwani hutazidi kuitwa mwororo na
2 laini. Twaeni mawe ya kusagia, usagie u-
nga, funue nyele, funue mguu, funue paja,



Digitized by Google Original from HARVARD UNIVERSITY

3 uruke mito, utafunuka utupu wako, aibu ya-
ko itaonekana, tatwaa kisasi, siji kwa mwa-
4 na adamu. Mkombozi wetu Yahuwa wa
5 majeshi, jina lake Mtakatifu wa Israeli. U-
kae kimya uende zako gizani, binti Wakasi-
di, kwani hutazidi kuitwa, bibi wa wafalme.
6 Nalikuwa na hasira na watu wangu, nika-
tia vibaya urithi wangu, nikawaleta mkononi
mwako, hukuwafanyia rehema, juu ya mzee
7 umefanya mzigo wako mzito mno. Ukane-
na, nitakuwa bibi milele, hatta hukuyatia ha-
ya moyoni, wala bukukumbuka mwisho wao.
8 Sikie sasa haya, mwororo ukaaye katika
tumaini, ukinena moyoni mwako, Nidmi
wala hapana mgine, sitakaa mjaani wala si-
9 tajua kufiwa. Zitakupata hizi mbili gháfula
siku moja, kufiwa watoto na mume, pia zote
zitakupata, kwa wingi wa matendo yako
mabaya, kwa nguvu ya uchawi wako sana.
10 Ukatumaini katika maovu yako, ukane-
na, hakuna anionaye. Hekima yako na ma-
arifa yako yamekupindua, ukanena moyoni
mwako, Ndimi, wala hakuna illa mimi.
11 Utakuja juu yako ubaya, hutajua utokako,



Digitized by Google
Original from
HARVARD UNIVERSITY

utaanguka juu yako msiba, huwezi kuutu-
liza, utakuja juu yako marra uharibifu
usipojua.
12 Simama bassi na wachawi wako, na wi-
ngi wa kuloga kwako, uliotendea kazi ta-
ngu ujana wako, illi labuda uweze kufaa,
13 illi labuda upate nguvu. Umechoka kwa
wingi wa washauri wako, wasimame sasa,
wakuokoe, wajuao falaki, watazamao nyota,
wabashirio kwa mwezi, katika yale yataka-
14 yokupata. Wako kama makapi, moto uta-
wala, hawatavukisha maisha yao katika
mkono wa moto, silo kaa la kukotea moto,
15 moto wa kukalia. Hivi itakuwa kwako
nao waliotenda kazi nawe, wafanyi biashara
wako tangu ujana wako, killa mmoja upa-
nde wake wamepotea, hakuna akuokoaye.

XLVIII. Sikieni haya, Ee nyumba ya Yako-
bo, mlioitwa kwa jina la Israeli, mliotoka
katika maji ya Yuda, mwapao kwa jina la
Yahuwa, mnenao Muungu wa Israeli, si
kwa kweli, wala si kwa haki.
2 Kwani wajitaja wa mji mtakatifu, wate-
gemea juu ya Muungu wa Israeli, Yahuwa



Digitized by Google
Original from HARVARD UNIVERSITY

3 wa majeshi jina lake. Nimehubiri mambo
ya kwanza tangu mwanzo, yakatoka ki-
nwani mwangu, nikayaonyesha, nikatenda
4 marra, yakawa. Kwa sababu nalikujua
mkaidi, na shingo lako mshipi wa chuma,
5 na paji la uso wako shaba. Hatta tangu
mwanzo nimekuhubiria, mbele ya kuwa
nikakuonyesha, usipate kusema, sanamu
yangu imetenda hii, na sanamu iliyocho-
ngwa, na sanamu iliyoyeyushwa, imeziamu-
6 ru. Ulisikia, tazama haya yote, na ninyi
hamtanena? Nimekusikia mapya, tangu
7 sasa yaliyofichwa, wala hamkuyajua. Sasa
yameumbwa wala si wakati ule, wala mbe-
le ya leo, wala hamkuyasikia, msiseme,
8 nami naliyajua. Hatta hukusikia, hatta
hukujua, hatta tangu hapo halikuzibuka
sikio lako, kwani nalikujua kwa hila utafa-
nya hila, na mwenyi hila tangu tumboni
umeitwa wewe.

9 Kwa ajili ya jina langu nitaakirisha hasira
yangu, na kwa sifa zangu nitajizuia kwako,
10 nisikukatie mbali. Nami nimekusafisha,
wala si kwa fetha, nimekuchagua katika



Digitized by Google

Original from
HARVARD UNIVERSITY

11 tanuru la mateso. Kwa ajili yangu, kwa
ajili yangu nitafanya, gissi gani itiwe unajisi? wala sitampa mgine utukufu wangu.
12 Sikie mimi, Yakobo na Israeli, niliyekuita, mimi ndimi, mimi wa kwanza, mimi te-
13 na wa mwisho. Mkono wangu tena uliweka inchi, na mkono wangu wa kuume umepima mbingu, nikiziitia mimi, zitasimama
14 pamoja. Kusanyikeni ninyi nyote, mkasikie, nani wao aliyekubiri haya? Yahuwa alimpenda, atafanya alitakalo katika Babeli,
15 na mkono wake Wakasidi. Mimi, mimi nimenena, nikamwita tena, nalimleta atafanyikia njia yake.
16 Karibuni kwangu, sikieni haya, tangu mwanzo sikusema kwa siri, tangu yalipokuwa nipo mimi, na sasa Bwana Yahuwa
17 amenipeleka na Roho yake. Ndilo asemalo Yahuwa Mkombozi wako, Mtakatifu wa Israeli, Mimi Yahuwa Muungu wako nikufunzaye kwa kufaa, akuendeshaye katika njia utakayoendea.
18 Laiti ungalisikia amri zangu, ingalikuwa amani yako kama mto wa maji, na haki ya-



Digitized by Google Original from HARVARD UNIVERSITY

19 ko kama mawimbi ya bahari. Wangali-
kuwa kama mchanga wazao wako, na wa-
tokao matumbo yako kama vikokoto vyake,
wala halingalikatika, wala halingalifutiwa
jina lake mbele yangu.
20 Tokeni katika Babeli, kimbieni katika
Wakasidi, kwa sauti ya kuimba mhubiri,
msikize haya, mweneze hatta mwisho wa
inchi, semeni, Amekomboa Yahuwa mtu-
21 mwa wake Yakobo. Wala hawakuona kiu
alipowaleta katika jangwa, akatokeza kwao
maji katika mwamba, akapasua mwamba,
22 yakatoka maji. Hapana amani, amesema
Yahuwa, kwa mabaya.
XLIX. Sikieni mimi, visiwa, kasikilizeni mata-
ifa wa mbali, Yahuwa katika tumboni ali-
niita, katika tumbo la mamangu alikumbu-
2 sha jina langu. Akafanya kinwa changu
kama upanga mkali, kivulini mwa mkono
wake akanisetiri, akanifanya mshale ulioza-
3 gaa akanificha katika podo lake. Akania-
mbia, Mtumwa wangu wee, Israeli, kwani
4 kwa wewe nitajisifu. Nikanena mimi, ni-
metenda kazi burre, kwa ubatili na kisicho-



Digitized by Google
Original from
HARVARD UNIVERSITY

faa nimetumia nguvu zangu, illakini huku-
mu yangu kwa Yahuwa, na kazi yangu kwa
Muungu wangu.
5 Bassi akanena Yahuwa anifanyaye katika
tumboni, kwa mtumwa wake, nimletee tena
Yakobo, Israeli asipokusanyika nitakuwa
mtukufu machoni pa Yahuwa, na Muungu
wangu ndiye nguvu zangu.
6 Akanena, Chepesi uwe wewe kwangu
mtumwa, uinue makabila ya Yakobo, uwa-
rudishe waliovuka wa Israeli, nitakufanya
nuru kwa mataifa, uwe na wokovu wangu
hatta mwisho wa inchi.
7 Ndilo asemalo Yahuwa mkombozi wa
Israeli, mtakatifu wake, kwa yule aliyetha-
rauliwa na mtu, aliyechukiwa na taifa, kwa
mtumwa wa wakuu, Wafalme wataona wa-
taondoka, wakuu watasujudu, kwa sababu
ya Yahuwa aliye amini, Mtakatifu wa Isra-
eli, aliyekuchagua.
8 Ndilo asemalo Yahuwa, Wakati wa ku-
pendeza nimekusikia, na siku ya kusayidia
mimi kwako, nitakuhifathi, nitakuweka
kwa agano la watu, kuiinua inchi, kurithi-



Digitized by Google
Original from
HARVARD UNIVERSITY

9 sha urithi ulioharibika. Uwaambie walio-
fungwa, tokeni, nao walio gizani, mjionye-
she. Watalishwa njiani, na mahali pote pa
10 juu malisho yao. Hawataona njaa tena
wala kiu, wala hari wala jua halitawapiga
tena, kwani awarehemuye atawaongoza,
hatta kwa chemchemi za maji atawachukua.
11 Nami nitafanya milima yangu yote njia, na
12 njia pana zangu zitakuwa juu. Angalieni,
hawa wanakuja katika mbali, na hawa
katika kaskazini, na katika magaribi na
hawa katika inchi ya Sinim.
13 Imbeni, mbingu, ufurahi, inchi, pigeni
kelele mkiimba, milima, kwani Yahuwa a-
metuliza watu wake, akarehemu wateswa
14 wake. Sayuni ikanena, Ameniacha Yahu-
15 wa, Bwana amenisahau. Atasahau mwana-
mke mtoto wake anyonyaye, asirehemu
waana wa tumbo lake, hatta hawa wakisa-
16 hau, mimi sikusahau wewe. Angalia, ni-
mekuandika juu ya vitanga vya mikono
yangu, kuta zako mbele yangu dayima.
17 Wafanya hima wakujengao, wakuharibuo,
wakuangushao watatoka kwako.



Digitized by Google
Original from
HARVARD UNIVERSITY

18 Inue macho yako kuzunguka ukaone,
hawa wote wajikusanya kwako, watakujia.
Mimi hayi amesema Yahuwa, kwani kwa
hawa wote utajipamba kwa uzuri utajifu-
19 ngia kama arusi. Kwani unyika wako, na
pasipo watu, na inchi ya uharibifu wako,
kwani sasa pembamba kwako kwa wakaao,
20 nao waliokumeza wako mbali. Hatta wa-
tasema masikioni mwako waana wa kufiwa
kwako, pembamba kwangu mahali, nipe
21 nafasi nikae. Nawe utasema moyoni, nani
aliyenizalia hawa, nami nimefiwa, na peke
yangu, kuhamishwa na kusafiri, nani aliyelea
hawa? Mimi nimeachwa peke yangu, wali-
kuwa wapi hawa?

22 Ndilo asemalo Bwana Yahuwa, Nitainua
mkono wangu kwa mataifa, na kwa watu
nitatweka bandera yangu, wataleta waana
wako katika kifua na binti zako watachu-
23 kuliwa begani. Watakuwa wafalme baba
zako za kunyonya, na malkia mama zao wa
kunyonya, uso kwa inchi watakuinamia, na
mavumbi ya miguuni pako wataramba, wa-
tajua ya kwamba ndimi Yahuwa, hawatao-



Digitized by Google
Original from
HARVARD UNIVERSITY

na haya waningojao.
24 Ataondolewa aliye hodari mateka, aliye-
25 twaliwa kwa haki atatoka? Kwani ndivyo
asemavyo Yahuwa, hatta waliotwaliwa nao
walio hodari wataondolewa, na mateka ya
mjeuri watatoka, nitateta mimi nao watetao
nawe, na waana wako mimi nitawaokoa.
26 Nitawalisha wakutetao na nyama zao we-
nyewe, na kama mvinyo watalewa na damu
zao wenyewe, nao wenyi mwili wote wata-
jua ya kwamba mimi Yahuwa akuokoaye
na mkombozi wako, mwenyi nguvu wa Is-
raeli.
L. Ndilo asemalo Yahuwa, Iko wapi khati
ya talaka ya mama wako, niliyemwacha?
Ao kwa yupi aniwiaye nimewakuza? Anga-
lieni kwa maovu yenu mmejiuza wenyewe,
na kwa makosa yenu mama wenu ameachwa.
2 Kwa hiyo nikija hapana mtu, nikiita ha-
pana kujibu. Kupunguka umepunguka
mkono wangu katika kukomboa, wala ha-
pana kwangu uwezo wa kuponya? Angalia,
kwa kukemea mimi nakausha bahari, na-
fanya mito jangwa, zitaoza samaki zao kwa



Digitized by Google
Original from
HARVARD UNIVERSITY

3 kukosa maji, zitakufa kwa kiu. Nazivika
mbingu kwa weusi, nafanya sako kifuniko
4 chao. Bwana Yahuwa amenipa ulimi wa
waalimu, nijue kumwambia neno aliyecho-
ka wakati wake, huamsha assubuhi assubu-
hi, huniamsha sikio nisikie kama waalimu.
5 Bwana Yahuwa amenifukua sikio wala
6 mimi si mwasi, sikurudi nyuma. Nalitoa
mwili kwa wapigao, na machavu yangu kwao
wang'oao nyele sikuficha uso wangu katika
manyonge na mate.
7 Naye Bwana Yahuwa atanisayidia, kwa
hiyo sioni haya, kwa hiyo nimeweka uso
wangu kama jiwe, nikajua ya kwamba si-
8 taaibika. Karibu anifanyaye haki, nani a-
takayeshindana nami? tusimame pamoja,
9 anishtakiye nani? aje kwangu. Tazama
Bwana Yahuwa atanisayidia, nani atakaye-
nihukumu? Hawa wote watachakaa, noo-
ndo itawala.
10 Nani kwenu amwogopaye Yahuwa asiki-
aye sauti ya mtumwa wake, aendaye katika
giza, wala hapana kuangaza kwake, atumai-
ni kwa jina la Yahuwa, ategemee kwa



Digitized by Google
Original from
HARVARD UNIVERSITY

11 Muungu wake. Enyi nyote mwashao mo-
to, mjizungushao macheche, enendeni kati-
ka anga la moto wenu, na katika macheche
mliyoyawasha. Kwa mkono wangu itaku-
wa kwenu hivi, katika huzuni mtalala.

LI. Sikieni mimi mfuatao haki, mtafutao Ya-
huwa, tazameni mwamba mlikokatika, na
2 kuchimbuka birika mlikovutiwa. Tazame-
ni Ibrahimu baba wenu, na Sara aliyewazaa,
kwani peke yake nalimwita, nikambariki,
3 nikamzidisha. Kwani Yahuwa atatuliza
Sayuni, atatuliza maharibifu yake yote, a-
tafanya unyika wake kama Adeni, na ja-
ngwa lake kama bustani ya Muungu. Fu-
raha na kicheko kitaonekana kwake, kushu-
kuru na sauti ya kuimba.

4 Sikilizeni mimi watu wangu, taifa langu,
mnipe masikio, kwani sheria itatoka kwa-
ngu, na hukumu yangu nitaisterehisha kwa
5 nuru ya watu. Haki yangu karibu umeto-
ka wokovu wangu, mikono yangu itawahu-
kumia watu. Kwa mimi visiwa vitangoja,
6 na kwa mkono wangu watatazamia. Inueni
mbinguni macho yenu, mkatazame inchi



Digitized by Google
Original from
HARVARD UNIVERSITY

chini, kwani mbingu kama moshi zimepita,
na inchi kama nguo itachakaa, na wakaao
humo watakufa pamoja, na wokovu wangu
utakuwa milele, na haki yangu haitavunjika.
7 Nisikie mimi mjuao haki, watu wenyi
sheria yangu moyoni mwao, msiogope aibu
ya watu, wala kwa mashutumu yao msitiwe
8 hofu. Kwani kama vazi noondo itawala,
na kama suffuf itawaharibu, na haki yangu
itakuwa milele, na wokovu wangu kizazi
kwa kizazi.
9 Amke, amke, uvae nguvu, mkono wa
Yahuwa. Amke kama siku za kale, vizazi
vya milele. Siwe ndiwe uliyemkata mwenyi
10 kiburi, ukatia nyoka jeraha? Siwe ndiwe
uliyekausha bahari, maji ya vilindi vingi,
ukifanya malindi ya bahari njia ya kuvukia
11 waliokombolewa? Nao waliokombolewa
na Yahuwa watarudi, watakuja Sayuni na
kuimba, na furaha milele juu ya vitwa vyao.
Kicheko na furaha watapewa, zitakimbia
huzuni na kuugua.
12 Mimi, mimi ndimi awatulizaye, nani we-
we, utiwe hofu na mtu, atakufa, na mwana



Digitized by Google Original from HARVARD UNIVERSITY

13 Adamu, kama majani atakuwa. Ukamsa-
hau Yahuwa aliyekufanya, atandaye mbi-
ngu, awekaye inchi, ukaogopa dayima killa
siku mbele ya hasira yake aoneaye, akijifa-
nya tayari aharibu. Iko wapi hasira yake
aonaye?
14 Hufanya haraka aliyehamishwa afunguli-
we, asife katika shimo, wala chakula chake
15 kisipunguke. Na mimi Yahuwa Muungu
wako atengaye bahari, mawimbi yake ya-
kavuma, Yahuwa wa majeshi jina lake.
16 Nikaweka maneno yangu kinwani mwako
na katika kivuli cha mkono wangu nimeku-
hifathi, niziweke mbingu, nifanye imara in-
chi, niambie Sayuni, ndiwe watu wangu.
17 Amke, amke, ondoke Yerusalemi, uliye-
kunywa kwa mkono wa Yahuwa kikombe
cha hasira yake, chembe cha kikombe cha
18 shidda umekunywa umesonga. Hapana kio-
ngozi kwake katika waana wote aliowazalia,
wala amshikaye mkono, katika waana wote
19 aliowalea. Haya mawili yamekupata, nani
atakayelia nawe, kuachwa, kuharibika, na
20 njaa, na upanga, kwa nani nikutulize? Wa-



Digitized by Google

Original from
HARVARD UNIVERSITY

ana wako wamezimia, wamelazwa mwanzo
wa killa njia, kama ng'ombe wa mwitu ka-
tika wavu, wamejaa hasira ya Yahuwa, ku-
kemea Muungu wako.
21 Kwa hiyo sikie bassi haya, uliyeteswa, na
22 uliyelewa, illa si kwa mvinyo. Ndilo ase-
malo Bwana wako Yahuwa, na Muungu
wako atetaye kwa watu wake, Nimeondoa
katika mkononi mwako kikombe cha shidda
chembe cha kikombe cha hasira yangu, hu-
23 tazidi kukinywa tena. Nitakitia mkononi
mwao anayekuharibu, waliokuambia nafusi,
iname tupite, ukaweke kama inchi mwili
wako, na kama njia kwao waliopita.
LII. Amke, amke, uvae nguvu zako Sayuni,
uvae mavazi ya utukufu wako, Yerusalemi
mji mtakatifu, kwani hatazidi kuja kwako
2 asiyetahiriwa wala mnajisi. Ujikung'ute
katika mavumbi, ondoke uketi Yerusalemi,
jifungulie mafungo ya shingoni mwako,
binti Sayuni uliyefungwa.
3 Kwani ndilo asemalo Yahuwa, Umeku-
zwa burre, na pasipo fetha utakombolewa.
4 Kwani ndilo asemalo Bwana Yahuwa, wa-



Digitized by Google
Original from
HARVARD UNIVERSITY

lishuka wetu wangu Misri kwanza, wasa-
5 firi huko, Ashur wakawaonea burre. Bassi
sasa ninani hapa, amesema Yahuwa, kwani
watu wangu wamechukuliwa burre, wawa-
tawalao wawafanye walie, amesema Yahu-
wa, na dayima killa siku jina langu lane-
6 nwa unajisi. Kwa hiyo watu wangu wata-
nijua jina langu, kwa hiyo siku ile, ndimi
mimi, ninaye, nipo mimi.
7 Wazuri mno juu ya milima miguu yake
abashiriye, asikizaye amani, abashiriaye
mema, asikizaye wokovu, aambiaye Sayuni,
8 amiliki Muungu wako. Walinzi wako wa-
tapaliza sauti, wataimba sauti pamoja, kwa-
ni jicho kwa jicho wataona, arudishapo
Yahuwa Sayuni.
9 Pigeni kelele, imbeni pamoja, maharibi-
ka ya Yerusalemi, kwani Yahuwa ametuliza
10 watu wake, amekomboa Yerusalemi. A-
meweka wazi Yahuwa mkono wa utakatifu
wake machoni pa mataifa yote, wataona
'ncha zote za inchi wokovu wa Muungu
wetu.
11 Tokeni, tokeni, ondokeni huko, msiguse



Digitized by Google

Original from
HARVARD UNIVERSITY

uchafu, ondokeni katika kati yake, jitaka-
seni, mchukuao vyombo vya Yahuwa.
12 Kwani si kwa haraka mtatoka, wala si kwa
kukimbia mtakwenda, kwani apitaye mbele
yenu Yahuwa, naye awakusanyaye Muungu
wa Israeli.
13 Yuko mtumwa wangu atatenda busara,
atatukuka, atainuka, atakuwa juu sana.
14 Kama wengi walivyoshangaa kwako, ame-
haribika kuliko mtu uso wake, na umbo
15 lake kuliko waana adamu. Hivi atanyuni-
za mataifa mengi, juu yake wafalme wata-
fumba kinwa, kwani yasiyohubiriwa kwao,
wataona, wasiosikia watafikiri.
LIII. Nani aliyesadiki habari zetu, na mkono
2 wa Yahuwa amefunuliwa nani? Atakuwa
kama chupuko mbele yake, na kama shina
katika inchi kavu hana namna, wala uzuri,
tukimwona, wala kuangaliwa tumtamani.
3 Ametharauliwa, watu wakamkataa, mtu wa
huzuni, ajuaye ugonjwa, kama kuficha uso
kwake, akatharauliwa, hatukumwona kitu.
4 Yakini ugonjwa wetu huyu amechukua,
na huzuni zetu amezitweka, tukamwona



Digitized by Google
Original from
HARVARD UNIVERSITY

amepigwa, ameteswa na Muungu, amethili-
5 ka. Naye alijeruhi kwa makosa yetu, aka-
pondwa kwa maovu yetu athabu ya amani
yetu juu yake, na kwa machubuko yake
tumepona.
6 Sisi wote kama kondoo tumepotea killa
mtu kwa njia yake tumezunguka, na Yahu-
wa ameleta juu yake maovu yetu sisi sote.
7 Alionewa, aliteswa, wala hakufunua kinwa,
kama mwana kondoo alichukuliwa kuuawa,
na kama kondoo kwa wale wakatao suffuf,
akanyamaza hakufumbua kinwa.
8 Alitwaliwa katika kufungwa na katika
kuhukumiwa, na kizazi chake nani ataka-
yenena, kwani alikatika katika inchi ya
wahayi, kwa makosa ya watu wangu alipi-
9 gwa. Akafanya pamoja na waovu kuzikwa
kwake na pamoja na tajiri katika mauti
yake, kwa sababu hakutenda jeuri, wala
hila kinwani mwake.
10 Yahuwa akapenda kumchubua, akampa
ugonjwa, ukifanya nafusi yake thabihu
kwa thambi, ataona uzao, atazidisha siku,
mapenzi ya Yahuwa mkononi mwake yata-



Digitized by Google
Original from
HARVARD UNIVERSITY

11 fanikiwa. Ataona ya kazi ya nafusi yake,
atashiba, kwa maarifa yake mtumwa wa
haki yangu atawapa haki wengi, na maovu
yao atachukua.
12 Kwa hiyo nitampa sehemu na wakuu, na
pamoja nao walio hodari atagawanya mate-
ka, kwa sababu amemimina nafusi yake
katika kufa, na pamoja na wakosao akaha-
sibika, naye akatwaa thambi za wengi,
akawaombea wakosao.
LIV. Utoe sifa mtasa usiyezaa, upige kelele
ukiimba, usiye na mimba, kwani waanawe
aliyeachwa wengi kuliko waanawe aliye
2 na mume, amenena Yahuwa. Upanue ma-
hali pa hema yako, na mapazia ya masika-
ni yako uyanyoshe, usiache, ufanye ndefu
kamba zako, ufanye imara mismari yako.
3 Kwani upande wa kuume na wa kushoto
utatoka, na uzao wako utawarithi mataifa,
utafanya miji iliyoachwa ikaliwe.
4 Usiogope kwani hutatiwa haya, wala hu-
tageuka uso, kwani hutaaibika, kwani haya
ya ujana wako utaisahau, na aibu ya ujaani
5 wako hutaikumbuka tena. Kwani mume



Digitized by Google
Original from
HARVARD UNIVERSITY

wako mfanya wewe, Yahuwa wa majeshi
jina lake, na mkombozi wako, Mtakatifu
wa Israeli, Muungu wa inchi yote ataitwa.
6 Kwani kama mke aliyeachwa, aliyeteswa
rohoni, amekuita Yahuwa, na mke wa ujana,
ulipoachwa, amesema Muungu wako.
7 Muda mdogo nimekuacha na kwa rehe-
8 ma nyingi nitakukusanya. Kwa hasira ya
kiasi nalificha uso wangu muda kwako, na
kwa rehema ya milele nimekurehemu, ame-
9 sema mkombozi wako Yahuwa. Kwani
maji ya Nuhu haya kwangu, nilivyoapa
maji ya Nuhu yasipite tena juu ya inchi,
hivi nimeapa sitaona hasira juu yako, wala
10 sitakukemea. Kwani milima itaondoka,
na vilima vitaondolewa, wala rehema yangu
haitaondoka kwako, wala agano la amani
yangu halitaondolewa, amesema akurehe-
muye Yahuwa.
11 Ee uliyeteswa, uliyechukuliwa na tufano,
usiyetulizwa, nipo mimi niwekaye kwa ra-
ngi nzuri mawe yako, nitakuweka kwa sa-
12 mawati misinji yako. Nitafanya madirisha
yako jiwe jekundu, na milango yako ya



Digitized by Google

Original from
HARVARD UNIVERSITY

mawe yawakayo, na killa mpaka wako kwa
13 mawe yapendezayo. Watoto wako wote
watafundishwa na Yahuwa, na amani nyi-
14 ngi kwa watoto wako. Katika haki utaku-
wa imara, utakuwa mbali ya kuonewa, kwa-
ni hutaogopa, na katika kupondeka, kwani
hakutakukaribia.

15 Kukusanya watajikusanya illa si kwa mi-
mi killa akusanyikaye kwako juu yako a-
16 taanguka. Ndimi mimi niliyemumba mfua
akivukuta katika makaa ya moto, aletaye
chombo cha kazi yake, nami nimemumba
mthuru aharibu.

17 Killa kilichofanyika juu yako hakitasita-
wi, na killa ulimi uondokaye juu yako kati-
ka hukumu utahukumia: ndiyo urithi wa
watumwa wa Yahuwa na haki yao katika
kwangu, amesema Yahuwa.

LV. Ee killa aonaye kiu, njooni majini, naye
asiye na fetha njooni, nunueni, mle, njooni
mnunue pasipo fetha na pasipo thamani
mvinyo na maziwa.

2 Kwa nini mwatoa fetha kwa kisicho cha-
kula, na kazi yenu kwa kisichoshibisha?



Digitized by Google
Original from
HARVARD UNIVERSITY

Kusikia sikieni mimi, mle mema, mkafura-
3 hiwe nafusi zenu kwa manono. Inameni
sikio lenu, njooni kwangu, sikieni na nafusi
yenu itaishi, nitafanya nanyi agano la milele,
rehema imara za Daudi.
4 Yuko, nime'mweka kwa shahidi kwa wa-
5 tu, mkuu, na aamuruye watu. Taifa usi-
lolijua utaita, na taifa lisilokujua wewe, wa-
takujia mbio, kwa ajili ya Yahuwa Muungu
wako, na Mtakatifu wa Israeli kwani ame-
6 kutukuza. Tafuteni Yahuwa akionekana,
7 mwitie akiwa karibu. Aache mwovu njia
yake na mtu wa ubaya mawazo yake, waru-
di kwa Yahuwa, naye atawarehemu, na kwa
Muungu wetu, kwani atazidi kuachilia.
8 Kwani siyo mawazo yangu mawazo yenu,
wala njia zako njia zangu, amesema Yahu-
9 wa. Kwani mbingu zilivyo juu kuliko inchi,
hivi juu njia zangu kuliko njia zenu, na ma-
10 wazo yangu kuliko mawazo yenu. Kwani
kama mvua ishukavyo na theluji katika mbi-
nguni, wala hairudi huko isiponywesha inchi,
ikaichupuza, ikaimeesha, apewe mbegu a-
11 pandaye, na chakula alaye, hivi litakuwa ne-



Digitized by Google Original from HARVARD UNIVERSITY

no langu, litokalo kinwani mwangu, halinirudii burre lisipofanya nilivyopenda, nalo litafanikiwa kwa ile niliyolipelekea.
12 Kwani kwa furaha mtatoka, na kwa amani mtaletwa, milima na vilima vitapiga kelele mbele yenu vikiimba, na killa mti wa
13 mwituni utapiga makofi. Mahali pa mwiba itamea mberoshi, na mahali pa mbigili mhades, itakuwa kwa Yahuwa kwa jina, kwa ishara ya milele isivyokatika.

LVI. Ndilo asemalo Yahuwa, shikeni hukumu, mkafanye haki, kwani karibu ni wokovu
2 wangu kuja, na haki yangu ifunuke. Heri mtu atendaye haya, na mwana Adamu ashikaye hilo, kulinda sabato katika unajisi, na kujilinda mkono katika kutenda uwovu wote.
3 Wala asiseme mwana wa mgeni aambatanaye na Yahuwa, kunena, kutengwa nimetengwa na Yahuwa katika watu wake, wala asiseme towashi, nipo mimi mti uliokauka.
4 Kwani ndiyo asemayo Yahuwa kwa matowashi watakaolinda sabato zangu, watakao niliyopenda mimi, na washikao agano langu,
5 nitawapa hawa nyumbani mwangu, na kati-



Digitized by Google Original from HARVARD UNIVERSITY

ka kuta zangu, mkono na jina kupita waa-
na na binti, jina la milele nitawapa, wala
halitapotea.
6 Na waana wa mgeni watakaoambatana
na Yahuwa kumngojea na kupenda jina la
Yahuwa, kuwa kwake kwa watumwa, killa
alindaye sabato isitiwe unajisi, na washikao
7 agano langu, nitawaleta kwa mlima wa uta-
katifu wangu, nitawafurahisha nyumbani
mwangu mwa kuomba, makafara yao na
thabihu zao, kukubalika juu ya mathbahu
yangu,kwani nyumba yangu nyumba ya
8 kuomba itaitwa, kwa watu wote. Asema
Bwana Yahuwa, akusanyaye waliofukuzwa
wa Israeli, nitakusanya tena kuliko kusa-
nyiko lake.
9 Nyama zote za mashamba njooni kula,
10 killa nyama ya mwituni. Walinzi wake vi-
pofu, wote wajinga, wote mbwa bubu, ha-
wawezi kulia, waotao, walalao, wapendao
11 usingizi. Nao mbwa wakali wasiojua ku-
shiba, nao wachungaji hawajui kufahamu,
wote kwa njia yake wameangalia, kwa fayi-
12 da yake yeye hatta mwisho. Njooni nita-



Digitized by Google Original from HARVARD UNIVERSITY

twaa mvinyo, tutakunywa kileo, itakuwa
kama leo kesho, na kuzidi sana.
LVII. Mwenyi haki amepotea wala hakuna a-
wekaye moyoni, na watu wa rehema wame-
twaliwa, wala hapana afikiriye ya kwamba
mbele ya mabaya ametwaliwa mwenyi haki.
2 Ataingia katika amani, watastarehe katika
malalo yao, waendao mbele yake.
3 Nanyi karibuni waana wa wachawi, uzao
4 wa uzinzi na asharati. Mmemthihaki nani,
juu ya nani mmefumbua kinwa, mmetoza
ulimi? Sinyi waana wa makosa, uzao wa
5 uwongo? Mkifanya nyegi kwa miti miku-
bwa chini ya killa mti umeao, mkichinja
watoto katika wadi chini ya miamba iliyo-
pasuka.
6 Katika vikokoto vya mtoni sehemu yako,
hivi ndivyo kura yako, kwa hivi mmemimi-
na sadaka ya kunywa, mmetoa sadaka ya
unga, nifarajike na haya?
7 Juu ya mlima mrefu uendao juu umewe-
ka malalo yako, hatta huko umepanda mtoa
8 thabihu. Na nyuma ya mlango, na mwi-
mo umeweka makumbusho yako, kwani si



Digitized by Google

Original from
HARVARD UNIVERSITY

mimi uliyefunuliwa, ukapanda, umepanua
malalo yako, umejichongea kuliko wale, u-
9 mependa malalo yao, mahali ulipoona. U-
kamwendea mfalme kwa marhamu, ukazidi-
sha rangi zako, ukapeleka wajumbe wako
10 hatta mbali, ukajithili hatta kaburini. Kwa
kuwa nyingi njia zako umechoka, wala hu-
kunena, imekatika tamaa, chakula cha mko-
no wako umekiona, kwa hiyo hukuhuzuni-
ka.
11 Umemwogopa nani ukaona hofu, useme
uwongo, wala hukunikumbuka mimi, wala
hukujitia moyoni? Si mimi niliyenyamaza
12 tangu milele, wala hukuniogopa. Nitahu-
biri haki yako, na matendo yako, wala ha-
13 yakukufaa. Uliapo, wakuponye wenzako,
na wote watachukuliwa na upepo, watachu-
kuliwa na ubatili, naye anitarajiaye atairithi
inchi, ataumiliki mlima wa watakatifu wa-
14 ngu. Akinena, fanyizeni, fanyizeni, fanye-
ni sawa njia, ondoeni kwazo katika njia ya
watu wangu.
15 Kwani ndilo asemalo aliye juu, aliyetu-
kuka akaaye pa milele, na Mtakatifu jina



Digitized by Google
Original from
HARVARD UNIVERSITY

lake, kwa juu na patakatifu nitakaa, na kwa
kupondeka na kunenyekea roho, nifanye
hayi roho yao wanenyekeao, niwajilie wenyi
16 moyo uliopondeka. Kwani sitateta milele,
wala hatta mwisho sitaona hasira, kwani ro-
ho mbele yangu ingezimika, na nafusi nili-
zifanya.
17 Kwa uovu wa tamaa zake naliona hasira,
nikampiga, kunificha nikaghathabika, aka-
18 enda kipotoe njia ya moyo wake. Njia za-
ke nimeziona, nitamponya, nitamsterehisha,
nitamrudisha faraja yeye, nao wamliliao.
19 Naumba uzao wa midomo, Amani amani,
mbali na karibu, amenena Yahuwa, nime-
20 mponya. Na waovu kama bahari iliyocha-
fuka, isiyoweza kutulia, maji yake yakitoa
21 tope na taka. Hapana amani, amesema
Muungu wangu, kwa waovu.
LVIII. Pigo kelele kooni, usiache, paliza
sauti yako kama paanda, kaonyeshe watu
wangu makosa yao, na nyumba ya Yakobo
2 thambi zao. Nami siku kwa siku wanita-
futa, wataka kujua njia zangu, kama taifa
waliofanya haki, wala hawakuacha hukumu



Digitized by Google Original from HARVARD UNIVERSITY

ya Muungu wao, waniulizia hukumu za ha-
ki, wapenda kumkaribia Muungu.
3 Kwa nini tumefunga, wasema, nawe hu-
kuona, tumetesa nafusi zetu wala hukujua.
Nanyi katika kufunga mmetaka, mlipe-
ndalo, na kazi zenu zote mmetwaa kwa
4 nguvu. Nanyi mmefunga kwa kuteta na
kugombana, na kutikisa konde vibaya. Ha-
mkufunga kama siku ya kusikiza juu sauti
5 yenu. Ndiyo hiyo kufunga nilivyochagua
siku ya kutesa mtu nafusi yake, kujiinama
kitwa kama mwanzi, na kutanda sako na
majifu? Ndiyo hiyo mliyoita kufunga, na
siku ya kumpendeza Yahuwa?
6 Siyo hiyo kufunga niliyochagua? kufungua
mafungo ya ubaya, kufungua mizigo mizito,
kuwaacha waliopondeka huru, na vunja
7 killa mti wa shingoni. Siyo kugawanya
chakula chako naye mwenyi njaa, na kuleta
nyumbani walioteswa wasio na kwao, uki-
mwona utupu umfunike, wala usijifiche
katika wenyi nyama moja nanyi.
8 Ndipo itakapotokea nuru yako kama
assubuhi, na afya yako itamea marra, ita-



Digitized by Google Original from HARVARD UNIVERSITY

kutangulia haki yako, utukufu wa Yahuwa
9 utakuhifathi. Utaomba na Yahuwa ataku-
sikia, utaita, naye atasema, mimi hapa.
Ukiondoa katika kati yako killa mti wa
shingoni, kutoa kidole na kunena maovu.
10 Ukimvutia mwenyi njaa nafusi yako,
ukishibisha nafusi iliyoteswa, nuru yako
itatoka gizani, na kiwi chako kama aththu-
11 uri. Naye Yahuwa atakuchukua dayima,
atashibisha nafusi yako wakati wa ukavu,
atanonesha mifupa yako, utakuwa kama bu-
stani iliyotiwa maji, na kama kutoka maji,
12 pasipokosa maji yake. Nao wako wataje-
nga tena palipoachwa zamani, misinji kwa
kizazi na kizazi utaifanya imara, utaitwa
azibaye mavunjiko, arudishaye mapito ya
kukalia.
13 Ukigeuza mguu wako katika sabato,
katika kutenda ulipendalo siku ya utakatifu
wangu, ukiita sabato furaha, takatifu ya
Yahuwa, tukufu, ukiitukuza, usipofanya
njia zako, usipoona ulipendalo, wala kunena
14 neno, ndipo utapendezewa kwa Yahuwa,
nami nitakupandisha juu ya pa juu pa inchi,



Digitized by Google Original from HARVARD UNIVERSITY

nitakulisha urithi wa Yakobo baba wako,
kwani kinwa cha Yahuwa kimenena.

LIX. Haukupunguka mkono wa Yahuwa u-
siokoe, wala hayakuzibwa masikio yake
2 asisikie. Maovu yenu yametenga ninyi
na Muungu wenu, na thambi zenu zime-
3 mficha uso asiwasikie. Kwani mikono ye-
nu imetiwa taka kwa damu, na mikono ye-
nu kwa uovu, midomo yenu imenena uwo-
ngo, ulimi wenu umezoea ubaya.
4 Hapana aitaye kwa haki, wala ahuku-
muye kweli, kutumaini juu ya ubatili, na
kunena uwongo, kupata mimba ya mathara,
5 kuzaa uovu. Watama mayayi ya pili, wa-
fuma tendabui, alaye mayayi yao hufa,
6 likivunjika hutoka nyoka. Tendabui yao
haitakuwa kuvaa, wala hawatajifunika kwa
kazi yao. Kazi yao kazi ya uovu, na ku-
7 tenda jeuri mkononi mwao. Miguu yao
huenda mbio kwa mabaya, hufanya haraka
kumwaga damu isiyo na hatiya. Mawazo
yao mawazo maovu, uharibifu na kuvunjika
8 katika njia zao. Njia ya amani hawakuijua,
hapana hukumu katika mwendo wao, ma-



Digitized by Google Original from HARVARD UNIVERSITY

pito yao yamepotoka, killa ayaendeaye hu-
kosa amani.
9 Kwa sababu hiyo hukumu mbali yetu,
wala haki haitushiki, twangoja nuru, nayo
10 giza, kwa anga, twaenda katika kiwi. Tu-
mepapasa kama vipofu ukuta, kama wasio
na macho twapapasa, tumejikwaa aththuuri
kama usiku, katika maharibifu kama wafu.
11 Tumevuma kama duba sote, na kama hua
kuugua tumeugua, tumengoja hukumu wala
haiko, na wokovu umekuwa mbali.
12 Kwani makosa yetu yamezidi mbele yako,
na thambi zetu zimejibu juu yetu, kwani
makosa yetu kwetu, na maovu yetu tumeya-
13 jua. Kukosa na uwongo kwa Yahuwa, na
kurudi katika kumfuata Muungu wetu,
kunena usingizio na kuasi, kuwaza na kufi-
14 kiri moyoni maneno ya uwongo. Imegeuka
nyuma hukumu, na haki imesimama mbali,
kwani kweli imeanguka njiani wala adili
15 haiwezi kuingia. Ikawa kweli haionekani,
arudiye katika mabaya hutekwa, Yahuwa
akaona na ubaya machoni pake, kwani
hapana hukumu.



Digitized by Google Original from HARVARD UNIVERSITY

16 Akaona ya kwamba hapana mtu, aka-
shangaa ya kwamba hapana mwombezi,
akajifanyia wokovu mkono wake, na haki
17 yake ikamtegemea. Akavaa haki kama chu-
ma, na chapeo cha wokovu kitwani mwake,
akavaa nguo za kisasi kwa mavao, akajiku-
18 njia kama joho uwivu. Kama kwa malipo,
kama kwa kurudisha hasira kwao watetao
naye, malipo kwa adui zake, kwa visiwa
19 atarudisha malipo. Wataogopa katika ma-
garibi jina la Yahuwa, na katika kutoka
jua utukufu wake. Akija kama mto wa
maji adui, roho ya Yahuwa itatweka ba-
ndera juu yake.

20 Atakuja kwa Sayuni mkombozi, na kwao
warudio katika makosa kwa Yakobo, ame-
21 nena Yahuwa. Na mimi ndilo agano langu
nao, amenena Yahuwa, Roho yangu juu
yako, na maneno yangu yaliyotiwa nami
kinwani mwako, hayatatoka katika kinwa-
ni mwako, na kinwani mwa uzao wako,
na kinwani mwa uzao wa uzao wako, ame-
nena Yahuwa, tangu leo hatta milele.

LX. Ondoke, uwe na nuru, kwani nuru yako



Digitized by Google Original from HARVARD UNIVERSITY

yaja, utukufu wa Yahuwa juu yako umeto-
2 ka. Kwani liko giza litaifunika inchi na
giza kuu watu, na juu yako atatokea Yahu-
wa na utukufu wake juu yako utaonekana.
3 Watakwenda watu katika nuru yako, na wa-
falme katika anga la kutokea kwako.
4 Inue macho yako kuzunguka, ukaone.
Hawa wote wamekusanyika kwako, wame-
kujia, waana wako katika mbali watakuja,
5 na binti zako mbavuni watalishwa. Ndipo
utakapoona, utang'aa, utaogopa, utapanua
moyo wako, kwani wamekugeukia wingi
wa bahari, uwezo wa mataifa utakujia.
6 Ngamia zilizo nyingi zitakufunikiza, nga-
mia wateule wa Mediani na Efa, wote wa
Seba watakuja, thahabu, na uvumba wata-
7 leta, na sifa za Yahuwa watazinena. Ma-
kundi yote ya Kedari watakukusanyikia,
kondoo waume wa Nebayoth watakungo-
jea, watapanda kwa kupendeza juu ya ma-
thabahu yangu, nyumba ya utukufu wangu
nitaitukuza.
8 Nani hawa kama mawingu warukao na
9 kama njiwa kwa madirisha yao? Kwani



Digitized by Google
Original from
HARVARD UNIVERSITY

visiwa vitaningoja na merikebu za Tarshi-
shi kwanza, kuleta waanawo katika mbali,
na fetha yao na thahahu yao pamoja nao,
kwa jina la Yahuwa Muungu wako, na
mtakatifu wa Israeli, kwani amekutuku-
10 za. Na waana wa wageni watajenga kuta
zako, na wafalme wao watakungojea, kwa-
ni katika hasira yangu nimekupiga na ka-
tika kupenda kwangu nimekurehemu.
11 Na malango yako yatakuwa mawazi da-
yima, mchana wala usiku hayafungwi, kule-
ta kwako uwezo wa mataifa, na wafalme
12 wao wameletwa. Kwani taifa na ufalme
usiokutumikia utapotea, hatta mataifa ya-
taharibika kabisa.
13 Utukufu wa Lebanoni utakujia, mbero-
shi, na mtidhar, na msherbini pamoja, ku-
tukuza mahali pa utakatifu wangu, na
mahali pa miguu yangu nitapatukuza.
14 Watakuja kwako kwa kuinama waana wao
waliokutesa watainama hatta nyayo za mi-
guu yako, wote waliokushutumu, nao wa-
takuita, mji wa Yahuwa, Sayuni ya Mta-
katifu wa Israeli.



Digitized by Google

Original from
HARVARD UNIVERSITY

15 Mahali pa kuwa umeachwa na umechuki-
wa, usiopitika, nitakufanya kilele cha zama-
16 ni, furaha ya kizazi na kizazi. Utanyonya
maziwa ya mataifa na ziwa la wafalme uta-
amua, utajua ya kwamba ndimi Yahuwa a-
kuokoaye, na Mkombozi wako mwenyi ngu-
17 vu wa Yakobo. Mahali pa shaba nitaleta
thahabu, na mahali pa chuma fetha, na pa
miti shaba, na pà mawe chuma, nitafanya
kodi yako amani, na ushuru wako haki.
18 Haitasikiwa tena kwako kunyang'anya,
kuthuru wala kuharibu katika mipaka ya-
ko, utaita kuta zako wokovu, na milango
19 yako sifa. Halitakuwa tena kwako jua
kwa nuru mchana, wala kwa anga mwezi
hautakutolea nuru, atakuwa kwako Yahu-
wa kwa nuru milele, na Muungu wako utu-
20 kufu wako. Halitashuka tena jua lako,
wala mwezi wako hautapunguka, kwani
Yahuwa atakuwa kwako kwa nuru milele,
itakwisha siku yako ya kulia.
21 Watu wako wote wenyi haki, kwa milele
watairithi inchi, mche niliopanda mimi,
kazi ya mikono yangu kunitukuza. Ndogo



Digitized by Google
Original from HARVARD UNIVERSITY

atakuwa elfu, na mwembamba taifa hodari,
Mimi Yahuwa wakati wake nitaihimiza.
LXI. Roho ya Yahuwa juu yangu, kwa sa-
babu Yahuwa amenitia mafuta niwabashirie
wenyi upole, amenipeleka niwafunge walio-
pondeka moyo, niwahubirie uhuru walio-
twaliwa, na kwao waliofungwa kufungua
2 mafungo. Nihubiri mwaka wa kumpende-
za Yahuwa na siku ya kisasi kwa Muungu
3 wetu, kuwatuliza wote waliao. Kuwafa-
nyia waliao katika Sayuni uzuri mahali pa
majifu, mafuta ya furaha pa kulia vazi la si-
fa pa roho ya shidda, wapate kuitwa miti
ya haki miche ya Yahuwa atukuzwe.
4 Watajenga maharibika ya zamani, pasi-
po watu zamani za kale watainua, watafa-
nya mipya miji iliyoharibika, palipoachwa
5 kizazi na kizazi. Watasimama wageni wa-
talisha makundi yako, na waana wa wageni
wakulima wako, na kutunza mizabibu.
6 Nanyi mtaitwa wakohani wa Yahuwa, wa-
ngoje wa Muungu wetu watawataja, mta-
kula mema ya mataifa, na kwa utukufu wao
mtajisifu.



Digitized by Google
Original from
HARVARD UNIVERSITY

7 Kwa aibu yenu maradufu, na kwa ma-
shutumu watafurahiwa na sehemu yao, kwa
hiyo katika inchi yao watapewa maradufu,
8 furaha ya milele itakuwa kwao. Kwani
mimi Yahuwa nipendaye hukumu, nichu-
kiaye yaliyoibwa kwa kafara, nami nitafa-
nya kazi yao kwa kweli, na agano la milele
9 nitapiga nao. Na wazao wao watajulika
kwa mataifa, nao wawatokeao kati ya watu,
wote wakiwaona watawatambua, kwani ndio
uzao uliobarikiwa na Yahuwa.

10 Kufurahi nitamfurahia Yahuwa nitape-
ndezewa nafusi yangu katika Muungu wa-
ngu, kwani amenivika vazi la wokovu, kwa
mavao ya haki amenikunjia, kama bwana
arusi ajiwekea fahari, na bibi arusi ajipamba
11 johari zake. Kwani kama inchi itoavyo
uchipuka wake, na kama bustani humeesha
mbegu zake, hivi Bwana Yahuwa atamee-
sha haki na sifa mbele ya mataifa yote.

LXII. Kwa ajili ya Sayuni sitanyamaza wala
kwa ajili ya Yerusalemi sitatulia, hatta ito-
kapo haki yake kama anga, na wokovu wa-
2 ke kama taa iwakayo. Wataona mataifa



Digitized by Google Original from HARVARD UNIVERSITY

haki yako, na wafalme wote utukufu wako.
Utatajwa jina jipya, kitakalotoa kinwa cha
Yahuwa.
3 Utakuwa taji ya utukufu mkononi mwa
Yahuwa na kilemba cha kifaume mkononi
4 mwa Muungu wako. Hutaitwa tena, ali-
yeachwa, wala inchi yako haitaitwa tena
iliyoharibika, kwani utatajwa nilipendalo na
inchi yako iliyomilikwa kwani Yahuwa a-
pendezaye nawe, na inchi yako itaolewa.
5 Kwani kama huoana kijana na bikira, hivi
waana wako wataoana na wewe, na furaha
ya mume juu ya mke, atafurahi Muungu
wako juu yako.
6 Juu ya ukuta wako Yerusalemi nimeweka
walinzi, usiku kucha na mchana kuchwa
dayima hawatanyamaza, wakimkumbusha
7 Yahuwa, msiwe na kimya. Msimfanyie ki-
mya, hatta afanyapo imara, na hatta awe-
kapo Yerusalemi sifa ya inchi yote.
8 Ameapa Yahuwa kwa mkono wake wa
kuume, na mkono wake wa nguvu, sitatoa
tena ngano yako kwa chakula cha adui za-
ko, wala waana wa wageni hawatakunywa



Digitized by Google Original from HARVARD UNIVERSITY

9 tena mvinyo wako, uliotendea kazi. Kwa-
ni waliokusanya watakula, nao watamsifu
Yahuwa, nao waliochuma watakunywa ka-
tika behewa za utakatifu wangu.
10 Piteni, piteni katika milangoni, fanyeni
sawa njia ya watu, fanyizeni, fanyizeni, njia
pana, ondoeni mawe yake, twekeni bandera
kwa watu.
11 Yahuwa amesikiza hatta mwisho wa in-
chi, Mwambieni binti Sayuni, wokovu wa-
ko waja, ijara yake naye, na kazi yake
12 mbele yake. Watawaita watu wa utaka-
tifu, waliokombolewa na Yahuwa, nawe u-
tatajwa uliotakwa, mji usioachwa.
LXIII. Nani huyu ajaye katika Edom na ma-
vazi mekundu katika Bozra? Huyu aliye
na nguo za fahari, akisafiri kwa wingi wa
nguvu zake?
Mimi ninenaye kwa haki, mkuu wa kuo-
koa.
2 Kwa nini mavazi yako mekundu na nguo
zako kama akanyagaye zabibu?
3 Nimekanyaga zabibu peke yangu, wala
katika watu hakuna mtu nami, nitawaka-



Digitized by Google Original from HARVARD UNIVERSITY

nyaga katika hasira yangu, nitawakanyaga-
kanyaga katika ghathabu yangu, na damu
zao zitarashiwa juu ya mavazi yangu, nami
4 nitatia rangi nguo zangu zote. Kwani si-
ku ya kisasi moyoni mwangu, na mwaka
wa wakombolewa wangu umekuja.
5 Nalitazama wala hapana msayidia, nika-
shangaa, hapana ategemeaye, nikaniletea
wokovu mkono wangu, na kuwaka kwangu
6 kukanichukua. Nitawakanyaga watu kati-
ka ghathabu yangu, nitawalevya kwa hasi-
ra yangu, nitashusha chini uwezo wao.
7 Nitakumbuka wema wa Yahuwa, sifa za
Yahuwa, kama kwa yote aliyotuletea Yahu-
wa, na wingi wa heri kwa nyumba ya Is-
raeli, waliopewa naye kwa rehema zake na
8 kwa wingi wa wema wake. Kwani alisema,
Lakini watu wangu hawa, waana wasio na
9 uwongo, akafanyika kwao mwokozi. Kati-
ka shidda zao zote aliona shidda, na malai-
ka wa uso wake akawaokoa. Kwa mape-
nzi yake na kwa upendeleo wake ndiye ali-
yewakomboa, akawatwaa, akawachukua si-
ku zote za zamani.



Digitized by Google
Original from HARVARD UNIVERSITY

10 Nao wakaasi, wakakasirisha roho ya uta-
katifu wake, akageuka kuwa adui, akapiga-
na nao mwenyewe.
11 Akakumbuka siku za zamani za Musa,
watu wake, Yuko wapi aliyewapandisha ka-
tika baharini, na wachungaji wa kundi la-
ke? Yuko wapi aliyeweka kati yao roho
12 ya utakatifu wake? Aliyewachukua kwa
mkono wa kuume wa Musa, kwa mkono
wa fahari wake, akitenga maji mbele yao,
13 ajifanyie jina la milele. Aliyewaleta kwa
vilindi kama frasi katika unyika wasijikwae.
14 Kama nyama wa boondeni akashuka, roho
ya Yahuwa ikimpumzisha. Hivi ukaleta
watu wako ujifanyie jina la fahari.
15 Angalie katika mbinguni, ukaone makao
ya utakatifu wako, na fahari yako, uko wa-
pi uwivu wako, na uwezo wako, sauti ya
moyo wako na huruma zako kwangu? Zi-
mezuiliwa?
16 Kwani ndiwe baba wetu, Ibrahimu asi-
potujua wala Israeli asipotutambua. Ndi-
we Yahuwa baba wetu, mkombozi wetu,
tangu milele jina lako.



Digitized by Google
Original from
HARVARD UNIVERSITY

17 Mbona umetukosesha, Yahuwa, katika
njia zako, umefanya mgumu moyo wetu
katika hofu yako? Geuke kwa watumwa
18 wako, kabila la urithi wako. Kidogo tu
wameimiliki watu wa utakatifu wako, adui
19 zetu wamekanyaga patakatifu pako. Tuli-
kuwa tangu zamani, hukuwamiliki wale,
wala halikuitwa juu yao jina lako.
LXIV. Laiti ungepasua mbingu, ungeshuka,
2 milima ingeyeyuka mbele yako, kama ku-
waka moto huyeyasha, maji yachemka kwa
moto, kuonyesha jina lako kwa adui zako,
3 mbele yako mataifa waogope. Ukifanya
ya hofu pasipo kutazamia, ukashuka, ikaye-
yuka milima mbele yako.
4 Wala tangu milele hawakusikia, wala
hawakupokea masikioni, wala jicho haliku-
ona Muungu illa wewe, amemfanyia amngo-
5 jaye. Umemkuta afurahiye, atendaye ha-
ki, wakukumbukao katika njia zako. Na-
we umeona hasira, tukatenda thambi, kati-
ka haya kuishi na tutaokoka.
6 Nasi sote wachafu, na kama kitambaa
cha taka haki zetu zote, tumekauka wote



Digitized by Google Original from HARVARD UNIVERSITY

kama jani, na maovu yetu kama upepo
7 yametuchukua. Hapana aitiaye jina lako,
ajitahidiye akushike, kwani umejificha uso
kwetu, umetulegeza kwa mkono wa maovu
yetu.

8 Bassi sasa Yahuwa, baba wetu ndiwe,
sisi udongo nawe mfinyangi wetu, na kazi
ya mkono wako sisi sote.

9 Usione hasira, Yahuwa, nyingi mno, wala
milele usikumbuke uovu, nawe uangalie,
twasihi, watu wako sisi sote.

10 Miji ya utakatifu wako imekuwa unyika,
Sayuni imekuwa unyika, Yerusalemi umea-
11 chwa. Nyumba ya utakatifu wetu na fa-
hari yetu, walipokusifu baba zetu, ime-
kuwa imeteketea kwa moto, killa kuta-
12 manika kwetu kumeharibika. Kwa haya
utajizuia, Yahuwa? Utanyamaza, utatutesa
sana mno?

LXV. Wamenitaka wasioniulizia, nimeone-
kana nao wasionitafuta, nimesema, Nipo,
nipo, kwa taifa lisiloitwa kwa jina langu.
2 Nimenyosha mikono yangu mchana kuchwa
kwa watu waasi, waendao katika njia isiyo



Digitized by Google
Original from HARVARD UNIVERSITY

3 njema, kwa mawazo yao. Watu wanitiao
hasira hatta mbele yangu dayima. Wakitoa
thabihu katika bustani, na wavukizao juu
4 ya matofali. Wakaao katika makaburi, na
katika makube wakaa usiku, walao nyama
ya nguruwe, na mchuzi wa machukizo
5 katika vyombo vyao. Wanenao ujitenge,
usinikaribie, kwani 'ni mtakatifu kuliko
wewe, hawa moshi puani mwangu, moto
uwakao mchana kuchwa.
6 Iko, imeandikwa mbele yangu, sitanya-
7 maza, nitalipa, nitalipa kifuani mwao, Ma-
ovu yenu na maovu ya baba zenu pamoja,
amenena Yahuwa, waliovukiza juu ya mili-
ma, na juu ya vilima walionishutumu, nami
nitawapimia kazi yao ya kwanza kifuani
mwao.
8 Ndivyo asemavyo Yahuwa, kama mvinyo
ukionekana katika tawi, husema, usiharibu
kwani mbaraka humo, hivi nitafanya kwa
ajili ya watumwa wangu, nisiwaharibu wote.
9 Nitaleta katika Yakobo uzao, na katika
Yuda amilikiye milima yangu, wateule wa-
ngu wataimiliki, na watumwa wangu wata-



Digitized by Google
Original from
HARVARD UNIVERSITY

10 kaa humo. Itakuwa Sharon kwa zizi la
makundi, na boonde Akor kwa kujilaza
ng'ombe, kwa watu wangu walionitafuta.
11 Nanyi waachao Yahuwa, wasahauo mli-
ma wa utakatifu wangu, mkifanyiza meza
kwa Bahati, na kujaza sadaka ya kunywa
12 kwa Ajali. Nitawahasibu ninyi kwa upanga,
na ninyi nyote mtainama mchinjwe. Kwa
sababu nimeita wala hamkuitika, nimenena
wala hamkusikia, mkatenda vibaya macho-
ni pangu, nayo nisiyoyapenda mmechagua.
13 Kwa hiyo ndivyo asemavyo Bwana Yahuwa,
Wako watumwa wangu watakula, nanyi
mtaona njaa, wako watumwa wangu wata-
kunywa, nanyi mtaona kiu, wako watumwa
wangu watafurahiwa nanyi mtatahayarika.
14 Wako watumwa wangu wataimba kwa
wema wa moyoni, nanyi mtalia kwa huzuni
wa moyoni, na kuvunjwa roho mtapiga
15 yowe. Mtaacha jina lenu kwa laana kwa
wateule wangu, naye Bwana Yahuwa ata-
waua, ataita watumwa wake kwa jina lingi-
16 nelo. Ajibarikiye katika inchi, ajibariki
kwa Muungu amina, na aapaye katika inchi,



Digitized by Google
Original from
HARVARD UNIVERSITY

aape kwa Muungu amina. Kwani shidda
za kwanza zimesahauliwa, na kwani zimefi-
chwa machoni pangu.
17 Kwani nipo mimi niumbaye mbingu mpya
na inchi mpya, wala hazitakumbukwa za
18 kwanza, wala hazitatiwa moyo. Illakini
furahini, shangilieni dayima kwa hizi nizi-
umbazo, kwani mimi niumbaye Yerusalemi
19 shangwi na watu wake furaha. Nitashangi-
lia kwa Yerusalemi, nitawafurahia watu wa-
ngu, wala haitasikiwa tena humo sauti ya
kulia wala sauti ya yowe.
20 Hatakuwa humo tena mtoto wa siku, wa-
la mzee, asiyetimia siku zake. Kwani kija-
na mwenyi miaka mia atakufa, na mwenyi
21 thambi mwenyi miaka mia atalaaniwa. Nao
watajenga nyumba watajikalia watapanda
22 mizabibu, watakula mazao yao. Hawataje-
nga na mgine atakalia, wala hawatapanda
na mgine atakula, kwani kama siku za mti
siku za watu wangu, na kazi ya mikono yao
watatumia pia wateule wangu.
23 Hawatatenda kazi burre, wala hawatazaa
kwa taabu, kwani uzao wa mbaraka wa Ya-



Digitized by Google
Original from
HARVARD UNIVERSITY

huwa hawa, na watokao kwao pamoja nao.
24 Itakuwa mbele ya kuita mimi nitasikiliza,
hatta wakiwa katika kunena mimi nitasikia.
25 Mbwa wa mwituni na mwana kondoo wataji-
lisha pamoja, na simba kama ng'ombe ata-
kula majani, na nyoka mavumbi yake. Ha-
watathuru, wala hawataharibu katika mli-
ma wote wa utakatifu wangu, amenena Ya-
huwa.

LXVI. Ndilo anenalo Yahuwa, mbingu kiti
changu na inchi pa miguu yangu, wapi
nyumba hiyo mtanijengea mimi, na wapi
2 mahali pale pa kunipumzisha? Nayo haya
yote mkono wangu umeyafanya, nayo yote
yamekuwa, amesema Yahuwa. Nitamwa-
ngalia aliyeteswa, aliyepondeka roho, atete-
mekaye kwa neno langu.
3 Achinjaye ng'ombe, kama apigaye mtu,
afanyaye thabihu ya mwana kondoo kama
amkataye mbwa kitwa, afanyaye sadaka ya
unga damu ya nguruwe, avukizaye uvumba
abarikiye ubatili. Hatta hiyo wamechagua
katika njia zao, na katika machukizo yao
nafusi yao imependezwa.



Digitized by Google

Original from
HARVARD UNIVERSITY

4 Hatta mimi nitachagua waliyoyafikiri, na
hofu zao nitazileta, kwa sababu nikiita ha-
wakuitika, nikinena hawakusikia, wakate-
nda mabaya machoni pangu, nayo nisiyo-
yapenda wameyachagua.
5 Sikieni neno la Yahuwa, mtetemekao kwa
neno lake, ndugu zenu waliowachukia wali-
owatupa kwa ajili ya jina langu, walinena,
atukuke Yahuwa, naye ataonekana kwa fu-
raha yenu, nao wataona haya.
6 Sauti ya uvumi katika mjini, sauti kati-
ka hekalu, sauti ya Yahuwa akilipa malipo
7 kwa adui zake. Mbele ya mimba, akazaa,
mbele ya kuja utungu wake, ametoa mume.
8 Nani aliyesikia kama hiyo, nani aliyeona
kama hiyo? Inchi izae kwa siku moja?
Taifa lizaliwe mara moja? Kwani Sayuni
9 akiona utungu amezaa waanawe. Mimi
nivunje wala sizalishe? amesema Yahu-
wa? Nifanye mimba nikafunge, amenena
Muungu wako?
10 Furahini pamoja na Yerusalemi mshangi-
lie nanyi nyote mmpendao, mfurahiwe pa-
11 moja naye kwa furaha nyote mmliliao. Mpa-



Digitized by Google Original from HARVARD UNIVERSITY

te kunyonya na kushibishwa na maziwa ya
faraja zake, mpate kukama na kufurahiwa
na fahari ya utukufu wake.
12 Kwani ndilo asemalo Yahuwa, Mimi ndi-
mi nimpitishaye amani kama mto, na kama
maji yafurikayo utukufu wa mataifa, mta-
nyonya, mtachukuliwa mbavuni, na juu ya
13 magote mtabembelezwa. Kama mtu ali-
yetulizwa na mama wake, hivi nitakutuliza
ninyi, na katika Yerusalemi mtapewa faraja.
14 Na mtaona, moyo wenu utafurahiwa, na
mifupa yenu kama miche itamea, utata-
mbulikana mkono wa Yahuwa pamoja na
watumwa wake, na ghathabu kwa adui za-
ke.
15 Kwani yuko Yahuwa, kwa moto yuaja,
na kama tufanu gari lake, alipe katika
hasira ghathabu yake, na kukemea katika
16 ndimi za moto. Kwani kwa moto Yahuwa
ahukumu, na kwa upanga wake, wenyi
mwili wote, na wengi waliojeruhi kwa Ya-
17 huwa. Wajitakasao, wajisafishao katika
bustani nyuma ya mmoja wa kati, walao
nyama ya nguruwe, na chukizo, na panya,



Digitized by Google
Original from
HARVARD UNIVERSITY

pamoja watakoma, amesema Yahuwa.
18 Nami matendo yao na mawazo yao, una-
kuja wa kukusanya mataifa wote, na ndimi,
19 watakuja, wataona utukufu wangu. Nita-
weka ishara kwao, nitapeleka waliovuka
kwa mataifa, Tarshishi, Puli, na Ludi,
wavutao upindi, Tubal, na Yawan, visiwa
vilivyoko mbali, wasiosikia habari zangu,
wala hawakuona utukufu wangu, nao wa-
tahubiri utukufu wangu kwa mataifa.
20 Nao wataleta ndugu zenu zote katika
mataifa yote, sadaka kwa Yahuwa, kwa
frasi, na kwa gari, na kwa machela, na kwa
nyumbu, na kwa nyama wepesi, hatta mli-
ma wa utakatifu wangu, Yerusalemi, ame-
nena Yahuwa, kama waletavyo waana wa
Israeli sadaka katika chombo kisafi, kwa
21 nyumba ya Yahuwa. Na tena wa hawa
nitatwaa kwa wakohani, kwa Walawi, ame-
22 sema Yahuwa. Kwani kama mbingu mpya
na inchi mpya nizifanyazo, zikaavyo mbele
yangu, amesema Yahuwa, hivi utakaa uzao
23 wenu na jina lenu. Itakuwa wakati wa
mwezi kwa mwezi, na wakati wa sabato



Digitized by Google Original from HARVARD UNIVERSITY

kwa sabato, watakuja wenyi mwili wote,
wainame mbele yangu, amenena Yahuwa.
24 Watatoka wataona mizoga ya watu walio-
nikosa, kwani mdudu wao hafi, wala moto
wao hauzimiki, watakuwa kuwachukiza we-
nyi mwili wote.



Digitized by Google

Original from
HARVARD UNIVERSITY

Bible Downloads:
DIGITAL BIBLE SOCIETY
www.dbs.org

THE BORROWER WILL BE CHARGED AN OVERDUE FEE IF THIS BOOK IS NOT RETURNED TO THE LIBRARY ON OR BEFORE THE LAST DATE STAMPED BELOW. NON-RECEIPT OF OVERDUE NOTICES DOES NOT EXEMPT THE BORROWER FROM OVERDUE FEES.

WIDENER
BOOK DUE
CANCELLED
AUG 10 1988
2734478

WIDENER
BOOK DUE
CANCELLED
SEP 10 1988
2762851

Digitized by Google
Original from
HARVARD UNIVERSITY